JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI

# TUME YA TAIFA YA MIPANGO







# MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2025/26





**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**
**TUME YA TAIFA YA MIPANGO**

# MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2025/26

# Yaliyomo


Orodha ya Vifupisho v

**SURA YA KWANZA**

Utangulizi 1
1.1 Usuli 2
1.2 Mawanda ya Utekelezaji wa Vipaumbele 3
1.3 Malengo ya Mpango 3
1.4 Utekelezaji na Ufuatiliaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2025/26 3
1.5 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2025/26 3
1.6 Maandalizi ya Mpango 4

**SURA YA PILI**

Hali ya Uchumi 7
2.1 Utangulizi 8
2.2 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda 8
2.2.1 Uchumi wa Dunia 8
2.2.2 Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 9
2.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia 10
2.2.4 Mfumuko wa Bei wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika 10
2.2.5 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki 11
2.3 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa 12
2.3.1 Uchumi wa Taifa 12
2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini 13
2.3.3 Sekta ya Nje 13
2.3.4 Sekta ya Fedha 14
2.3.5 Deni la Serikali 16
2.3.6 Demografia na Maendeleo ya Watu 16
*2.3.6.1 Demografia* 16
*2.3.6.2 Hali ya Ajira Nchini* 17
*2.3.6.3 Maendeleo ya Watu* 18
2.4 Mwenendo wa Sekta Binafsi 18
2.4.1 Ukuzaji wa Mitaji 19
2.4.2 Mitaji kutoka Nje 19
2.5 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025/26 20
2.5.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla 20
2.5.2 Misingi (Assumptions) ya Mpango kwa Mwaka 2025/26 20

**SURA YA TATU**


| | | | |
|---|---|---|---|
| | Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango | | 23 |
| 3.1 | Utangulizi | | 24 |
| 3.2. | Miradi ya Kielelezo | | 24 |
| | 3.2.1. | Miundombinu ya Usafirishaji | 24 |
| | 3.2.2 | Miradi ya Miundombinu ya Nishati | 26 |
| | 3.2.3 | Miradi ya Kuongeza Uzalishaji Viwandani | 28 |
| 3.3 | Programu na Miradi ya Kimkakati ya Kisekta | | 29 |
| | 3.3.1 | Sekta ya Ujenzi | 31 |
| | 3.3.2 | Sekta ya Uchukuzi | 32 |
| | 3.3.3 | Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | 34 |
| | 3.3.4 | Sekta ya Nishati | 36 |
| | 3.3.5 | Sekta ya Kilimo | 37 |
| | 3.3.6 | Sekta ya Mifugo | 38 |
| | 3.3.7 | Sekta ya Uvuvi | 40 |
| | 3.3.8 | Sekta ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani | 41 |
| | 3.3.9 | Sekta ya Madini | 43 |
| | 3.3.10 | Sekta ya Mazingira na Maliasili | 44 |
| | 3.3.11 | Sekta ya Utalii | 45 |
| | 3.3.12 | Sekta ya Sanaa, Michezo na Ubunifu | 46 |
| | 3.3.13 | Sekta ya Kukuza Uwekezaji na Biashara | 48 |
| | 3.3.14 | Sekta ya Uwekezaji wa Umma na Sekta Binafsi | 50 |
| | 3.3.15 | Sekta ya Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi | 50 |
| | 3.3.16 | Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi | 51 |
| | 3.3.17 | Sekta ya Afya | 55 |
| | 3.3.18 | Sekta ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira | 56 |
| | 3.3.19 | Sekta ya Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 58 |
| | 3.3.20 | Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii | 60 |
| | 3.3.21 | Kuendeleza Ujuzi | 61 |
| | 3.3.22 | Sekta ya Utawala Bora na Utawala wa Sheria | 62 |


**SURA YA NNE**


| | | | |
|---|---|---|---|
| Vipaumbele na Malengo kwa Mwaka 2025/26 | | | 69 |
| 4.1 | Utangulizi | | 70 |
| 4.2 | Vigezo vya Kuchagua Vipaumbele vya Mapendekezo ya Mpango | | 70 |
| 4.3 | Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi | | 70 |
| | 4.3.1 | Sekta ya Ujenzi | 70 |
| | 4.3.2 | Sekta ya Uchukuzi | 71 |
| | 4.3.3 | Sekta ya Nishati | 73 |
| | 4.3.4 | Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | 73 |
| 4.4 | Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma | | 74 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | 4.4.1 | Sekta ya Kilimo | 74 |
| | 4.4.2 | Sekta ya Mifugo | 75 |
| | 4.4.3 | Sekta ya Uvuvi | 76 |
| | 4.4.4 | Sekta ya Uzalishaji Viwandani | 77 |
| | 4.4.5 | Sekta ya Madini | 78 |
| | 4.4.6 | Sekta ya Utalii | 78 |
| | 4.4.7 | Sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo | 79 |
| 4.5 | Kukuza Uwekezaji na Biashara | | 81 |
| | 4.5.1 | Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Biashara | 81 |
| | 4.5.2 | Uwekezaji wa Sekta Binafsi | 82 |
| | 4.5.3 | Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi | 82 |
| 4.6 | Kuchochea Maendeleo ya Watu | | 83 |
| | 4.6.1 | Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi | 83 |
| | 4.6.2 | Sekta ya Afya | 83 |
| | 4.6.3 | Sekta ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira | 85 |
| | 4.6.4 | Sekta ya Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 86 |
| | 4.6.5 | Sekta ya Hifadhi ya Jamii | 87 |
| | 4.6.6 | Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii | 89 |
| | 4.6.7 | Sekta ya Utawala Bora na Utawala wa Sheria | 90 |
| | 4.6.8 | Sekta ya Mazingira na Maliasili Asilia | 92 |
| 4.7 | Kuendeleza Ujuzi | | 93 |

**SURA YA TANO**

| | | |
|---|---|---|
| | Ufuatiliaji, Tathmini na Vihatarishi | 97 |
| 5.1 | Utangulizi | 98 |
| 5.2 | Msingi wa Ufuatiliaji na Tathmini | 98 |
| 5.3 | Nguzo za Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini | 98 |
| 5.4 | Njia za Utekelezaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini | 99 |
| 5.5 | Muundo wa Kitaasisi wa Ufuatiliaji na Tathmini | 100 |
| 5.6 | Vihatarishi vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa | 101 |

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| **ADC** | Aquaculture Development Centres |
| **ADEM** | Agency for the Development of Educational Management |
| **AFCON** | Africa Cup of Nations |
| **AFDP** | Agriculture and Fisheries Development Programme |
| **AHSP** | Annual Health Sector Performance Report |
| **AMIS** | Airport Management Information |
| **ASDP II** | Agricultural Sector Development Programme II |
| **ATCL** | Air Tanzania Company Limited |
| **ATE** | Association of Tanzania Employers |
| **AU** | African Union |
| **BAKITA** | Baraza la Kiswahili Tanzania |
| **BBT** | Building Better Tomorrow |
| **BEVAC** | Beekeeping Value Chain |
| **BOOST** | Boost Primary Students' Learning |
| **CAMARTEC** | Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology |
| **CBE** | College of Business Education |
| **CBR** | Central Bank Rate |
| **CNG** | Compressed Natural Gas |
| **COSTECH** | Commission for Science and Technology |
| **DAWASA** | Dar es Salaam Water and Sewarage Authority |
| **DIT** | Dar es Salaam Institute of Technology |
| **DMDPII** | Dar es Salaam Metropolitan Development Project II |
| **DMGP** | Dar es Salaam Maritime Gateway Program |
| **DMI** | Dar es Salaam Maritime Institute |
| **DRC** | Democratic Republic of the Congo |
| **EAC** | East African Community |
| **EACOP** | East African Crude Oil Pipeline |
| **EASTRIP** | East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project |
| **EIA** | Environmental Impact Assessment |
| **EOCC** | Emergency Operations and Communication Centre |
| **EP4R** | Education Programme for Results |
| **EPZA** | Export Processing Zones Authority |
| **ETF** | Enhanced Transparency Framework |
| **FCC** | Fair Competition Commission |
| **FCT** | Fair Competition Tribunal |
| **FDCs** | Folk Development Colleges |
| **FOLUR** | Food Systems, Land Use and Restoration |
| **FORLAND** | Forestry, Land Use and Value Chains Development |
| **FYDP III** | Third Five Year Development Plan |
| **GAVI** | Global Alliance for Vaccines and Immunization |
| **GPE** | Global Partnership for Education |

| | |
|---|---|
| **Ha** | **Hectare** |
| **HBF** | **Health Basket Fund** |
| **HEET** | **Higher Education for Economic Transformation Project** |
| **HEP** | **Hamlet Electrification Project** |
| **ICHF** | **Improved Community Health Fund** |
| **IJCs** | **Integrated Justice Centers** |
| **ILFS** | **Integrated Labour Force Survey** |
| **IMF** | **International Monetary Fund** |
| **IWT** | Illegal Wildlife Trade |
| **JNHPP** | Julius Nyerere Hydropower Plant |
| **JNIA** | Julius Nyerere International Airport |
| **JPM** | John Pombe Magufuli |
| **KIA** | Kilimanjaro International Airport |
| **KM** | Kilometer |
| **KPI** | Key Performance Indicator |
| **KWh** | Kilowatt Hour |
| **LGAs** | Local Government Authorities |
| **LNG** | Liquefied Natural Gas |
| **LPG** | Liquefied Petroleum Gas |
| **LVD** | Lake Victoria to Dodoma |
| **MDAs** | Ministries, Departments and Agencies |
| **MICE** | Meetings, Incentives, Conferences and Exhibition |
| **MIT** | Ministry of Industry and Trade |
| **MoCU** | Moshi Co-operative University |
| **MW** | Megawatt |
| **NACTE** | National Council for Technical Education |
| **NCAA** | Ngorongoro Conservation Area Authority |
| **NCT** | National College of Tourism |
| **NDC** | National Development Corporation |
| **NEMC** | National Environment Managament Council |
| **NHC** | National Housing Corporation |
| **NHIF** | National Health Insuarance Fund |
| **NIDA** | National Identification Authority |
| **NIT** | National Institute of Transport |
| **NMT** | National Museum of Tanzania |
| **NPMIS** | National Project Management Information System |
| **NPS** | National Prosecuting Service |
| **NRW** | Non-Revenue Water |
| **PAMOJA** | Project for Advancing Gender Equality in Tanzania |
| **PCP** | Programme for Country Partnership |
| **PFMRP** | Public Finance Management Reform Programme |
| **PIM-OM** | Public Investment Management Operational Manual |
| **PPP** | Public-Private Partnership |
| **PPPC** | Public-Private Partnership Centre |
| **PSRP** | Public Service Reform Programme |
| **PSRS** | Public Service Recruitment Secretariat |
| **PSSN** | Productive Social Safety Net |
| **SADC** | Southern African Development Community |
| **SDGs** | Sustainable Development Goals |

| | |
|---|---|
| **SDL** | Skills Development Levy |
| **SEZ** | Special Economic Zones |
| **SGR** | Standard Gauge Railway |
| **SIDO** | Small Industries Development Organisation |
| **SMMRP** | Sustainable Management of Mineral Resources Project |
| **SPV** | Special Purpose Vehicle |
| **SRWSSP** | Sustainable Rural Water Supply and Sanitation Programme |
| **TaESA** | Tanzania Employment Services Agency |
| **TAFICO** | Tanzania Fishing Corporation |
| **TAISP** | Tanzania Agricultural Input Support Project |
| **TAKUKURU** | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| **TANAPA** | Tanzania National Parks |
| **TANIPAC** | Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination |
| **TANROADS** | Tanzania National Road Agency |
| **TANTRADE** | Tanzania Trade Development Authority |
| **TANZIS** | Tanzania Innovation Systems |
| **TASAF** | Tanzania Social Action Fund |
| **TaSUBa** | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo |
| **TATC** | Tanzania Automotive Technology Centre |
| **TAWA** | Tanzania Wildlife Management Authority |
| **TAWIRI** | Tanzania Wildlife Research Institute |
| **TAZAMA** | Tanzania Zambia Mafuta |
| **TAZARA** | Tanzania - Zambia Railway Authority |
| **TBC** | Tanzania Broadcasting Corporation |
| **TBS** | Tanzania Bureau of Standards |
| **TDHS-MIS** | Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey |
| **TEA** | Tanzania Education Authority |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TEMDO** | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization |
| **TFSRP** | Tanzania Food Systems Resilience Program |
| **TGC** | Tanzania Gemmological Centre |
| **TIC** | Tanzania Investment Centre |
| **TIRDO** | Tanzania Industrial Research and Development Organisation. |
| **TIRP II** | Tanzania Intermodal Railway Project II |
| **TMCHIP** | Tanzania Maternal and Child Health Program |
| **TPSF** | Tanzania Private Sector Foundation |
| **TUCTA** | Trade Union Congress of Tanzania |
| **U&T** | Ufuatiliaji na Tathmini |
| **UDSM** | University of Dar es Salaam |
| **UNFPA** | United Nations Population Fund |
| **UNICEF** | United Nations Children's Fund |
| **USD** | United States Dollar |
| **UVIKO–19** | Ugonjwa wa Virusi vya Korona–2019 |
| **VHF** | Very High Frequency |
| **VVU** | Virusi Vya Ukimwi |
| **WMA** | Weight and Measurement Agency |
| **WRRB** | Warehouse Receipt Regulatory Board |
| **WSDP** | Water Sector Development Programme |

SURA YA KWANZA

# *Utangulizi.*





## 1.1 Usuli

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 ni wa tano (5) na wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa 2021/22 – 2025/26 ambao una dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Mpango huu ni nyenzo ya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na mipango ya maendeleo ya mwaka mmoja mmoja ambapo unaainisha hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa hatua mbalimbali za maendeleo ikilinganishwa na malengo yaliyowekwa. Kwa msingi huo, Mpango huu utakamilisha masuala yaliyoibuliwa na Mipango mingine iliyopita pamoja na kuwa kiungo kwa ajili ya mipango ya muda wa kati na mfupi itakayofuata baada ya kuzinduliwa kwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/26 yamezingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mwelekeo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Mpango wa Muda Mrefu wa Maendeleo (2011/12 - 2025/26), Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Agenda ya Maendeleo ya Afrika 2063, Agenda 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu; Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Makubaliano mengine ya kimataifa na ya kikanda. Aidha, Mpango huu umezingatia matokeo ya mapitio ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taifa ya kila mwaka ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, maendeleo na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, mabadiliko ya tabianchi na mageuzi ya kidijitali yanayoendelea duniani.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango ni pamoja na: Kukua kwa Pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.1 kwa mwaka 2023; kuongezeka kwa mtandao wa barabara za vijijini na mijini kwa kiwango cha lami kufikia km 15,366.36 mwaka 2024/25 kutoka km 13,235.1 mwaka 2020/21; Uzalishaji wa umeme umeongezeka kutoka MW 2,373 mwaka 2023/24 kufikia MW 4,031.71 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa kiwango cha utoshelevu wa chakula nchini kufikia asilimia 128 mwaka 2024/25 kutoka asilimia 124 mwaka 2023/24; mchango wa uzalishaji wa bidhaa viwandani katika mauzo yote nje umeongezeka kutoka asilimia 21.6 mwaka 2023/24 hadi asilimia 39 mwaka 2024/25; mchango wa madini katika jumla ya mapato ya fedha za nje umeongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 3,551.4 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,395.3 mwaka 2022/23; idadi ya watalii imeongezeka kufikia 5,360,247 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na watalii 3,784,214 mwaka 2023/24; thamani ya miradi ya uwekezaji na biashara imeongezeka na kufikia dola

**2024** 2023
▲ 5.5% | ▼ 5.1%
*Kiwango cha ongezeko la kwa pato la taifa*

▲ 15,366 km **2024**
▼ 13,235 km 2023
*Mtandao wa barabara za vijijini umeongezeka*

▲ 4,031 mw **2024**
▼ 2,373 mw 2023
*Kiwango cha uzalishaji umeme kimeongezeka*

128% ▲ **2024**
*Kiwango cha utoshelevu wa chakula kimeongezeka*

39% ▲ **2024**
*Kiwango cha mchango wa uzalishaji wa bidhaa kilichoongezeka*

**2023/ 2024**
$3,551 mil
*Kiwango cha mchango wa madini katika fedha za kigeni*

za Marekani milioni 8,813 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6,796.09 mwaka 2023/24; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu waliopata mikopo na kufikia 250,567 mwaka 2024/25 ikilinganishwa wanafunzi 220,278 mwaka 2023/24; asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba au maji yaliyolindwa imeongezeka kutoka asilimia 79.6 mwaka 2023/24 hadi asilimia 83 mwaka 2024/25. (Mafanikio ya utekelezaji wa mipango kwa sekta zote yameainishwa katika sura ya Tatu).

## 1.2 Mawanda ya Utekelezaji wa Vipaumbele

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26 umejikita katika maeneo ya kipaumbele ya kitaifa yafuatayo: kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza ujuzi. Maeneo haya ya kipaumbele yamelenga kuhakikisha mwendelezo wa Mipango ya muda wa kati ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ya kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati na ustawi wa juu wa watu. Uainishaji wa programu na miradi ya vipaumbele kwa mwaka 2025/26 umezingatia hatua za utekelezaji katika kufikia malengo yaliyoainishwa katika mipango ya kisekta, taarifa za tafiti na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022; na mabadiliko ya mwenendo wa kiuchumi na kijamii.

## 1.3 Malengo ya Mpango

Lengo kuu la Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 ni kutekeleza malengo yaliyowekwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ili kufikia azma ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Hivyo, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/26 umelenga kukamilisha programu na miradi ya maendeleo ya kielelezo na kimkakati pamoja na kuendelea kuwekeza katika maeneo yenye uwezo wa kuchochea ukuaji wa sekta za uzalishaji.

Aidha, Mpango huu utaweka mkazo katika kuimarisha miundombinu, kuendeleza rasilimali watu, kuongeza ushirikiano kati ya sekta za umma na binafsi, kuongeza uwekezaji katika masuala ya utafiti, sayansi, na teknolojia.

## 1.4 Utekelezaji na Ufuatiliaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2025/26

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 utazingatia utaratibu na miongozo ya Serikali kama ilivyoelekezwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Utaratibu huu umekuwa ukitolewa maelekezo kupitia miongozo ya mipango na bajeti ya kila mwaka ambapo Tume ya Taifa ya Mipango itakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wake.

## 1.5 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2025/26

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26 utagharamiwa kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato vinavyohusisha rasilimali za ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2025/26, Serikali itatenga jumla ya shilingi bilioni 18,921 sawa na asilimia 33.5 ya Bajeti Kuu ya

Serikali ya shilingi bilioni 56,490.3 kwa ajili ya kugharamia programu na miradi ya maendeleo ikilinganishwa na shilingi bilioni 15,959.36 sawa na asilimia 31.7 ya Bajeti Kuu ya Serikali ya shilingi bilioni 50,291.4 kwa mwaka 2024/25. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 14,045.5 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 4,875.9 ni fedha za nje kutoka vyanzo mbalimbali. Vilevile, Serikali inalenga kuongeza ushirikiano na mchango wa sekta binafsi katika kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia njia bunifu na mbadala za kugharamia miradi hiyo. Njia hizi zitajumuisha matumizi ya utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) pamoja na utoaji wa dhamana za maendeleo kupitia masoko ya mitaji, lengo ni kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi muhimu ya maendeleo ambayo ni kichocheo kikuu cha ukuaji wa uchumi wa taifa. Kwa ujumla, Serikali itahakikisha rasilimali fedha zinatumika kwa tija ili kuimarisha ustawi wa wananchi na maendeleo endelevu ya kiuchumi.




**2024/2025**
*Kiwango cha asilimia kutoka bajeti kuu ya serikali kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo*

## 1.6 Maandalizi ya Mpango

Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026 yamehusisha wadau mbalimbali kama vile, wizara, idara zinazojitegemea, sekretariati za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, taasisi, mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kiraia, mashirika ya umma na sekta binafsi. Aidha, njia mbalimbali zimetumika katika ushirikishwaji wa makundi haya tajwa ikiwemo vikao vya majadiliano, uandishi na uhariri. Vilevile, wadau wa maendeleo watashirikishwa katika utekelezaji kupitia majadiliano kwenye maeneo mahsusi ya ushirikiano, ufadhili wa miradi ya maendeleo na programu za kisekta. Takwimu zilizoainishwa katika Mpango zimetokana na tafiti, taarifa za utekelezaji za sekta, machapisho mbalimbali ya kisayansi na kitaalamu ya ndani na nje ya nchi.



**Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 una dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu"**





SURA YA PILI

# *Hali ya Uchumi.*

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mwenendo wa viashiria vya uchumi wa dunia, kikanda na kitaifa kwa mwaka 2024 pamoja na mwelekeo kwa mwaka 2025. Uchambuzi wa viashiria vya uchumi na mwenendo wake ni muhimu katika kupanga maendeleo ya taifa kwa kuwa inawezesha kulinganisha mwenendo wa uchumi wa nchi na uchumi wa dunia kwa ajili ya kupendekeza sera sahihi. Aidha, uchambuzi wa viashiria vya uchumi jumla unajenga msingi imara wa kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26. Viashiria vilivyofanyiwa mapitio ni pamoja na: Pato la Taifa; mfumuko wa bei; mwenendo wa sekta ya nje; sekta ya fedha; deni la Serikali; na demografia na maendeleo ya watu.

## 2.2 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda

### 2.2.1 Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Aprili, 2025 kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imeendelea kupungua hadi kufikia asilimia 3.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023. Upungufu huo ulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo athari za utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika kukabiliana na mfumuko wa bei; migogoro ya kisiasa hususan Ulaya Mashariki na Mashariki ya Kati; gharama kubwa za mikopo katika masoko ya fedha zilizoathiri zaidi nchi zinazoendelea; na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa upande mwingine, taarifa ya IMF imeonesha kuwa, ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kuendelea kupungua na kufikia asilimia 2.8 kwa mwaka 2025.

**Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Matarajio, 2019 – 2025**




***Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF - WEO), Aprili 2025.*

### 2.2.2 Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili, 2025 kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa kwa nchi za ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ulikuwa asilimia 1.5 na asilimia 3.1 ikilinganishwa na wastani wa ukuaji wa asilimia 5.2 na asilimia 3.9 mwaka 2023 mtawaliwa. Kupungua kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kulitokana na migogoro ya kisiasa ikiwemo migororo inayoendelea nchini DRC na Sudani ambapo kumekuwa na ukuaji hasi wa asilimia 27.6 kwa Sudani Kusini. Aidha, athari za mabadiliko ya tabianchi zimepunguza ukuaji wa uchumi kwenye baadhi ya nchi za jumuiya hizo ikiwemo Malawi, Msumbiji na Sudani Kusini kufuatia hali ya ukame na mafuriko iliyoleta athari kubwa katika sekta za kilimo, miundombinu na maisha ya watu. Aidha, kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa jumuiya hizo kinatarajiwa kufikia asilimia 2.7 kwa EAC na asilimia 3.5 kwa SADC kwa mwaka 2025 kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na.1.2 na 1.3.**




***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Aprili 2025*

**Kielelezo Na. 1.3: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), 2022 - 2025**




***Chanzo:*** *: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Aprili 2025 na Tovuti za Ofisi za Takwimu*

## 2.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili, 2024, mfumuko wa bei wa dunia ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2023. Hali hii ilitokana na kuimarika kwa bei za bidhaa na huduma duniani kulikotokana na utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kupunguza ongezeko la ukwasi na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia hususan mafuta na mbolea. Aidha, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua na kufikia asilimia 4.3 mwaka 2025 na asilimia 2.2 mwaka 2026. Mfumuko wa bei kwa nchi zenye kipato cha chini uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 18.3 mwaka 2024 ikilingananishwa na wastani wa asilimia 17.4 mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 7.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.0 mwaka 2023. Vilevile, mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2023.

## 2.2.4 Mfumuko wa Bei wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili, 2025 nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, Mfumuko wa bei kwa nchi hizo umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 18.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 17.6 mwaka 2023. Ongezeko

*Mfumuko wa bei ya dunia*

**2024** 2023
▼ 5.8% | ▲ 6.7%

▼ 4.3% | ▼ 2.2%
**2025** **2026**

*Mfumuko wa bei ya dunia wa nchi zenye kipato cha chini*

**2024** 2023
▼ 18.3% | ▲ 17.4%

*Mfumuko wa bei ya dunia kwa nchi zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi*

**2024** 2023
▼ 7.7% | ▲ 8.0%

*Mfumuko wa bei ya dunia kwa nchi zilizoendelea kiuchumi*

**2024** 2023
▼ 2.6% | ▲ 4.6%

la mfumuko wa bei lilitokana na sababu mbalimbali ikiwemo athari za kushuka kwa thamani ya fedha pamoja na uzalishaji usioridhisha katika shughuli za kilimo. Nchi zilizokuwa na mfumuko wa bei wa juu ni pamoja na Zimbwabwe (asilimia 736.1), Sudan Kusini (asilimia 128.4), Nigeria (asilimia 33.2), Malawi (asilimia 32.2) na Angola (asilimia 28.2). Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikuwa wastani wa asilimia 62.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 52.4 mwaka 2023.

### 2.2.5 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili, 2025 mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki, umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 23.45 mwaka 2024 kutoka asilimia 15.5 mwaka 2023. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo kupungua kwa uzalishaji wa chakula kulikosababishwa na mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la gharama za usafirishaji. **Kielelezo Na.1.4** kinaonesha mfumuko wa bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Kielelezo Na. 1.4: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mwaka 2023 - 2024 na Matarajio Mwaka 2025**




| | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|
| Tanzania | 3.8 | 3.1 | 4 |
| Kenya | 7.7 | 4.5 | 4.1 |
| Somalia | 6.2 | 5.5 | 4.6 |
| Burundi | 27.1 | 20.2 | 39.6 |
| Rwanda | 14 | 4.8 | 7 |
| DRC | 19.9 | 17.7 | 8.9 |
| Uganda | 5.4 | 3.3 | 4.2 |
| Sudan Kusini | 39.7 | 128.4 | 65.7 |

***Chanzo:*** *Ofisi za Taifa za Takwimu za Nchi husika na IMF*

## 2.3 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa

### 2.3.1 Uchumi wa Taifa

Katika mwaka 2024, Pato halisi la Taifa kwa bei za mwaka 2015 lilifikia shilingi bilioni 156,635.32 ikilinganishwa na shilingi bilioni 148,521.02 mwaka 2023, sawa na ukuaji wa asilimia 5.5 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo: kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere; kuendelea na utekelezaji endelevu wa miradi ya kimkakati na ya kielelezo inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; usimamizi madhubuti wa sera za fedha; hali nzuri ya hewa iliyoimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo; na uwekezaji wa Serikali katika huduma za jamii, ikiwemo elimu, afya, maji na hifadhi ya jamii.

Aidha, sekta ya sanaa na burudani iliendelea kuongoza kwa kuwa na ukuaji wa asilimia 17.1, ikifuatiwa na sekta ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme asilimia 14.4, habari na mawasiliano asilimia 14.3 pamoja na sekta ya fedha na bima asilimia 13.8. Hata hivyo, shughuli za kilimo ziliendelea kuongoza kwa kuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa wa asilimia 26.3 ikifuatiwa na ujenzi asilimia 12.8 na uchimbaji madini na mawe asilimia 10.1. Hali hii inaonesha umuhimu wa sekta ya kilimo katika uchumi wa nchi pamoja na kuwa na ukuaji mdogo wa asilimia 4.1 mchango wake kwenye Pato la Taifa umeendelea kuwa na umuhimu kwa kusaidia katika upatikanaji wa chakula, malighafi za viwanda, mauzo nje ya nchi na kutoa ajira kwa watu wengi hususan vijana kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na.1.5 na 1.6.**

**Kielelezo Na. 1.5: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi (Asilimia) kwa mwaka 2023 na 2024**




***Chanzo:*** *Takwimu za Pato la Taifa kwa Mwaka 2024, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)*

*Pato Halisi la Taifa*

**156 bil** ▲ 2024

**148 bil** ▼ 2023

*Sekta ya sanaa*
**17.1%** ▲

*Sekta ya Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji Umeme*
**14.4%** ▲

*Sekta ya Habari na Mawasiliano*
**14.3%** ▲

*Sekta ya Fedha na Bima*
**13.8%** ▲

*Sekta ya Ujenzi*
**12.8%** ▲

*Sekta ya Madini*
**10.1%** ▲

**Kielelezo Na. 1.6: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa Mwaka 2024 (Asilimia)**




***Chanzo:*** *Takwimu za Pato la Taifa kwa Mwaka 2024, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)*

## 2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini

Wastani wa mfumuko wa bei ulipungua na kufikia asilimia 3.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2023. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei ulipungua kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti, kutengemaa kwa bei za mafuta katika soko la dunia na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani. Viwango vya mfumuko wa bei nchini bado vipo ndani ya malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kutokuzidi asilimia 8.0 na malengo ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya kuwa kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0.

## 2.3.3 Sekta ya Nje

### a. Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa na Huduma

Sekta ya nje imeendelea kuimarika sambamba na kuimarika kwa uchumi wa dunia. Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, na huduma ilipungua hadi dola za Marekani milioni 866.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,196.5 mwaka 2023. Kupungua huku kulitokana na kuimarika kwa urari wa biashara ya huduma.

Katika mwaka 2024 thamani ya mauzo ya bidhaa ilikuwa dola za Marekani milioni 9,121.6 ikilinganishwa na dola za Marekani 7,696.6 mwaka 2023. Aidha, thamani ya mauzo ya huduma nje ya nchi ilifikia dola za Marekani milioni 6,899.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6,231.7 mwaka 2023. Vilevile, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje

*Wastani wa Mfumuko wa bei ya nchini*

**2024** ▼ 3.1% | 2023 ▲ 3.8%

*Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa*

**$866.7 mil** ▼

**$2,196 mil** ▲
2023

*Thamani ya mauzo ya bidhaa katika dola za kimarekani*
**2024**

**$9,121 mil** ▲

**$7,696 mil** ▼
2023

*Thamani ya mauzo ya huduma nje ya nchi*
**2024**

**$6,899 mil** ▲

**$6231 mil** ▼
2023

iliongezeka kwa asilimia 4.0 na kufikia dola za Marekani milioni 14,278.9 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 13,728.9 mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji.

b. **Mwenendo wa Biashara ya Huduma**

Katika kipindi cha mwaka 2024, mapato yatokanayo na huduma nje ya nchi yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 6,899.4, sawa na ongezeko la asilimia 10.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6,231.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Ongezeko hili lilichangiwa na kuimarika kwa mapato ya utalii na usafirishaji. Ongezeko la mapato ya utalii lilitokana na ukuaji wa sekta ya utalii, ambapo idadi ya watalii walioingia nchini iliongezeka na kufikia watalii 2,141,895 katika kipindi cha mwaka 2024, ikilinganishwa na watalii 1,808,205 kwa kipindi kama hicho mwaka 2023.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2024, malipo ya huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 8.9, kufikia dola za Marekani milioni 2,608.9 kutoka dola za Marekani milioni 2,395.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Hii ilitokana na kuongezeka kwa malipo ya huduma za usafirishaji na ongezeko la malipo ya huduma za usafiri nje ya nchi na huduma nyinginezo.

c. **Akiba ya Fedha za Kigeni**

Hadi Desemba 2024, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,546.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,440.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Kiasi hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa kipindi cha miezi 4.4, ambayo ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.0. Ongezeko hili lilichangiwa na utekelezaji wa programu ya Benki Kuu ya ununuzi wa dhahabu nchini, pamoja na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yaliyotokana na kuongezeka kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia, idadi ya watalii nchini na mauzo ya mazao ya biashara hususan korosho na tumbaku.

### 2.3.4 Sekta ya Fedha

Katika kipindi cha mwaka 2024/25, Serikali ililenga kuhakikisha ukwasi wa fedha unabaki katika kiwango kinachochagiza ukuaji wa uchumi kwa kutumia mfumo wa ujazi wa fedha ili kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kuhakikisha uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni. Hii inatokana na utekelezaji wa sera ya fedha yenye kuongeza ufanisi ili kuendana na mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi.

Katika mwaka 2024, Serikali ilianza kutekeleza mfumo wa riba ya Benki Kuu kwa kuzingatia maoteo ya mfumuko wa bei na mwenendo wa hali ya uchumi ambapo riba ya Benki Kuu ya asilimia 5.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2024 iliongezeka na kufikia asilimia 6 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2024 ili kudhibiti athari za kushuka kwa thamani ya shilingi kwenye mfumuko wa bei. Utekelezaji wa sera ya fedha kwa kutumia riba

*Mapato yatokananayo na huduma nje ya nchi*
**$6,899 mil ▲** 2024
**$6,231 mil ▼** 2023

*Idadi ya Watalii kutoka nje*
2024 **2.14 mil ▲**
**1.80 mil ▼** 2023

*Malipo ya huduma nje ya nchi*
2024 **$2,608 mil ▲**
**$2,395 mil ▼** 2023

*akiba ya fedha za kigeni*
2024 **$5,546 mil ▲**
**$5,440 mil ▼** 2023

ya Benki Kuu ulikuwa wa kuridhisha na ulifanikiwa kuhakikisha kuwa riba ya siku 7 katika soko la fedha baina ya mabenki inakuwa tulivu, ndani ya wigo usiozidi asilimia 2 chini au juu ya riba ya Benki Kuu. Hali hii inaashiria uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi kinachoendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi.

a. **Viwango vya Riba**

Mwaka 2024,wastani wa riba ya jumla katika soko la fedha baina ya benki iliongezeka na kufikia asilimia 7.5 ikilinganishwa na asilimia 5.37 kwa mwaka 2023. Aidha, wastani wa riba za jumla za dhamana za Serikali za muda mfupi ziliongezeka hadi wastani wa asilimia 10.67 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 7.32 mwaka 2023. Hali hii ilitokana na kupungua kwa ukwasi (tight financial conditions) katika masoko ya fedha, kama ilivyokuwa katika benki kuu za nchi nyingine kutekeleza sera ya fedha ili kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei.

Riba za mikopo kwa ujumla zilipungua hadi wastani wa asilimia 15.47 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 15.75 mwaka 2023. Riba za amana ziliongezeka hadi kufikia asilimia 9.17 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 8.65 mwaka 2023. Ongezeko hili lilitokana na kupungua kwa ukwasi katika benki.

b. **Mikopo kwa Sekta Binafsi**

Mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha mwaka 2024. Katika mwaka 2024 ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia wastani wa asilimia 12.4. Mwenendo huu unatokana na ongezeko la mahitaji ya mikopo mipya sambamba na kuimarika kwa uchumi wa dunia na nchi..

Aidha, mikopo kwa sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 41.0, kutokana na matokeo ya hatua za kisera zilizolenga kushusha viwango vya riba pamoja na juhudi za Serikali kuongeza bajeti katika sekta ya kilimo. Vilevile, mikopo katika shughuli binafsi ilikua kwa asilimia 14.7, sekta ya biashara (asilimia 12.7), uzalishaji viwandani (asilimia 16.3), ujenzi (asilimia 4.4), na uchukuzi na mawasiliano (asilimia 13.2).

Matokeo hayo yanaonesha mwelekeo chanya katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta mbalimbali nchini. Ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, hususan katika sekta za kilimo, viwanda na uzalishaji, pamoja na uchimbaji madini, linaashiria uimarishaji wa mazingira ya biashara na ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Hatua za kisera zilizolenga kupunguza viwango vya riba na kuongeza bajeti katika sekta muhimu hususan kilimo zimeonekana kuwa na matokeo chanya katika kuchochea ukuaji huo.

c. **Ukwasi na Faida za Biashara katika Benki**

Mwaka 2024, hali ya ukwasi katika sekta ya benki iliendelea kuwa ya kuridhisha, ikiwa juu ya ukomo unaokubalika kisheria. Aidha, mikopo chechefu ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024, ikilinganishwa na asilimia 4.3 mwaka 2023. Kupungua kwa mikopo chechefu kulitokana na hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu zikiwemo kuzielekeza benki kutumia taarifa za wakopaji kutoka kwa kampuni za kuchakata na kutunza kumbukumbu za mikopo; na kuzitaka benki na taasisi za fedha kuimarisha taratibu za utoaji na ufuatiliaji wa mikopo. Aidha, mwaka 2024, uwiano wa mtaji halisi na mtaji mkuu kwa mali hatarishi ulikuwa asilimia 19.3 na asilimia 19.9 ikilinganishwa na asilimia 17.7 na asilimia 18.4 mtawalia katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

### 2.3.5 Deni la Serikali

Hadi Machi 2025, deni la Serikali la nje lilifikia dola za Marekani milioni 26,670.32 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 23,720.86 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 12.4. Ongezeko hilo lilitokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo ya zamani na mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, Mashirika ya Fedha ya Kimataifa yaliendelea kuongoza kwa kuchangia asilimia 67.8 ya deni lote la nje ikilinganishwa na asilimia 63.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Benki za biashara zilichangia asilimia 26.9 na Washirika wa Maendeleo walichangia asilimia 5.3 ya deni lote la nje.

### 2.3.6 Demografia na Maendeleo ya Watu

#### *2.3.6.1 Demografia*

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, idadi ya watu Tanzania imeendelea kuongezeka kutoka watu 44,928,923 mwaka 2012 hadi watu 61,741,120 mwaka 2022. Ukuaji huo unatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na kasi ya ongezeko la idadi ya watu ya wastani wa asilimia 3.2 kwa mwaka. Katika ukuaji huu, idadi ya watu Tanzania Bara inakadiriwa kuwa 64,241,822 mwaka 2024, kati ya idadi hiyo wanawake ni 32,756,383 sawa na asilimia 51 na wanaume ni 31,485,439 sawa na asilimia 49. Idadi ya watu walio katika umri wa kufanya kazi (15-64) Tanzania Bara ni 33,764,430 sawa na asilimia 52.6. Idadi ya vijana (15-35) ni 21,695,045 sawa na asilimia 33.8; na idadi ya wanawake walio katika umri wa kuzaa (15-49) ni 15,257,789 sawa na asilimia 46.6. Aidha, idadi ya watu Tanzania Bara inatarajiwa kuongezeka na kufikia watu 66,054,123 mwaka 2025 na watu 67,877,764 mwaka 2026. Viashiria hivi vya idadi ya watu vinakadiriwa kuwa katika uwiano uliobainishwa mpaka mwaka 2026, ambapo utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 utahitimishwa na kuanza kwa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Mwenendo wa viashiria hivi unaonesha kutobadilika kwa muundo wa idadi ya watu (population pyramid) nchini, kuendelea kuwepo kwa viwango vikubwa vya uzazi, utegemezi na viwango vidogo vya kutoka katika umaskini, hivyo kuendelea kuwa na muundo wa idadi ya watu wenye idadi kubwa ya watoto na vijana ambao bado wapo shule.

**Kielelezo Na. 1.7: Jumla ya Idadi ya Watu Tanzania Bara wenye sifa mbalimbali, 2023-2026 ('000000')**




***Chanzo:*** *Ripoti ya Makadirio ya Idadi ya Watu Kitaifa (2024), Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha makundi yote ya watu yanapata huduma bora, ili kuwa na idadi ya watu yenye ubora na tija kwa uchumi na jamii. Jitihada hizo ni pamoja na uboreshaji wa huduma za afya, elimu, ujuzi, lishe, uwezeshaji wananchi kiuchumi, na miundombinu.

### *2.3.6.2 Hali ya Ajira Nchini*

Serikali imeendelea kuzalisha fursa mpya za ajira kutokana na mipango na mikakati ya maendeleo inayotekelezwa katika kukuza ajira nchini. Kwa kutumia tafsiri mpya ya Ajira inayosema: "Ajira mpya hutokea pale mfanyakazi anapoajiriwa kujaza nafasi iliyo wazi au nafasi mpya iliyoundwa kutokana na ukuaji wa shughuli za taasisi au uboreshaji wa mgawanyo wa majukumu kwenye taasisi au kujiajiri katika sekta rasmi na isiyo rasmi". Katika kipindi cha kuanzia Novemba 2020 hadi Februari 2025 jumla ya ajira 8,084,204 zilizalishwa katika sekta rasmi na isiyo rasmi nchini. Kati ya ajira zilizozalishwa, wanaume walikuwa 4,125,987 (asilimia 51.0) na wanawake walikuwa 3,958,218 (asilimia 49.0) ya ajira zote zilizozalishwa kwa kipindi husika. Aidha, kiasi cha ajira 1,047,179 (asilimia 13.0) zilizalishwa katika sekta rasmi, na ajira 7,037,024 (asilimia 87.0) zilizalishwa katika sekta isiyo rasmi.

**Kielelezo Na. 1.8 Idadi ya Ajira Zilizozalishwa katika Kipindi cha Mwaka 2020 hadi 2024**




***Chanzo:*** *Ofisi ya Waziri Mkuu kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu*




*Kiwango cha Ajira kilichozalishwa katika Sekta Rasmi na isiyo Rasmi*



### *2.3.6.3 Maendeleo ya Watu*

Serikali imeendelea kuboresha maendeleo ya watu ili kufikia matamanio yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Juhudi hizo ni pamoja na: kuendelea kutoa elimu ya msingi na sekondari bila ada; kuendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kupitia ujenzi wa miundombinu katika taasisi za elimu nchini; kuendelea kuongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; kuendelea kuboresha upatikanaji wa maji mijini na vijijini; kuendelea na ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali; na kuendelea na ujenzi wa barabara za kufungua fursa za kiuchumi katika maeneo ya mijini na vijijini. Kutokana na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo, kumekua na matokeo chanya katika viashiria vya maendeleo ya watu ikiwemo:

i. Kuongezeka kwa makadirio ya wastani wa umri wa kuishi kwa Tanzania Bara kutoka miaka 67.8 mwaka 2023 hadi miaka 68.0 mwaka 2024. Hii ni kwa mujibu wa makadirio ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022;

ii. Vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 81 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20 hadi kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2022/23[1];

iii. Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019/20 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022/23;

iv. Kujengwa kwa vituo 1,254 vya kutolea huduma ya afya mwaka 2024 kutoka vituo 1,126 mwaka 2023 hivyo, kuongeza upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi;

v. Kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kufikia asilimia 86.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 75.6 mwaka 2023;

vi. Kuongezeka kwa idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu kutoka asilimia 79.6 mwaka 2023/24 hadi kufikia asilimia 83 mwaka 2024/25;

vii. Kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami kutoka km 13,235.1 mwaka 2020 hadi km 15,366.36 mwaka 2024; na

viii. Kuunganishwa na huduma ya umeme kwa vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara mwaka 2024/25.

*wastani wa umri*

**68.0** ▲ **2024**

67.8 ▼ 2023

*vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano*

**43** ▼ **2024** | **81** ▲ 2020

*vifo vitokanavyo na uzazi*

**104** ▼ **2024** | **556** ▲ 2020

*ujenzi wa vituo vya afya*




*upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi*

**86%** ▲ **2024** | **75.6%** ▼ 2023

## 2.4 Mwenendo wa Sekta Binafsi

Malengo ya Tanzania ni kufikia hadhi ya nchi yenye kipato cha kati ifikapo mwisho wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, kupitia ukuaji endelevu wa uchumi unaochochewa na mageuzi ya kisera yanayotoa kipaumbele kwa ushiriki wa sekta binafsi. Tanzania imejipanga vyema kutumia utulivu wa kisiasa na uwepo wa maliasili ili kuvutia uwekezaji

1 Takwimu za afya zinatokana na Utafiti wa Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey ya mwaka 2022. Aidha, maelezo haya yanatumika pia kwa kipengele na. iii

wa ndani na nje ya nchi. Ushiriki wa sekta binafsi umeleta manufaa makubwa, ikiwa ni pamoja na kuongeza fursa za ajira, kuchochea shughuli za kibiashara, na kuboresha urari wa malipo. Manufaa haya yanachangia kufanikisha lengo la kujenga uchumi shindani na wa viwanda, kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

### 2.4.1 Ukuzaji Rasilimali

Mwaka 2024, ukuzaji wa rasilimali kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 76,301.64 kutoka shilingi milioni 69,226.05 mwaka 2023. Ongezeko hili lilichangiwa na ujenzi wa majengo, barabara, madaraja, na miradi mingine ya miundombinu. Katika kipindi hicho, uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika ulikuwa asilimia 37.1 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Mwaka 2024, ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 77,126.78 kutoka shilingi bilioni 71,482.46 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.9.

### 2.4.2 Mitaji kutoka Nje

Kwa mujibu wa Taarifa ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2024, uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 3.9 na kufikia dola za Marekani milioni 23,042.5 mwaka 2023. Katika ya uwekezaji huo,uwekezaji wa moja kwa moja ulikuwa dola za Marekani milioni 19,139.6, sawa na asilimia 83.1 ya uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje, uwekezaji wa hisa ulifikia dola za Marekani milioni 204.3 (asilimia 0.9) na uwekezaji mwingine ulifikia dola za Marekani milioni 3,698.6 (asilimia 16.1). Aidha, mitaji iliyowekezwa na sekta binafsi kutoka nje ya nchi kwa bei za miaka husika ilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,694.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,745.8 zilizowekezwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 2.9.

Mwaka 2023, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ulikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,648.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,437.6 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 14.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato na muunganiko na ununuzi wa kampuni za kimataifa pamoja na kuimarika kwa ugharamiaji wa miradi ya kimataifa. Aidha, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliongezeka ambapo nchi za OECD zilikuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wa asilimia 42.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 42.7 mwaka 2022. Vilevile, mchango wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje wa nchi za EAC na SADC ulikuwa asilimia 30.0 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 18.0 mwaka 2022. Nchi za Mauritius na Afrika Kusini zilichangia zaidi katika uwekezaji kutoka nchi za SADC na Kenya ilichangia zaidi katika uwekezaji kutoka nchi za EAC.

### Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi

Mwaka 2023, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliendelea kujikita zaidi katika shughuli za uchimbaji madini na mawe, fedha na bima pamoja na uzalishaji viwandani. Shughuli hizo zilichangia wastani wa asilimia 70.4 ya uwekezaji wote wa moja kwa moja kutoka nje. Aidha, shughuli za uchimbaji madini na mawe zilikuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 532.5, sawa na asilimia 32.3 ya uwekezaji wote, ikifuatiwa na uzalishaji viwandani wenye thamani ya dola za Marekani milioni 361 (asilimia 21.9) na shughuli za fedha na bima zenye thamani ya dola za Marekani milioni 267.6 (asilimia 16.2) mwaka 2023.

## 2.5 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025/26

Kwa kuzingatia mapitio ya hali ya uchumi kama ilivyoanishwa katika sehemu 2.2, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26 unalenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kupanua wigo wa ujumuishi wa jamii katika shughuli za kiuchumi, kuongeza kasi ya mageuzi ya uchumi na kuondoa umaskini, kuongeza mapato yatokanayo na fedha za kigeni na kuweka mkazo kwenye shughuli za uchumi zinazozalisha ajira kwa wingi na kuchochea ustawi kwa Watanzania wote ikiwemo kukamilisha miradi inayoendelea ili ianze kutoa huduma kwa Watanzania kwa ufanisi.

### 2.5.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla

Malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

i. Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.0 mwaka 2025 kutoka ukuaji wa asilimia 5.5 mwaka 2024;
ii. Mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja wa wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;
iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 16.7 ya Pato la Taifa ifikapo 2025/26 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.8 mwaka 2024/25
iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.3 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2025/26 kutoka matarajio ya asilimia 12.8 mwaka 2024/25;
v. Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 3.0 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2025/26 kutoka matarajio ya asilimia 3.4 mwaka 2024/25; na
vi. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

### 2.5.2 Misingi (Assumptions) ya Mpango kwa Mwaka 2025/26

Mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yamejegwa katika misingi ifuatayo:

i. Uwepo wa demokrasia, amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi na katika nchi jirani;
ii. Kuendelea kudumisha utawala bora na utawala wa sheria nchini;
iii. Kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini;
iv. Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara;
v. Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili (ikiwemo ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko ).




Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha makundi yote ya watu yanapata huduma bora



SURA YA TATU

# *Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango*



## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na ile ya kimkakati katika mwaka 2024/25. Miradi ya kielelezo inajumuisha miradi ambayo utekelezaji wake utaleta matokeo makubwa kitaifa, wakati miradi ya kimkakati ni ile inayotekelezwa na sekta ikiwa na lengo la kukuza uchumi na kutoa huduma kwa jamii. Sura hii pia inatoa kwa kina hatua zilizochukuliwa, matokeo ya hatua za utekelezaji na manufaa mapana kwa Taifa.

## 3.2. Miradi ya Kielelezo

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kutekeleza miradi 17 ya kielelezo inayolenga kuleta matokeo katika maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Kati ya miradi hiyo kuna miradi ambayo ipo katika hatua za mwisho za (kwa sehemu imeanza kutumika), miradi inayoendelea na ambayo ipo katika hatua za awali. Miradi ya kielelezo kwa sehemu kubwa ni ya miundombinu ya usafiri na usafirishaji, nishati na miradi ya kuongeza uzalishaji viwandani.

### 3.2.1. Miundombinu ya Usafirishaji

Miradi ya miundombinu ya uchukuzi ni ile inayohusiana na ujenzi ikiwemo barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege kwa ajili ya kutolea huduma za uchukuzi. Katika eneo hili Serikali imetekeleza miradi ifuatayo:

i. **Ujenzi wa Madaraja ya Juu**

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imetekeleza miradi ya ujenzi wa madaraja ya juu ambayo ujenzi wake utachochea shughuli za kiuchumi na kurahisisha usafiri na usafirishaji kwa kupunguza msongamano wa magari mijini.

Madaraja haya ni pamoja na: Kigongo – Busisi (JPM) lililopo Mwanza ambapo hadi Aprili 2024 utekelezaji wake umekamilika; na utekelezaji wa madaraja ya juu ya Uhasibu na Chang'ombe katika jiji la Dar es Salaam ambapo utekelezaji wake umekamilika. Kukamilika kwa miradi hii kutachochea ukuaji wa uchumi, kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa zinazoingia nchini na zinazokwenda nchi jirani. Miradi hii pia itakuza biashara na kuvutia uwekezaji.



ii. **Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa**

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa ili kuinua na kuimarisha usafirishaji wa bidhaa na usafiri ndani ya nchi pamoja na kuunganisha Tanzania na nchi jirani. Katika kipindi cha utekelezaji hadi kufikia Desemba, 2024, utandazaji wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa umefikia km 680.38, ikilinganishwa na lengo la km 1,219 mwaka 2025/26 ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro umefikia asilimia 99.72, Morogoro – Makutupora (asilimia 97.98), Makutupora – Tabora (asilimia 14.53), Tabora – Isaka (asilimia 6.65), Mwanza - Isaka (asilimia 63.16) na Tabora – Kigoma (asilimia 7.88). Aidha, kuanza kwa huduma za usafirishaji wa abiria kutoka Dar es Saalam hadi Dodoma kumepunguza muda wa safari kutoka saa tisa (9) hadi saa tatu (3) kwa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma na hivyo kuwezesha muda uliopunguzwa kutumika katika shughuli zingine za uzalishaji mali, ambapo hadi Machi 2025 abiria 2,054,828 wamesafirishwa na jumla ya watanzania 206,579 wamepata ajira katika utekelezaji wa mradi huu. Kati ya ajira hizo, Watanzania 753 wameajiriwa katika kutoa huduma kwenye vituo vya SGR, Watanzania 54,946 wamepata ajira za moja kwa moja na watanzania 150,880 ajira zisizo za moja kwa moja katika ujenzi wa reli ya SGR.

Kuanza kwa huduma hii kumechangia pia katika kuongeza tija katika uchumi na biashara kwa ujumla. Mradi huu umechangia Tanzania kuwa nchi ya 58 mwaka 2023/24 kutoka nafasi ya 83 mwaka 2019/20 kwa ubora wa reli duniani, jambo ambalo ni muhimu katika ushindani wa biashara wa kikanda na kimataifa. Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa ujenzi wa reli ya kusini (Mtwara port - Mbamba Bay km 1,000 na tawi la kuelekea Mchuchuma na Liganga) kwa kiwango cha kimataifa ambapo utekelezaji wake upo katika hatua za wali.

iii. **Ununuzi wa Meli na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi**

Serikali imeendelea na ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa- Masoko ambapo shughuli zilizofanyika ni pamoja na: ujenzi wa gati ambao umefikia asilimia 75; ujenzi wa jengo la utawala pamoja na jengo kupoza na kusambaza umeme eneo la bandari ambao umefikia asilimia 70; kuongeza kina cha maji ambao umekamilika kwa asilimia 100; ujenzi wa matenki ya kuhifadhia maji safi na maji kwa ajili ya majanga ambao umekamilika kwa asilimia 100; pamoja na ujenzi wa ukuta wa kuzuia mmomonyoko baharini ambao umefikia asilimia 78. Kwa ujumla hadi kufikia Desemba 2024, utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 75. Aidha, taratibu za ununuzi wa meli mbili (2) kupitia shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) unaendelea.

Mradi huu utakapokamilika utakuwa na manufaa yafuatayo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla: kuimarisha shughuli za uvuvi; kuvutia utalii wa ikolojia; kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya uvuvi, hususan katika Bahari Kuu; kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Uvuvi kwenye Pato la Taifa; kuongeza fursa za ajira; na kuongeza uwekezaji katika viwanda vya kuchakata samaki na katika mnyororo wa uongezaji thamani wa mazao ya uvuvi.

iv. **Kuboresha Shirika la Ndege la Taifa**

Katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali ilipanga kuimarisha na kuendeleza Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege mpya ili kufikisha idadi ya ndege 19 ifikapo 2025/26; kutoa mafunzo kwa marubani na wahandisi; na kuboresha miundombinu ya karakana. Uboreshaji wa huduma za Shirika la Ndege unatarajiwa kuchochea uwekezaji katika kutoa huduma za kusafirisha mizigo na abiria zenye kuhimili ushindani katika soko la kikanda na kimataifa na kuchagiza shughuli za sekta za utalii na kilimo na ndani ya nchi. Kufikia Desemba 2024/25 jumla ya ndege 16 zimenunuliwa sawa na asilimia 84.2 ya lengo ifikapo 2025/26. Huduma ya uhakika ya usafiri wa anga, pamoja na masuala mengine, imechangia ongezeko la watalii wa ndani na nje ya nchi, hivyo kuchangia ongezeko na mchango wa sekta ya utalii katika uchumi wa Tanzania. Vilevile usafirishaji wa mazao na bidhaa za kilimo umeongezeka kutokana na uwepo wa ndege kubwa ya mizigo, hivyo kuchochea ongezeko la mapato yatokanayo na sekta hiyo hususan sekta ndogo ya mbogamboga na matunda.

## 3.2.2 Miradi ya Miundombinu ya Nishati

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali ilipanga kutekeleza miradi Saba (7) ya kielelezo ya nishati inayojumuisha uzalishaji umeme wa maji, utafutaji mafuta, gesi asilia, na bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.




i. **Miradi ya Uzalishaji Umeme wa Maji**

Miradi ya kuzalisha umeme kwa njia ya maji inayotekelezwa ni: mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (MW 2,115) ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 99.9 ambapo mitambo yote tisa (9) imekamilika na umeme unaingizwa kwenye gridi ya Taifa kulingana na mahitaji. Vilevile, miradi miwili (2) ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222) ipo katika hatua za maandalizi. Kukamilika kwa miradi hiyo kutachangia upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa viwandani, ongezeko la ajira kutokana na kuongezeka



kwa shughuli za uzalishaji, kuchochea uwekezaji nchini, kupunguza matumizi ya mafuta kwa ajili ya uzalishaji wa umeme suala linalosababisha matumizi ya fedha nyingi za kigeni, na kukuza uchumi shindani na jumuishi.

ii. **Miradi ya usindikaji Gesi asilia na utafutaji mafuta**

Serikali ilipanga kutekeleza miradi ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Eyasi – Wembere na Mnazi Bay pamoja na mradi wa Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG). Miradi hiyo ipo katika hatua za maandalizi ambapo kwa upande wa utafutaji mafuta, taratibu zitakazowezesha uchimbaji wa visima vya utafutaji na uhakiki zinaendelea. Kuhusu mradi wa LNG, majadiliano baina ya Serikali na wawekezaji yanaendelea. Aidha, kwa upande wa mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania utekelezaji umefikia asilimia 54.9, ambapo ujenzi wa misingi kwa ajili ya kusimika mitambo umekwisha kamilika.

Kukamilika kwa miradi hii kutaongeza uzalishaji wa gesi asilia nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani ikiwemo viwandani pamoja na kuuza gesi hiyo katika nchi jirani za Kenya, Uganda, Zambia na Malawi. Hatua hiyo itachangia katika ukuaji wa uchumi, ongezeko la fedha za kigeni, fursa za ajira na huduma za ugavi, pamoja na biashara kwa Watanzania. Aidha, itachochea uchumi shindani na jumuishi, uwekezaji, kuongezeka kwa uzalishaji viwandani, kuchangia maendeleo ya watu na ujuzi.



iii. **Mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi**

Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi lenye urefu wa km 1,443 kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania ambao umefikia asilimia 54.9 ambapo ukamilishaji wa mradi huu utawezesha mafuta hayo kusafirishwa kwenda katika masoko ya kimataifa. Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza ajira za kudumu na zisizo za kudumu, kukuza mapato ya Serikali na kuhamasisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini. Hivyo, mradi huu utapanua shughuli za uwekezaji na biashara, kuchangia maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi na kuchochea ukuaji wa uchumi shindani na endelevu.

iv. **Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma Liganga**

Miradi hii ni miongoni mwa miradi ya kielelezo iliyopo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Lengo la mradi ni kuzalisha chuma tani milioni 2.9 na makaa ya mawe tani milioni 3 kwa mwaka. Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa kuzalisha MW 600 kwa kutumia makaa ya mawe ambapo kiasi cha MW300 zitatumika kuzalisha chuma cha pua na madini mengine kwenye viwanda vya Mchuchuma na Liganga. Umeme utakaobaki, kiasi cha MW 300, zitaingizwa katika Gridi ya Taifa ili kuongeza uhakika wa umeme utakaotumika katika viwanda na kuchangia ajenda ya mageuzi ya viwanda. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwenye miradi hii ni pamoja na ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha mradi; ulipaji wa leseni za uchimbaji; na kuanza majadiliano na mwekezaji. Shughuli zilizotekelezwa ni ulipaji wa fidia kwa asilimia 99.9 na kuanza maandalizi ya majadiliano na mwekezaji. Matokeo ya miradi huu ukikamilika ni pamoja na kupatiakana kwa malighafi ya chuma na makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya viwanda mbalimbali nchini; kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kununua chuma nje ya nchi; kuongeza maendeleo ya watu kupitia ajira zitazotolewa; na kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni kwa kuongeza mauzo ya chuma, makaa ya mawe na saruji nje ya nchi.

Utekelezaji wa miradi hii yenye uhusiano wa moja kwa moja na sekta ya madini, nishati na kilimo upo katika hatua za awali. Miradi hii itakapokamilika itachochea uchumi shindani na jumuishi, uwekezaji na biashara, kuongezeka kwa uzalishaji bidhaa viwandani na kuchangia maendeleo ya maarifa ya rasilimali watu na fursa za ajira.

### 3.2.3 Miradi ya Kuongeza Uzalishaji Viwandani

Serikali kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano iliainisha miradi mitatu ya kielelezo yenye kujielekeza moja kwa moja kwenye kuongeza uzalishaji viwandani. Miradi hiyo ni Mradi wa Magadi Soda (Engaruka), Kiwanda cha Sukari Mkulazi na Kanda Maalum za Uchumi na Uwekezaji.

i. **Mradi wa Magadi Soda ya Engaruka**

Mradi wa Engaruka ni miongoni mwa miradi ya kielelezo iliyopo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kufanya majadiliano na mwekezaji ili kuingia mkataba wa ubia; na kulipia leseni za uchimbaji. Aidha, shughuli zilizotekelezwa ni kukamilika kwa hatua za awali ni pamoja na kugawanya eneo la mradi katika maeneo matatu ambapo mawili yametangazwa Desemba, 2024 kwa ajili ya kupata wawekezaji na eneo moja

limebaki chini ya NDC. Hadi kufikia Februari, 2025 ulipaji wa fidia kwa wananchi 528 sawa na asilimia 88.7 ya wafidiwa wote 595 umefanyika. Aidha, ukamilishaji wa zoezi la ulipaji fidia unaendelea kwa wafidiwa 67 waliobaki. Matokeo ya Mradi huu ni pamoja na: kuongeza ajira; kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza magadi soda kutoka nchi za nje; na kuongeza mauzo nje ya nchi. Mradi utasaidia upatikanaji wa malighafi za magadi soda kwenye viwanda mbalimbali vinavyotumia malighafi hizo.

ii. **Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuongeza upatikanaji wa sukari nchini kwa kujenga kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha tani 250,000 za sukari kwa mwaka na kuzalisha fursa za ajira 100,000. Kiwanda cha sukari Mkulazi kimelenga kuongeza upatikanaji wa sukari nchini kwa kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka na kuzalisha fursa za ajira 11,315. Ukubwa wa shamba la mradi huu ni hekta 4,856 (ekari 12,000).

Hadi kufikia mwezi Desemba 2024, kiwanda kimezalisha jumla ya tani 19,124 za sukari ya matumizi ya nyumbani (brown sugar) na kutoa ajira 10,172 ambapo ajira rasmi ni 2,172 na zisizo rasmi ni 8,000. Vilevile, ufungaji wa mitambo ya kuzalisha sukari ya viwandani (industrial sugar) umefikia asilimia 98 ukitarajiwa kukamilika mwezi Aprili 2025 na uzalishaji wa majaribio kufanyika mwezi Juni 2025 wakati wa msimu wa uvunaji.

iii. **Kanda Maalum za Uchumi na Uwekezaji**

Eneo hili linahusisha kuendeleza kanda maalum za kiuchumi Bagamoyo na eneo la Benjamin Mkapa pamoja na maeneo mawili maalum ya uwekezaji ambayo ni bandari huru ya Mtwara na eneo la uwekezaji Manyara.

Katika eneo la miradi ya kanda maalum za uchumi na uwekezaji, Serikali kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ililenga kuendelea kuimarisha miundombinu katika kanda hizo na kuanzisha maeneo mengine mapya katika mikoa ya Singida (Manyoni), Pwani, Kigoma, Tanga, Manyara, Mara, na Ruvuma. Serikali imetenga maeneo 17 kwa ajili ya kuanzisha kanda maalum za uwekezaji ambapo maeneo mawili ya Benjamin William Mkapa SEZ na Mtwara yameanza uzalishaji, na maeneo 15 yapo katika hatua mbalimbali za uendelezaji. Utekelezaji wa miradi katika kanda hizi maalum utaongeza idadi na thamani ya uwekezaji na kongani za uwekezaji, ajira, uzalishaji, fedha za kigeni na huduma. Kukamilika kwa miradi hii kutaongeza ushindani katika soko la ndani na nje, uzalishaji viwandani na kuvutia uwekezaji nchini.

## 3.3 Programu na Miradi ya Kimkakati ya Kisekta

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi ya maendeleo kwa kuzingatia maeneo matano (5) ya vipaumbele ambapo katika mwaka 2024/25 Serikali iliendelea kutekeleza programu na miradi 1,604 ambayo ipo katika hatua mbalimbali. Utekelezaji wa miradi hii umesaidia kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.4 mwaka 2024 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 5.1 mwaka 2023; mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati; kuongezeka kwa mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma

kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4). Jedwali Na. 3.1 linaonesha muhtasari wa idadi ya progaramu na miradi ya maendeleo inayotekelezawa katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

**Jedwali Na 3.1 Muhtasari wa Idadi ya Programu na Miradi Inayotekelezwa kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Sekta | Idadi ya Programu/Miradi |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi | 163 |
| 2 | Uchukuzi | 71 |
| 3 | Nishati | 27 |
| 4 | Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | 7 |
| 5 | Kilimo | 88 |
| 6 | Mifugo na Uvuvi | 96 |
| 8 | Uzalishaji Viwandani | 43 |
| 9 | Madini | 13 |
| 10 | Utalii | 73 |
| 11 | Sanaa, Utamaduni na Michezo | 16 |
| 12 | Kukuza Uwekezaji na Biashara | 9 |
| 13 | Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi | 10 |
| 14 | Elimu | 153 |
| 15 | Afya | 198 |
| 16 | Maji na Usafi wa Mazingira | 482 |
| 17 | Hifadhi ya Jamii | 8 |
| 18 | Utawala Bora na Utawala wa Sheria | 10 |
| 19 | Mazingira na Maliasili | 17 |
| 20 | Ustawi na Maendeleo ya Jamii | 17 |
| 21 | Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 25 |
| 22 | Amani, Utulivu na Usalama | 74 |
| 23 | Kukuza Ujuzi | 4 |
| **Jumla** | | **1,604** |



*Ujenzi wa Airport Msalato, Dodoma.*

Utekelezaji wa programu na miradi ya kimkakati ya kisekta na mchango wake katika kufikia matokeo tarajiwa ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni kama ifuatavyo:

### *3.3.1 Sekta ya Ujenzi*

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi 163 ya ujenzi ambayo ipo katika hatua mbalimbali. Kati ya miradi iliyotekelezwa, miradi 109 ni ya ujenzi wa barabara inayosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Miradi mingine iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa madaraja 21, vivuko 28 , ujenzi wa viwanja vya ndege 7 na miradi 5 ya ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali.

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, Serikali kupitia programu za miradi imeweza kuongeza mtandao wa barabara zinazopitika wakati wote za kitaifa na mikoa, kuongeza mtandao wa barabara za vijijini na mijini kwa kiwango cha lami kufikia km 15,366.36 mwaka 2024 kutoka km 13,235.1 mwaka 2020. Utekelezaji wa miradi hii umetengeneza nafasi za ajira 30,129 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na ajira 26,367 mwaka 2023/24 pamoja na kuongezeka kwa kiwango cha mchango wa sekta katika Pato la Taifa kwa asilimia 2.6. Vilevile, kurahisishwa kwa shughuli za uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa kutoka maeneo ya uzalishaji; kurahisisha utoaji wa huduma; kuchochea utulivu wa bei ya soko; na kuchangia ushindani wa kibiashara ndani na nje ya nchi..

Aidha, sekta binafsi imekuwa ikishiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kwa mwaka 2024/25 jumla ya makampuni 1,322 yalipewa kandarasi za kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi. Vilevile, jumla ya miradi 1,030 ya ujenzi wa nyumba za makazi na biashara umeendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali na hivyo, kuchangia ongezeko la kipato na ajira, kuchochea uchumi na kujenga uwezo wa sekta binafsi ya ndani. Aidha, maboresho katika taasisi za usimamizi katika sekta ya ujenzi yamechangia kukuza ujuzi wa makandarasi na uwezo wa kutumia teknolojia za kisasa. Jedwali 3.2 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya ujenzi kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali 3.2: Viashiria na Shabaha za Utekelezaji katika Sekta ya Ujenzi** [2]

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Miundombinu (Nafasi katika mpangilio, kati ya nchi 189 kimataifa) | | | | | 2,373 | 4,018 | 4,915 |
| 2. | Kiwango cha wastani wa ukuaji (%) | 9.0 | 14.1 | 14.0 | 14.1 | | 9.9 | 9.9 |
| 3. | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 13.9 | 14.0 | 13.8 | 14 | 14.1 | 16.7 | 16.7 |
| 4. | Mchango wa kampuni za ndani katika soko la ujenzi (%) | 35 | 35 | 35 | 35 | 35 | 40 | 60 |
| 5. | Idadi ya ajira zilizozalishwa katika miradi ya maendeleo | 23,585 | 11,862 | 24,007 | 47,617 | 26,367 | 30,129 | 30,155 |
| 6. | Urefu wa mtandao wa barabara za kiwango cha changarawe (KM) | 25,779 | 25,152 | 25,034 | 24,793 | 25,197 | | |
| 7. | Nafasi ya barabara katika mpangilio wa kimataifa | 86 | | | 42 | 39 | 27 | 26 |

***Chanzo:** : Wizara ya Ujenzi*

### 3.3.2 Sekta ya Uchukuzi

Katika mwaka 2024/25, Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi 71 ya uchukuzi ambayo ipo katika hatua mbalimbali. Miradi iliyotekelezwa inahusisha uboreshaji wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa njia ya reli, anga na maji.

Utekelezaji wa miradi hii umechangia kuongezeka kwa mapato ya Serikali yatokanayo na bandari ambapo kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika bandari ya Dar es Salaam kulikofanywa na mwekezaji aliyekabidhiwa kuendesha sehemu ya bandari hiyo, muda wa meli kukaa bandarini umepungua kutoka siku 4.1 mwaka 2023/24 hadi siku 3.7 mwaka 2024/25; na idadi ya meli zinazoingia bandarini kwa mwezi imeongezeka kutoka 374 mwaka 2023/24 hadi kufikia meli 411 mwaka 2024/25; Kupungua kwa muda wa kuhudumia meli za makasha gatini kutoka wastani wa siku 10 mwaka 2023/24 hadi siku tatu (3) mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya wanaanga waliopata mafunzo kutoka 567 mwaka 2023/24 kufikia 1,088 mwaka 2024/25; na kuongezeka kwa mitambo ya ulinzi na ukaguzi katika viwanja vya ndege kutoka mitambo 85 mwaka 2023/24 kufikia mitambo 101 mwaka 2024/25.

2 Maeneo ambayo hayana takwimu kwenye jedwali yametokana na kutozalishwa kwa taarifa katika kipindi husika

Aidha, sekta binafsi imeendelea kuwa na mchango katika kufikia shabaha za sekta ya uchukuzi kwa kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kwa mwaka 2024/25 jumla ya kampuni 648 zilipewa kandarasi za kutekeleza miradi mbalimbali ya uchukuzi. Kati ya kampuni hizo za Watanzania ni kampuni 595 na kampuni 53 ni za kigeni. Ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya uchukuzi kumechangia ongezeko la ajira, kipato, uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje ya nchi; kuchochea uchumi na kujenga uwezo wa sekta binafsi ya ndani kiteknolojia kutoka nje ya nchi. Jedwali 3.3 linaonesha mwenendo wa viashiria na shabaha kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano.

**Jedwali 3.3 Viashiria na Shabaha za Utekelezaji katika Sekta ya Uchukuzi**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Nafasi ya reli katika mpangilio wa kidunia | 83 | 83 | 83 | 78 | 58 | 58 | 70 |
| 2. | Urefu wa reli ya kati kwa kiwango cha Standard Gauge (SGR) kwa kilometa | 395.2 | 451.43 | 487.9 | 553.03 | 625.84 | 680.38 | 1,219 |
| 3. | Kiasi cha shehena kinachosafirishwa na reli (tani) | 1,569,536 | 2,374,969 | 3,217,620 | 3,941,229 | 4,541,731 | 4,788,764 | 5,162,258 |
| 4. | Idadi ya abiria wanaosafirishwa na reli | 972,000 | 1,250,373 | 1,143,787 | 1,394,058 | 1,213,225 | 2,054,828 | 2,272,682 |
| 5. | Muda wa meli kurejea kituoni kwake (siku) | 9.5 | 8.8 | 9.7 | 8.7 | Wastani 13.1 | Wastani 11.2 | 8 |
| 6. | Idadi ya meli zinazoingia bandarini kwa mwezi | 281 | 353 | 391 | 473 | 374 | 411 | 254 |
| 7. | Muda wa makasha kukaa bandarini (siku) | 7 | 7 | 9.0 | 9.2 | 6.7 | 7.5 | 5 |
| 8. | Muda wa meli kukaa bandarini (siku) | 3.7 | 3.7 | 4.6 | 4.4 | 4.1 | 3.7 | 2 |
| 9. | Idadi ya bandari kavu | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 3 |
| 10. | Idadi ya meli zinazohudumiwa | 3,704 | 4,241 | 4,686 | 5,675 | 4,487 | 2,471 | 4,000 |
| 11. | Mizigo inayotoka nje kuelekea nchi za jirani (tani milioni) | 15.1 | 17.2 | 19.9 | 22.6 | 30.1 | 34.7 | 18.0 |
| 12. | Mizigo ya kwenda nje toka kwa nchi jirani (tani milioni) | 6.3 | 9.8 | 14.9 | 20.6 | 26.8 | 27.9 | 10.0 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 14. | Idadi ya ndege za mizigo zilizonunuliwa | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| 15. | Idadi ya ndege za abiria za masafa marefu zilizonunuliwa | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 3 | 3 |
| 16. | Idadi ya ndege za abiria za masafa ya kati (kanda) zilizonunuliwa | 2 | 2 | 4 | 4 | 6 | 6 | 8 |
| 17. | Idadi ya ndege za ATCL zinazofanya kazi | 10 | 10 | 12 | 13 | 14 | 15 | 19 |
| 18. | Idadi ya wanaanga waliofunzwa | 61 | 99 | 279 | 320 | 567 | 1,088 | 1,359 |
| 19. | Idadi ya viwanja vya ndege vyenye mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege (AMIS) | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 10 | 14 |
| 20. | Idadi ya mitambo ya ulinzi kwenye viwanja vya ndege (X-ray machines) | 46 | 80 | 83 | 83 | 85 | 101 | 71 |
| 21. | Viwanja vya ndege vyenye uzio kuzunguka kiwanja | 9 | 9 | 11 | 16 | 16 | 18 | 27 |
| 22. | Idadi ya rada za hali ya hewa zilizonunuliwa | 5 | 7 | 7 | 7 | 7 | 7 | 7 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Uchukuzi*

### 3.3.3 Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi 28 ya sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari yenye lengo la kuimarisha miundombinu ya mawasiliano mijini na vijijini, pamoja na kuunganisha mawasiliano na nchi jirani (Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia na Msumbiji) kupitia ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Aidha, Serikali imeweka anuani za makazi kwa ajili ya utambuzi wa maeneo, kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na posta nchini, kurahisisha upatikanaji wa huduma katika mifumo ya Serikali na sekta binafsi. Vilevile, katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea kuwekeza katika sekta ya mawasiliano ambapo watumiaji wa huduma za mawasiliano wameongezeka, mathalan uwiano wa watumiaji wa huduma za inteneti nchini umefikia asilimia 75 kwa mwaka 2024/25 kutoka asilimia 61.2 mwaka 2023/24, na kuongezeka kwa idadi ya watoa huduma waliosajiliwa kwenye mfumo wa anwani za makazi kutoka 831,436 mwaka 2023/24 kufikia 1,000,000 mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuendelea kuwezesha sekta nyingine za uzalishaji katika utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi kwa kuendelea kutumia mifumo ya TEHAMA; kuongezeka kwa miamala ya fedha mtandao na huduma nyingine za kimtandao; kupungua kwa bei za huduma za mawasiliano; kuongezeka kwa ajira pamoja na kuchochea ukuaji wa uchumi. Jedwali 3.4 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali 3.3 Viashiria na Shabaha za Utekelezaji katika Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Uwiano wa watumiaji wa intaneti nchini (%) | 47 | 49 | 48 | 54 | 60 | 74 | 80 |
| 2. | Idadi ya majengo yenye anwani za makazi (milioni) | - | - | - | 18,000,000 | 18,000,000 | 18,186,0000 | 18,250,000 |
| 3. | Idadi ya anwani zilizosajiliwa kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi | - | - | - | 12,385,956 | 12, 891,392 | 13,200,000 | 15,231,392 |
| 4. | Idadi ya huduma zilizosajiliwa kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi | - | - | - | 800,000 | 831,436 | 1,000,000 | 1,100,000 |
| 5. | Idadi ya watu wanaomiliki simu za mkononi (milioni) | 26,7 | 29,5 | 31.2 | 33.7 | 39.8 | 45.2 | 28.6 |
| 6. | Idadi ya barua za utambulisho zilizotolewa kupitia Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi | - | - | - | 800 | 848 | 15,000 | 15,500 |
| 7. | Kaya zenye angalau mwanakaya mmoja anayemiliki simu ya mkononi (%) | 82.6 | - | 85 | | 87.6 | 87.6 (2023/24) | 87.8 |
| 8. | Uwiano wa watu waliofikiwa na mitandao ya simu za mkononi (%) | 94 | | | | 98 | | 100 |
| 9. | Taasisi za Serikali zinazopata huduma ya intaneti yenye kasi (%) | 20 | - | - | - | 50 | - | 70 |

| Na. | Kiashiria | | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 10. | Uwiano wa watu waliofikiwa na mtandao wa simu za mkononi (%) | 2G | - | - | - | - | - | 98.2 | 100 |
| | | 3G | 68 | 70 | 71 | 77 | 89 | 91 | |
| | | 4G | 49 | 50 | 52 | 65 | 83 | 88 | |
| | | 5G | - | - | - | - | 15 | 20 | |

***Chanzo:*** *Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari*

### 3.3.4 Sekta ya Nishati

Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya nishati nchini kwa lengo la kuchochea kasi ya ukuaji na uzalishaji katika viwanda pamoja na matumizi mengine nchini. Katika kufikia lengo hilo, Serikali imetekeleza programu na miradi 27 ya Sekta ya Nishati ambayo ipo katika hatua mbalimbali. Mafanikio ya utekelezaji wa miradi hiyo ni pamoja na: uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa umeongezeka na kufikia MW 4,031.71 mwezi Aprili 2025, sawa na ongezeko la asilimia 86.6 ikilinganishwa MW 2,138 zilizounganishwa kufikia mwezi Machi 2024; kufikisha umeme katika vijiji vyote 12,318; kuongezeka kwa urefu wa Gridi ya Taifa kutoka km 7745.4 mwaka 2023/24 hadi kufikia km 8625.4 mwaka 2024/25; na kupungua kwa upotevu wa umeme kutoka asilimia 14.56 mwaka 2023/24 hadi asilimia 12.3 mwaka 2024/25.

Sekta binafsi imekuwa na mchango pia katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za sekta ya nishati katika maeneo ya mijini na vijijini. Jumla ya kampuni 2,860 zilipata kandarasi zilizowezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali ambapo takriban wananchi 68,905 walinufaika na ajira kupitia kampuni hizo. Aidha, sekta binafsi imeshiriki katika uzalishaji wa umeme kupitia vyanzo vya maji, jua na tungamotaka vyenye uwezo wa kuzalisha MW 338.1 ambapo MW 307.98 zinatumika kwa matumizi binafsi na MW 30.12 zinaingizwa katika Gridi ya Taifa. Jedwali Na. 3.5 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya nishati kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Aprili, 2025**
**4,032 mw ▲**
**2,138 mw ▼**
Machi, 2024
*Mfumo wa gridi ya Taifa umeongezeka*

**2024/25**
**12.30% ▼**
**14.56% ▲**
2023/24
*Upotevu wa umeme umepungua*

**68,905**
*Idadi ya wananchi walionufaika na ajira*

**Jedwali 3.5: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji vya Sekta ya Nishati**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Uzalishaji wa Umeme (MW) | 1,601.84 | 1,605.86 | 1,694.55 | 1,872.05 | 2,138 | 4,031.71 | 4,915 |
| 2. | Idadi ya Mikoa Iliyounganishwa na Gridi | 23 | 23 | 23 | 24 | 24 | 24 | 26 |
| 3. | Urefu wa Gridi ya Taifa (km) | 5,851.17 | 6,111.27 | 6,111.27 | 6,363.27 | 7,745 | 8,140 | 9,351 |
| 4. | Kupungua kwa Upotevu wa Umeme (%) | 16.19 | 15.16 | 14.71 | 14.62 | 14.56 | 12.3 | 7.9 |
| 5. | Asilimia ya [4]watu waliofikiwa na Umeme | 78.4 | - | - | - | - | 78.4 | 85 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Nishati*

### 3.3.5 Sekta ya Kilimo

Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali katika sekta ya kilimo yenye lengo la kuhakikisha usalama wa chakula, kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni, kuongeza ajira na kipato pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za viwandani. Ili kufikia malengo haya, Serikali ilitekeleza shughuli zifuatazo: Kuwezesha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; kuimarisha mifumo ya masoko hususan minada, stakabadhi ghalani na TMX; uanzishwaji wa Benki ya Ushirika kwa kuwezesha upatikanaji wa mtaji wa shilingi bilioni 20; kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi wa chakula; kuimarisha huduma za ugani; kuwezesha upatikanaji wa masoko ya mazao nje ya nchi; kuongeza upatikanaji wa wa mbolea kufikia tani 1,213,729 mwaka 2024/25 kutoka tani 678,017 mwaka 2020/21; kuwezesha uanzishwaji wa kilimo cha mashamba makubwa; kuimarisha utafiti; na kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kufikia tani 79,700.62 mwaka 2024/25 sawa na asilimia 99.6 ya lengo la kuzalisha na kuthibitisha tani 80,000 za mbegu dhidi ya mahitaji ya tani 127,650 .

Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii ni pamoja na: kuzalisha ajira kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 61.4 na kuchangia asilimia 65 ya malighafi za viwanda kwa mwaka 2024; kuongezeka kwa eneo la kilimo cha umwagiliaji kufikia hekta 727,280.6 ikiwa na lengo la kufikia hekta 1,200,000 ifikapo mwaka 2025/26; kuboresha miundombinu ya makazi na utoaji wa vitendea kazi kwa maafisa ugani nchini; kuongezeka kwa akiba ya Taifa ya chakula na utoshelevu wa chakula kufikia asilimia 128 mwaka 2024/25 kutoka asilimia 124 mwaka 2023/24; kuongezeka kwa wanachama na vyama vya ushirika kutoka wanachama milioni 6.9 mwaka 2023/24 kufikia milioni 8.4 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa kiasi cha mazao ya bustani yaliyozalishwa kufikia tani 7,518,560.84 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 83.5 lengo la kuzalisha tani milioni 9,000,000; na kuongezeka kwa mauzo ya mazao nje ya nchi.

4 Kiashiria hiki kinategemea utafiti wa hali ya upatikanaji wa nishati ya umeme Tanzania Bara

Sekta binafsi imeendelea kuwa na mchango katika kufikia shabaha za sekta ya kilimo kwa kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kwa mwaka 2024/25 jumla ya kampuni 42 zinashiriki katika shughuli mbalimbali zinazohusiana na mnyororo wa uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo. Jedwali 3.6 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya kilimo kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali 3.6: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Kilimo**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Hekta za kilimo cha umwagiliaji | 694,715 | 695,005 | 695,005 | 727,280.6 | 727,280.6 | 727,280.6 | 1,200,000 |
| 2. | Mbegu zilizoidhinishwa na zilizozalishwa (tani) | 76,285.56 | 44,581.08 | 50,747 | 58,807.61 | 71,356 | 79,700.62 | 80,000 |
| 3. | Akiba ya taifa ya chakula (tani) | 52,724.730 | 107,384.057 | 141,575.902 | 46,893.983 | 785,003.02 | 1,110,000 | 1,140,000 |
| 4. | Kiasi cha mazao ya bustani yaliyozalishwa (tani) | 6,597,863 (2019) | 7,304,723 (2020) | 7,304,723 (2021) | 7,723,116 (2022) | 7,518,560.84 (2023) | 7,518,560.84 | 9,000,000 |
| 5. | Kiasi cha uzalishaji wa mazao ya biashara ya asili (traditional) (tani). | 1,144,631 (2019) | 898,967 (2020) | 898,967 (2021) | 973,436 (2022) | 1,201,832.65 (2023) | 1,451,694.11 | 1,583,200 |
| 6. | Idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika | 113 | 183 | 267 | 267 | 267 | 331 | 338 |
| 7. | Idadi ya vyama vya ushirika vinavotumia mfumo wa soko rasmi | 1202 | 1302 | 1402 | 1573 | 2,231 | 4,046 | 2,782 |
| 8. | Idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika (milioni) | 4.2 | 4.5 | 5.1 | 6.2 | 6.9 | 8.4 | 14.5 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo*

### 3.3.6 Sekta ya Mifugo

Katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali kupitia sekta hii inatekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Shughuli zilizotekelezwa kupitia programu hii ni pamoja na: ujenzi wa miundombinu muhimu ya malisho, majosho na masoko; kutoa huduma za ugani; udhibiti wa magonjwa na uzalishaji wa mbegu bora; kufanya utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo; na uongezaji thamani na biashara ya mifugo na mazao yake.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa shughuli hizo ni pamoja na: kuongezeka kwa uzalishaji nyama kutoka tani 963,856.55 mwaka 2023/24 hadi kufikia tani 1,054,114.03 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa vipande vya ngozi vilivyozalishwa na kufikia jumla ya vipande vya ngozi 15,191,500 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na vipande milioni 14.69 mwaka 2023/24; kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa kutoka lita bilioni 3.97 mwaka 2023/24 kufikia lita bilioni 4.0 mwaka 2024/25; na kuongezeka kwa biashara ya ngozi na kufikia jumla ya vipande 1,651,088 mwaka 2024/25 kutoka vipande vya ngozi 1,542,916 mwaka 2023/24.

Aidha, Sekta binafsi imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza sekta kwa kushiriki katika uwekezaji katika shughuli mbalimbali ikiwemo ufugaji, uzalishaji wa malisho na vyakula vya mifugo, uzalishaji wa dawa na chanjo za mifugo. Hadi kufikia Aprili, 2025, jumla ya dozi 95,129,900 zimezalishwa na Sekta Binafsi. Ushiriki wa sekta binafsi katikashughuli za mifugo umechangia ongezeko la ajira, kipato, kuchochea ukuaji wa uchumi na kujenga uwezo wa sekta binafsi ya ndani. Jedwali 3.7. linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya mifugo kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali 3.7: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Mifugo**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Kiwango cha wastani wa ukuaji (%) | 4.9 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.5 | 6.5 |
| 2. | Mchango katika Pato la Taifa (bei za sasa) (%) | 7.4 | 7.1 | 7.2 | 6.7 | 6.2 | 6.2 | 7.0 |
| 3. | Kiwango cha vifo vya mifugo (%) | 27 | 24 | 21 | 18 | 16 | 16 | 12 |
| 4. | Kiwango cha magonjwa ya mifugo (%) | 6 | 5 | 4.5 | 3.5 | 2.5 | 2.5 | 3 |
| 5. | Kiwango cha uogeshaji mifugo katika josho (%) | 70 | 72 | 74 | 75 | 78 | 82 | 85 |
| 6. | Kiwango cha chanjo ya mifugo (%) | 25 | 37 | 39.5 | 40 | 42 | 42 | 50 |
| 7. | Wastani wa uzalishaji maziwa, ng'ombe wa asili (Lita) | 2 | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.8 | 0.85 | 4 |
| 8. | Ngozi bora iliyochakatwa (%) | 10 | 15 | 20 | 25 | 30 | 40 | 50 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 9. | Uzalishaji wa nyama (Tani) | 702,000 | 738,165.99 | 769,966.65 | 803,264.3 | 963,856.55 | 1,054,114.03 | 951,700 |
| 10. | Uzalishaji wa maziwa (Lita bilioni) | 3.01 | 3.1 | 3.4 | 3.6 | 3.97 | 4.1 | 4.3 |
| 11. | Asilimia ya maziwa yaliyochakatwa | 5 | 2 | 2 | 2 | 2.2 | 2.2 | 14 |
| 12. | Ngozi i zilizochakatwa (Tani) | 1,190 | 143 | 146 | 2,250 | 2,385 | 2,900 | 9,210.6 |
| 13. | Mauzo ya nyama nje ya nchi (Tani) | 692 | 1,774.00 | 10,415.00 | 12,243.79 | 14,701.10 | 14,900 | 7,200 |
| 14. | Usafirishaji wa ngozi (Tani) | 6,747 | 7,951 | 7,371 | 4,491 | 5,778 | 7,200 | 8,000 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mifugo na Uvuvi*

### 3.3.7 Sekta ya Uvuvi

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kuwekeza katika miundombinu ya uvuvi, vifaa, na ufugaji wa samaki wa kibiashara pamoja na kuhamasisha uwekezaji kupitia sekta binafsi na ufungamanishaji wa utafiti na uzalishaji wa kilimo cha kwenye maji. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: ujenzi wa miundombinu muhimu ya uvuvi ya masoko ya samaki, mialo, vituo vya ukuzaji viumbe maji, mashamba darasa ya ukuzaji viumbe maji, na vituo vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi; kuendeleza huduma za ugani; ujenzi wa bandari ya uvuvi; na ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ya uvuvi kupitia uwezeshaji wa sekta binafsi.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa shughuli hizo ni pamoja na: kuongezeka kwa ukuaji wa sekta ya uvuvi kutoka asilimia 1.4 mwaka 2023 hadi asilimia 2.3 mwaka 2024; kuongezeka kwa uzalishaji na upatikanaji wa samaki katika maji ya asili na kufikia kiasi cha tani 466,956.88 mwezi Aprili 2025 kutoka tani 429,168.39 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024; kuongezeka kwa kiasi cha samaki zilizovunwa na kufikia tani 510,547.33 mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na tani 463,996.89 za samaki zilizovunwa mwaka 2023/2024; kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula cha samaki nchini kutoka tani 3,455.4 mwaka 2023/24 hadi kufikia tani 5,879 mwaka 2024/25.

Aidha, Sekta binafsi ina mchango mkubwa katika maendeleo ya uvuvi na ufugaji samaki nchini kwa kuibua ubunifu, na kuwekeza katika maboresho ya minyororo ya thamani. Mchango wa sekta binafsi katika sekta ya uvuvi ni pamoja na kuwezesha kukua kwa kilimo cha mwani kama shughuli ya kibiashara kwa upande wa pwani; kuongezeka

kwa kwa ufugaji wa samaki kwenye vizimba katika Ziwa Victoria ambapo uwekezaji wake mpaka 2025 umefikia zaidi ya vizimba 1,636 vinavyomilikiwa na sekta binafsi; kuanzisha viwanda vya usindikaji samaki vinavyozalisha bidhaa mbalimbali kwa masoko ya ndani na nje; na kusaidia ubunifu kama vile majokofu na usafiri, ambao hupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa (post harvest loss) na kuboresha ubora wa bidhaa.

**Jedwali Na. 3.8: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Uvuvi**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%) | 6.3 | 6.7 | 2.6 | 1.9 | 1.4 | 2.3 | 8.4 |
| 2. | Asilimia katika Pato la Taifa (bei za sasa) | 1.8 | 1.7 | 1.8 | 1.8 | 1.7 | 1.9 | 1.9 |
| 3. | Asilimia katika Mapato yatokanayo na mauzo Nje | 3.0 | 3.4 | 3.2 | 3.3 | 3.4 | 3 | 4.5 |
| 4. | Ulaji kwa kila mtu | 8.5 | 7.8 | 8.22 | 7.80 | 7.9 | 8.5 | 10.5 |
| 5. | Mchango katika ulaji wa protini ya wanyama Kitaifa | 30 | 30 | 30 | 30 | 30 | 33 | 35 |
| 6. | Uzalishaji wa samaki (tani) | 497,567.28 | 493,850.24 | 502,305.34 | 513,218.90 | 530,379.66 | 575,000 | 600,000 |
| 7. | Idadi ya viwanda vya kusindika samaki | 12 | 15 | 17 | 20 | 21 | 21 | 17 |
| 8. | Idadi ya vituo vya ukuzaji viumbe maji (Aquaculture Development Centres - ADC) | 9 | 9 | 9 | 9 | 9 | 12 | 12 |
| 9. | Uzalishaji wa chakula cha samaki (tani) | 276.7 | 472.47 | 1,615.5 | 3,012.7 | 3,455.4 | 5,879 | 8,000 |
| 10. | Idadi ya Maafisa Ugani wa Uvuvi | 657 | 657 | 657 | 657 | 657 | 700 | 1,850 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mifugo na Uvuvi*

### 3.3.8 Sekta ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali iliendelea kuimarisha sekta ya uzalishaji wa bidhaa viwandani kwa kuwekeza katika miradi na programu zinazolenga kuongeza mchango wa sekta katika Pato la Taifa. Katika utekelezaji huo, jumla ya miradi 27 inaendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na: uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata na kuongeza thamani mazao ya kilimo, madini, na mifugo; uboreshaji wa miundombinu ya viwanda vya teknolojia ya kati na ya juu; na uwekezaji katika utafiti na teknolojia za kisasa za uzalishaji kupitia taasisi mbalimbali. Mafanikio yaliyopatikana

katika sekta ya viwanda ni pamoja na: kuimarisha mchango wa sekta katika Pato la Taifa kutoka asilimia 7 mwaka 2023/24 hadi kufikia asilimia 8.5 mwaka 2024/25; mchango katika ajira zote umefikia asilimia 12.8 mwaka 2024 kutoka asilimia 8.1 mwaka 2023; na mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya juu katika mauzo nje umefikia asilimia 36 mwaka 2024/25 kutoka asilimia 25 mwaka 2023/24; na kuongezeka kwa mchango katika mauzo yote nje kutoka asilimia 21.6 mwaka 2023/24 kufikia asilimia 39 mwaka 2024/25.

Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya viwanda. Sekta inategemea sekta binafsi ambayo ndiyo inayowekeza mitaji kwenye viwanda ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa na huduma nchini unakuwepo wakati wote. Jedwali Na. 3.9 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya uzalishaji wa bidhaa viwandani kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

**Jedwali Na. 3.9: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 8.2 | 8.4 | 7.8 | 7.1 | 7.0 | 8.5 | 8.5 |
| 2. | Kiwango cha ukuaji halisi wa Pato la Taifa (%) | 5.2 | 4.7 | 4.5 | 4.2 | 4.3 | 6.8 | 6.8 |
| 3. | Mchango katika ajira zote (%) | 7.4 (2019) | 8.5 (2020) | 8.0 (2021) | 8.0 (2022) | 8.1 (2023) | 12.8 (2024) | 12.8 (2025) |
| 4. | Mchango katika mapato ya mauzo nje (%) | 17.1 | 17.7 | 22.9 | 26.9 | 17.7 | 19 | 19 |
| 5. | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya kati katika mauzo nje (%) | 28 | 29.2 | 21.1 | 0 | 25 | 36 | 39 |
| 6. | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya juu katika mauzo nje (%) | 8 | 8.8 | 8.9 | 0 | 25 | 42 | 10 |
| 7. | Mchango katika mauzo yote nje (%) | 16.9 (2019) | 17.7 | 22.9 | 26.9 | 21.6 | 39 | 24 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Viwanda na Biashara*

### 3.3.9 Sekta ya Madini

Katika kukuza sekta ya madini, Serikali imeendelea kutekeleza miradi miwili (2) inayolenga kuimarisha usimamizi endelevu wa rasilimali za madini; uongezaji thamani wa madini; na kuhamasisha uwekezaji na biashara ya madini. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: usimamizi endelevu wa rasilimali za madini; na kuendeleza utafiti; upimaji; na mafunzo kuhusu madini.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kupungua kwa asilimia ya mauzo ya madini ghafi nje kutoka asilimia 10.45 mwaka 2022/23 kufikia asilimia 9 mwaka 2023/24; kupunguza mauzo ya madini ghafi nje; na kuongezeka kwa ukuaji wa sekta ya madini na kutoka asilimia 10.9 mwaka 2022 hadi asilimia 11.3 mwaka 2023; kuongezeka kwa mchango wa sekta ya madini katika pato la taifa kutoka asilimia 9.1 mwaka 2023 hadi asilimia 10.1 mwaka 2024. Vilevile, mauzo yatokanayo ya bidhaa za madini nje ya nchi yameongezeka na kufikia asilimia 60 mwaka 2023; kuongezeka kwa idadi ya leseni katika shughuli za madini kutoka leseni 9,642 mwaka 2022/2023 hadi leseni 11,510 mwaka 2023/2024 zikiwemo leseni 8,795 za uchimbaji mdogo wa madini; kuongezeka kwa viwanda vya dhahabu vya uongezaji thamani kufikia 13. Jedwali 3.10 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya madini kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali 3.10: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Madini[5]**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Wastani wa ukuaji (%) | 5.2 | 6.7 | 9.6 | 10.9 | 11.3 | 8.6 (Robo ya Tatu, 2024) | 11.6 |
| 2. | Mchango kwenye Pato la Taifa (%) | 17.7 | 6.7 | 7.2 | 9.1 | 9.0 | 10.1 | 11.2 |
| 3. | Jumla ya mapato ya fedha za nje (dola za Marekani, milioni) | 2,280.5 | 3,310.7 | 3,046.2 | 3,395.3 | 3,551.4 | 4119.9 | 3,760.4 |
| 4. | Mauzo ghafi nje (%) | 15 | 15 | 11.6 | 10.45 | 9 | | 5 |
| 5. | Mchango katika mapato yote ya fedha za nje yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje (%) | 45.2 | | 45.9 | 56.0 | 60 | | 51.7 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Madini*

5 Kimaeneo ambayo hayana takwimu kwenye Jedwali 3.10 yametokana na kutokamilika kwa uchakataji wa takwimu katika kipindi husika.

### 3.3.10 Sekta ya Mazingira na Maliasili

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi 21 katika sekta ya mazingira na maliasili kwa lengo la kuimarisha utunzaji wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kuimarisha mifumo ya utunzaji wa misitu; kuongeza matumizi ya nishati mbadala; na kuongeza maeneo ya misitu ya kibiashara. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuongezeka kwa maeneo ya misitu ya kibiashara yaliyoanzishwa kutoka hekta 507, 274 mwaka 2023/24 kufikia hekta 550,000 mwaka 2024/25; na kupungua kwa kiwango cha uharibifu wa misitu kutoka hekta 469,420 mwaka 2023/24 zaidi ya lengo la hekta 234,710 mwaka 2024/25. Mafanikio haya yamepelekea kuongezeka kwa biashara ya kaboni; kupunguza athari za uharibifu wa mazingira; kuongeza uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na kuboresha afya za wananchi kupitia matumizi ya nishati safi.

Aidha, sekta binafsi na wadau wa maendeleo wameendelea kutoa mchango mkubwa katika shughuli za uhifadhi wa mazingira na maliasili pamoja na kuwekeza katika biashara ya kaboni. Jedwali 3.11 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya usimamizi wa mazingira na maliasili asilia kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali 3.11: Viashiria na Shabaha ya utekelezaji wa Sekta ya Usimamizi wa Mazingira na Maliasili Asilia**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Wastani wa Ukuaji (%) | 4 | 2.7 | 2.6 | 2.7 | 2.5 | 6 | 7 |
| 2. | Mchango katika Pato la Taifa kutokana na matumizi endelevu ya misitu, maji na rasilimali za bahari | 4 | 3.2 | 3.5 | 3.1 | 4.3 | 6 | 7 |
| 3. | Kiwango cha kupungua kwa uharibifu wa misitu (Reduced Deforestation Rate) (Ha.) | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 234,710 |
| 4. | Maeneo ya misitu ya kibishara (commercial forest plantation) yaliyoanzishwa (Ha) | 500,000 | 507,274 | 507,274 | 507,274 | 507,274 | 550,000 | 550,000 |
| 5. | Asilimia ya miradi mikubwa inayokidhi uchambuzi wa athari kwa mazingira (EIA) na kanuni za ukaguzi | 90 | 100 | 100 | 100 | 100 | 93 | 65 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira*

### 3.3.11 Sekta ya Utalii

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, sekta ya utalii ililenga kuendeleza mazao mapya ya utalii kwa ajili ya ukuaji wa uchumi endelevu; na kuendeleza kanda ya utalii wa kusini mwa Tanzania. Ili kufikia malengo haya, Serikali imeendelea kutekeleza Programu na Miradi ya Maendeleo 11 katika sekta ya utalii ambayo ipo katika hatua mbalimbali. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kuboresha usimamizi wa maliasili na kukuza utalii Kanda ya Kusini; kukabiliana na ujangili na biashara haramu ya nyara; uendelezaji wa utalii wa mikutano na matukio; kuboresha uhifadhi ndani ya maeneo ya hifadhi; na kuwezesha mnyororo wa thamani wa mazao ya nyuki.

Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii ni pamoja na: kuongezeka kwa mchango wa sekta ya utalii katika Pato la Taifa kutoka asilimia 17.2 mwaka 2023/24 hadi kufikia asilimia 17.5 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa mchango wa fedha za kigeni kutoka asilimia 25 mwaka 2023/24 hadi kufikia asilimia 26 mwaka 2024/25; na kuongezeka kwa idadi ya watalii nchini kutoka watalii 3,784,214 mwaka 2023/24 hadi watalii 5,360,247 mwaka 2024/25. sawa na asilimia 107.2 ya lengo la watalii 5,000,000 kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Aidha, Sekta binafsi imeendelea kuwekeza katika miundombinu ya kisasa ya hoteli, migahawa, huduma za usafiri wa watalii, kampeni za masoko ya kimataifa pamoja na ubunifu katika utoaji wa huduma. Vilevile, sekta hii imeendelea kuchangia katika ukuaji wa sekta nyingine kama usafiri, biashara, uwekezaji pamoja na sekta ya huduma. Jedwali 3.12 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya utalii kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali Na. 3.12: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji vya Sekta ya Utalii**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa (bei za sasa) (%) | 17.5 | 14.9 | 10.1 | 13.0 | 17.2 | 17.5 | 18.9 |
| 2. | Idadi ya watalii kutoka nje ya nchi | 1,527,230 | 620,867 | 922,692 | 1,454,920 | 1,808,205 | 2,141,895 | 5,000,000 |
| 3. | Idadi ya watalii ndani ya nchi | 959,831 | 788,933 | 2,363,260 | 1,084,737 | 1,976,009 | 3,218,352 | |
| 4. | Wastani wa idadi ya siku za kulala mtalii. | 13 | 10 | 10 | 9 | 10 | 10 | 14 |
| 5. | Wastani wa matumizi ya mtalii kwa siku kwa safari za vifurushi na zisizo za vifurushi (dola za Marekani) | - | 321<br>115 | 364<br>141 | 367<br>166 | 419<br>178 | 416<br>172 | 276<br>276 |
| 6. | Mchango katika mapato ya fedha za kigeni (%) | 25 | 5.3 | 21 | 25 | 25 | 26 | 27 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 7. | Mapato yatokanayo na watalii (dola za Marekani bilioni) | 2.6 | 0.7 | 1.3 | 2.5 | 3.9 | 4.1 | 6.0 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maliasili na Utalii*

### 3.3.12 Sekta ya Sanaa, Michezo na Ubunifu

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi 18 yenye lengo la kuongeza mchango wa sekta katika ukuaji wa uchumi na ajira. Katika kufikia lengo hilo, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: ujenzi na ukarabati wa viwanja kwa ajili ya mashindano ya AFCON; ujenzi wa vituo vya michezo na vituo vya kupumzikia wananchi; ujenzi wa vituo vya umahiri vya michezo; kuanzishwa kwa bodi ya ithibati ya wanahabari; utoaji wa mikopo kwa kazi za sanaa na utamaduni; na kukuza Kiswahili Kikanda na Kimataifa.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa shughuli hizo ni pamoja na: kuongezeka kwa idadi ya miundombinu ya michezo iliyoboreshwa nchini kote kutoka 68 mwaka 2023/24 kufikia 174 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya wanariadha wanaocheza nje ya nchi kutoka 17 mwaka 2023/24 kufikia 62 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya wataalamu wa Kiswahili wanaofanya kazi nje ya Tanzania kutoka 111 mwaka 2023/24 kufikia 384 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya machapisho ya Kiswahili yaliyouzwa nje ya nchi kutoka 242 mwaka 2023/24 kufikia 502 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa mchango wa sekta ya sanaa, michezo na ubunifu katika Pato la Taifa na kufikia asilimia 0.4; kuongezeka kwa ubora na ubunifu wa kazi za utamaduni na sanaa; kuongezeka kwa vipaji na kuongeza ushindani kimataifa; kuongezeka kwa utoaji wa habari kwa umma; kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari kwa kusajili na kutoa leseni kwa magazeti 357, redio 215, televisheni 56, redio za mtandaoni 27 na televisheni mtandao 413; na kutambulika kwa lugha ya Kiswahili kimataifa pamoja na kuwezesha upatikanaji wa fedha za kigeni.

Aidha, sekta binafsi imeendelea kuwa na mchango katika kuendeleza sekta ya sanaa, michezo na ubunifu kwa kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mwaka 2024/25 jumla ya kampuni 19 zilipewa kandarasi za kutekeleza miradi mbalimbali ya sekta ya habari, sanaa, michezo na ubunifu. Kati ya kampuni hizo, 10 ni za Watanzania na 9 ni za nje. Vilevile, sekta binafsi imeendelea kushiriki katika kuendeleza na kukuza vipaji vya michezo ambapo jumla ya vilabu vya michezo 692 vimeanzishwa. Pia, sekta binafsi inashiriki katika kukuza vipaji na ubunifu katika sanaa mbalimbali. Ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo umechangia ongezeko la ajira, kipato, kuchochea uchumi na kujenga uwezo wa sekta binafsi ya ndani. Jedwali 3.13 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya sanaa, michezo na ubunifu kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali 3.13: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sanaa, Utamaduni na Michezo**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya miundombinu ya michezo iliyoboreshwa nchini kote | 63 | 64 | 64 | 66 | 68 | 174 | 72 |
| 2. | Idadi ya miundombinu iliyojengwa/kukarabatiwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamaoyo (TaSUBa). | 35 | 48 | 50 | 52 | 53 | 58 | 40 |
| 3. | Idadi ya filamu na muziki zilizoidhinishwa, kusambazwa na kutumika | 15,303 | 2,962 | 3,763 | 3,201 | 4,070 | 4,342 | 25,735 |
| 4. | Idadi ya wasanii waliosajiliwa katika tasnia ya ubunifu | 3,462 | 3,931 | 4,299 | 5,254 | 6,473 | 7310 | 8,666 |
| 5. | Idadi ya wataalamu katika tasnia ya ubunifu waliopata mafunzo | 2,852 | 450 | 442 | 500 | 10,837 | 11,500 | 4,297 |
| 6. | Idadi ya michezo na mashindano ya kimataifa yaliyoandaliwa na Tanzania kushiriki | 178 | 0 | 98 | 135 | 157 | 110 | 350 |
| 7. | Idadi ya vibali vilivyotolewa kwa vyama vya michezo na wanamichezo binafsi | 178 | 0 | 57 | 45 | 194 | 110 | 400 |
| 8. | Idadi ya wanariadha wanaocheza nje ya nchi | 54 | - | 21 | 31 | 17 | 62 | 150 |
| 9. | Idadi ya wageni wanaoendesha shughuli za kuzalisha filamu nchini Tanzania. | 359 | 60 | 87 | 100 | 64 | 70 | 1,059 |
| 10. | Idadi ya wasanii/ wataalamu katika tasnia ya ubunifu/makundi yanayofanya maonesho yao nje ya nchi | 1,620 | 330 | 430 | 461 | 467 | 61 | 1,755 |
| 11. | Idadi ya wasanii wa nje/ wataalamu katika tasnia ya ubunifu wanaofanya maonesho yao nchini Tanzania | 720 | 142 | 153 | 162 | 167 | 2 | 2,312 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 12. | Idadi ya wataalamu wa Kiswahili wanaofanya kazi nje ya Tanzania | 56 | 64 | 71 | 95 | 111 | 384 | 656 |
| 13. | Idadi ya machapisho ya Kiswahili yaliyouzwa nje ya nchi | 200 | 252 | 2189 | 1640 | 242 | 502 | 700 |
| 14. | Idadi ya tuzo za kimataifa zilizoandaliwa na kutolewa kwenye utamaduni, sanaa na tasnia ya ubunifu | 47 | 38 | 41 | 188 | 62 | 68 | 130 |
| 15. | Idadi ya vikundi vya utamaduni na sanaa kutoka nje ya nchi vilivyoshiriki katika matamasha ya kimataifa yanayoandaliwa kila mwaka na TaSUBa. | 5 | 4 | 4 | 6 | 23 | 11 | 20 |
| 16. | Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya | 300 | 439 | 533 | 684 | 758 | 503 | 1,300 |
| 17. | Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa TaSUBa | 350 | 439 | 533 | 684 | 758 | 947 | 1200 |
| 18. | Idadi ya wilaya zinazofikiwa na matangazo ya TBC (TBCFM na TBCTaifa) | 102 | 119 | 121 | 134 | 137 | 138 | 161 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo*

### 3.3.13 Sekta ya Kukuza Uwekezaji na Biashara

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi 1,487 yenye lengo la kukuza uwekezaji na biashara katika sekta mbalimbali. Katika kufikia lengo hilo, Serikali ilitekeleza shughuli zifuatazo: Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI); kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; na kujenga uchumi shindani na shirikishi.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuongezeka kwa thamani ya miradi ya uwekezaji kutoka dola za Marekani milioni 6,796.09 mwaka 2023/24 kufikia dola za Marekani milioni 8,813 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya ajira kutokana na miradi ya uwekezaji kutoka 248,048 mwaka 2023/24 kufikia 280,000 mwaka 2024/25; kufutwa kwa tozo 383 ambapo kumerahisisha ufanyaji biashara na uwekezaji; na kuimarika kwa uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma hivyo kujenga uchumi shindani na shirikishi.

Aidha, sekta binafsi imeendelea kuchangia miradi ya uwekezaji na biashara ambapo jumla ya miradi 9,678 ya uwekezaji yenye thamani ya dola za Marekani milioni 8,658 imesajiliwa. Mafanikio ya miradi hii ni pamoja na kuongezeka kwa ajira rasmi na zisizo rasmi, kuongezeka kwa Pato la Serikali, upatikanaji wa malighafi za viwanda, na upatikanaji wa bidhaa ambazo awali zilikuwa zinaagizwa kutoka nje pamoja na kuongeza fedha za kigeni. Jedwali 3.14 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya kukuza uwekezaji na biashara kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali 3.14: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Kukuza Uwekezaji na Biashara**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na TIC na EPZA | 230 | 249 | 305 | 378 | 737 | 640 | 600 |
| 2. | Thamani ya miradi ya uwekezaji (dola za Marekani, Milioni) | 2,680.71 | 3,449.03 | 2,371.68 | 5,450.64 | 6,796.09 | 8,813 | 8,500 |
| 3. | Idadi ya ajira kutokana na miradi ya uwekezaji | 49,055 | 39,123 | 50,282 | 55,741 | 248,048 | 280,000 | 250,000 |
| 4. | Idadi ya kongano za uwekezaji | 10 | 12 | 13 | 14 | 27 | 21 | 5 |
| 5. | Idadi ya miongozo ya uwekezaji ya mikoa | 13 | 7 | 0 | 2 | 0 | 26 | 26 |
| 6. | Idadi ya Ofisi za Utoaji Huduma Mahala Pamoja | 11 | 13 | 13 | 13 | 13 | 15 | 18 |
| 7. | Kiasi cha ardhi ya uwekezaji iliyotengwa (ekari) | 90,990 | 98,861 | 99,735 | 159,813 | 214,972.94 | 391,030.94 | 528,917 |
| 8. | Idadi ya makongamano ya uwekezaji kimataifa | 21 | 49 | 63 | 89 | 204 | 180 | 150 |
| 9. | Idadi ya maboresho ya sheria na kanuni za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | | 35 | 42 | 55 | 66 | 80 | 88 |
| 10. | Idadi ya maboresho ya kufuta au kupunguza tozo, ada na ushuru katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | | 218 | 232 | 307 | 374 | 383 | 388 |

***Chanzo:*** *Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji*

### 3.3.14 Sekta ya Uwekezaji wa Umma na Sekta Binafsi

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imetekeleza programu na miradi mitano (5) yenye lengo la kutoa huduma, kuongeza ufanisi katika sekta za miundombinu, na kuboresha mazingira ya biashara. Shughuli zilizotekelezwa katika kufikia malengo hayo ni pamoja na: kuratibu majadiliano baina ya Serikali na wawekezaji; kupata washauri elekezi kwa ajili ya ufunguaji wa makampuni; na kufunguliwa kwa kampuni za uendeshaji (SPV). Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii ni pamoja na: kuanza kutekelezwa kwa miradi takribani mitano (5) ya ubia nchini; kuvutia uwekezaji kutoka nje; kuongeza mapato; kuongeza ajira; na kusaidia uendelezaji wa sekta nyingine.

Aidha, sekta binafsi imeendelea kushirikiana na Serikali ili kuwekeza katika miradi muhimu katika sekta za kilimo, viwanda, miundombinu, utalii, ujenzi, na mawasiliano. **Jedwali 3.15** linaonesha orodha ya miradi ya PPP ambayo ipo katika hatua za utekelezaji.

**Jedwali 3.15: Orodha ya Miradi Iliyopo katika Hatua za Utekelezaji**

| Na. | Kiashiria | Taasisi inayotekeleza | Mratibu | Thamani ya mradi (Dola za Marekani Milioni) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa jengo la kisasa la biashara la *Stop Business Complex.* | Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam | LGAs | 14.8 |
| 2 | Utoaji wa Huduma za Mabasi kwa Mradi wa *Dar Rapid Transit* Awamu ya Kwanza | Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi | LGAs | 81.4 |
| 3 | Utoaji wa Huduma za Mabasi kwa Mradi wa *Dar Rapid Transit* Awamu ya Pili | Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi | LGAs | 248.67 |
| 4 | Ujenzi wa barabara kipande cha kwaza kutoka Kibaha-Mlandizi hadi Chalinze – 78.9km | Wakala wa Barabara Tanzania | MDAs | 328 |
| 5 | Kuanzishwa kwa Vituo vya Ukaguzi wa Magari | Tanzania Police Corporation Sole | MDAs | 117 |
| | | | | |

***Chanzo:*** *Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi*

### 3.3.15 Sekta ya Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi mitatu (3) ya diplomasia ya uchumi yenye lengo la kuvutia uwekezaji wa nje na kufungua fursa za biashara. Shughuli zilizotekelezwa katika kuratibu diplomasia ya uchumi ni pamoja na: kuendesha makongamano yenye lengo la kuvutia uwekezaji; na uendelezaji wa miundombinu nje ya nchi.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuongezeka kwa idadi ya Hati za Makubaliano ya Pamoja zilizosainiwa kati ya Tanzania na nchi nyingine kutoka 78 mwaka 2023/24 kufikia 84 mwaka 2024/25 kulikochochea kuongezeka kwa

uwekezaji kutoka nje, fursa za ajira kwa Watanzania nje ya nchi, na kuimarisha shughuli za biashara. Jedwali 3.16 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya mahusiano ya kimataifa na diplomasia ya uchumi kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali 3.16: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya mikutano kati ya Tanzania na nchi moja moja, ya kikanda na kimataifa iliyoshiriki | 30 | 32 | 80 | 90 | 101 | 110 | 250 |
| 2. | Idadi ya Watanzania walioshiriki katika ulinzi wa amani nje ya nchi | - | - | 1401 | 1401 | 1532 | 1500 | 3,500 |
| 3. | Idadi ya ofisi na nyumba za kuishi zilizokarabatiwa | - | 4 | 4 | 4 | 4 | 4 | 14 |
| 4. | Idadi ya Hati za Makubaliano ya Pamoja zilizosainiwa kati ya Tanzania na nchi nyingine | 12 | 32 | 33 | 66 | 78 | 84 | 80 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki*

### 3.3.16 Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi ya elimu na maendeleo ya ujuzi ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na miradi ya kuendeleza elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu, ufundi na elimu ya juu. Afua zilizotekelezwa kupitia utekelezaji wa miradi hiyo ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa, maabara, mabweni, hosteli, ofisi, nyumba za walimu, karakana na majengo mtambuka katika shule, vyuo na taasisi za elimu na mafunzo pamoja na ununuzi na uwekaji wa vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia.

Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii ni pamoja na: kuongezeka kwa mchango wa sekta katika Pato la Taifa; kupungua kwa mdondoko wa wanafunzi katika ngazi zote za elimu; kuongezeka kwa usajili katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na elimu ya juu; kuongezeka kwa idadi ya walimu, wahadhiri na watumishi katika taasisi za elimu na mafunzo; kuimarika kwa uwiano wa wanafunzi kwa darasa kutoka 68:1 mwaka 2023/24 kufikia 63:1 mwaka

2024/25 katika elimu ya msingi; kuimarika kwa uwiano wa wanafunzi kwa darasa kutoka 37:1 mwaka 2023/24 kufikia 34:1 mwaka 2024/25 katika elimu ya sekondari ya chini; kuongezeka kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka 220,278 mwaka 2023/24 hadi kufikia 250,567 mwaka 2024/25; na kuongezeka kwa asilimia ya wanafunzi wanaohitimu masomo ya sayansi na uhandisi kwa mwaka kutoka asilimia 16.2 mwaka 2022/23 kufikia 17.2 mwaka 2023/24 .

Serikali imefanya mageuzi katika sekta ya elimu kwa kufanya mapitio ya Sera ya Eimu na maboresho ya mtaala wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu ambapo msisitizo umewekwa katika utoaji wa elimu ya amali (elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi) kuanzia ngazi ya elimu ya msingi hadi elimu ya juu. Utekelezaji wa mabadiliko hayo utawezesha Tanzania kuzalisha rasilimali watu yenye umahiri katika nyanja mbalimbali inayokidhi mahitaji ya soko la ajira.

Aidha, sekta binafsi imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza sekta ya elimu kwa kushiriki katika afua mbalimbali ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya shule na vyuo pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mwaka 2024/25 jumla ya shule binafsi 6,422 zimeendelea kutoa fursa ya elimu kwa Watanzania. Shule hizo zimeandikisha jumla ya wanafunzi 1,083,888 ambapo elimu ya awali wanafunzi 118,010, elimu ya msingi wanafunzi 651,210 na elimu ya sekondari wanafunzi 314,668. Vilevile, kwa mwaka 2024 sekta binafsi imewezesha ajira kwa walimu 64,756 ambapo walimu 7,228 elimu ya awali, msingi 35,473 na sekondari 22,055. Aidha, kuimarika kwa ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya elimu na maendeleo ya ujuzi kumechangia ongezeko la ajira, kipato pamoja na kuchochea uchumi na kujenga uwezo wa sekta binafsi ya ndani. Jedwali 3.17 linaonesha mwenendo wa utekelezaji wa viashiria vya sekta ya elimu kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali 3.17: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Elimu**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | **Elimu** | | | | | | | |
| **1.1** | **Elimu ya Awali** | | | | | | | |
| 1.1.1 | Kiwango cha uandikishaji rika lengwa (% ya wanaostahili) | 78.5 | 78.5 | 76.9 | 83.9 | 89.5 | 89.5 | 100 |
| 1.1.2 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa | 1:149 | 1:130 | 1:123 | 1:117 | 1:127 | 1:151 | 80 |
| **1.2** | **Elimu ya Msingi** | | | | | | | |
| 1.2.1 | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) | 110.6 | 110.6 | 109.7 | 108.5 | 98.2 | 84.2 | 100 |
| 1.2.2 | Kiwango cha uandikishaji wa rika lengwa | 95.7 | 95.7 | 95.3 | 94.4 | 86.0 | 79.6 | 100 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1.2.3 | Asilimia ya kundirika la wanafunzi waliofaulu mtihani wa Elimu ya Msingi | 82.24 | 82.68 | 81.90 | 79.62 | 80.58 | N/A | 100 |
| 1.2.4 | Uwiano wa Idadi ya wanafunzi wa elimu ya msingi kwa mwalimu | 1:54 | 1:51 | 1:56 | 1:57 | 1:55 | 1:56 | 1:50 |
| 1.2.5 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa kitabu | 1:4 | 1:3 | 1:2 | 1:2 | 1:2 | 1:2 | 1:1 |
| 1.2.6 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa | 1:75 | 1:75 | 1:74 | 1:70 | 1:68 | 1:63 | 1:60 |
| 1.2.8 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi wa kiume kwa tundu la choo | 1:54 | 1:54 | 1:51 | 1:52 | 1:46 | 1:43 | 1:25 |
| 1.2.7 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi wa kike kwa tundu la choo | 1:51 | 1:51 | 1:48 | 1:48 | 1:43 | 1:47 | 1:20 |
| 1.2.8 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa dawati | 1:4 | 1:4 | 1:4 | 1:4 | 1:4 | 1:4 | 1:2 |
| 1.2.9 | Asilimia ya shule za msingi zenye umeme | 43.5 | 42.2 | 48.8 | 56.0 | 61.9 | 68.0 | 60.0 |
| **1.3** | **Elimu ya Sekondari ya Chini (I – IV)** | | | | | | | |
| 1.3.1 | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) | 46 | 46.0 | 47.4 | 48.2 | 52.7 | 51.7 | 48 |
| 1.3.2 | Asilimia ya uandikishaji wa watoto wenye umri wa rika lengwa ikilinganishwa na idadi ya watoto wote wenye umri wa kwenda shule | 36 | 36.0 | 37.0 | 38.3 | 41.8 | 40.6 | 42 |
| 1.3.3 | Uwiano wa Idadi ya wanafunzi wa elimu ya sekondari kwa mwalimu | 1:23 | 1:23 | 1:24 | 1:25 | 1:26 | 1:26 | 1:20 |
| 1.3.4 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi wa elimu ya sekondari kwa darasa | 1:41 | 1:40 | 1:42 | 1:36 | 1:37 | 1:34 | 1:40 |
| 1.3.5 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi wa sekondari kwa tundu la choo | 1:27 | 1:20 | 1:27 | 1:28 | 1:34 | 1:28 | 1:20 |
| 1.3.6 | Asilimia ya shule za sekondari zenye umeme | 69.8 | 69.8 | 73.9 | 77.2 | 77.5 | 81.4 | 85 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1.3.7 | Asilimia ya kundirika la wanafunzi waliofaulu mtihani wa elimu ya sekondari ya chini | 80.65 | 85.84 | 87.3 | 87.79 | 89.37 | NA | 90.0 |
| **1.4** | **Elimu ya Sekondari ya Juu (V – VI)** | | | | | | | |
| 1.4.1 | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) | 6.9 | 6.9 | 6.7 | 7.6 | 7.7 | 9.1 | 10 |
| 1.4.2 | Kiwango cha uandikishaji rika lengwa (% ya wanaostahili) | 3.3 | 3.3 | 3.4 | 4.0 | 4.1 | 5.2 | 8 |
| 1.4.3 | Uandikishaji halisi wa wanafunzi wa kiume (%) | 3.3 | 3.3 | 3.4 | 3.9 | 4.1 | 5.0 | 4 |
| 1.4.4 | Uandikishaji halisi wa wanafunzi wa kike (%) | 3.2 | 3.2 | 3.4 | 4.1 | 4.1 | 5.4 | 4 |
| 1.4.5 | Asilimia ya wanafunzi wanaofaulu mtihani wa kidato cha VI | 99.51 | 99.5 | 99.6 | 99.9 | 99.9 | NA | 100 |
| **1.5** | **Elimu ya Juu** | | | | | | | |
| 1.5.1 | Idadi ya wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu | 132,392 | 145,000 | 177,892 | 202,016 | 220,278 | 250,567 | 180,000 |
| 1.5.2 | Idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu | 60,940 | 60,940 | 54,810 | 57,742 | 56,520 | N/A | 70,081 |
| 1.5.3 | Idadi ya wahitimu kwa wanafunzi wa kiume | 34,513 | 34,513 | 29,780 | 30,375 | 27,574 | | 39,690 |
| 1.5.4 | Idadi ya wahitimu kwa wanafunzi wa kike | 26,427 | 26,427 | 25,030 | 27,367 | 28,946 | | 44,700 |
| **1.6** | **Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi** | | | | | | | |
| 1.6.1 | Kiwango cha udahili jumla (%) | 4.5 | 5.8 | 7.4 | 6.9 | 8.0 | NA | 6.0 |
| 1.6.2 | Idadi ya wanafunzi wanaohitimu kwa mwaka | 86,547 | 146,671 | 154,800 | 140,014 | 89,967 | NA | 120,000 |
| 1.6.3 | Asilimia ya wanafunzi wanaohitimu masomo ya sayansi na uhandisi kwa mwaka | 36 | 18.1 | 17.3 | 16.2 | 17.2 | NA | 40 |
| 1.6.4 | Asilimia ya Wanafunzi wa kike wanaohitimu kwa mwaka | 42 | 32.6 | 33.20 | 33.21 | 35.7 | | 43 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia*

### 3.3.17 Sekta ya Afya

Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali kwa kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya, kuajiri wataalamu wa afya na kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za afya ambapo programu na miradi 14 imetekelezwa katika maeneo mbalimbali.

Programu na miradi hiyo inahusisha ununuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa, chanjo, vifaa na vifaatiba; ujenzi wa miundombinu ya afya ikiwemo hospitali mpya za halmashauri, ukarabati wa hospitali kongwe, ujenzi wa vituo vya afya, ukamilishaji wa zahanati, ujenzi wa nyumba za watumishi, ujenzi na upanuzi wa Hospitali za rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa; na utolewaji wa mafunzo kwa wataalam wa afya katika ngazi mbalimbali ikiwemo ngazi ya ubingwa na ubingwa bobezi.

Jitihada hizo zimepelekea kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya zikiwemo zahanati, vituo vya afya, Hospitali za Halmashauri, Hospitali za rufaa za Mikoa, Hospitali za rufaa za Kanda, Hospitali Maalum na kuboresha Hospitali ya Taifa ya Muhimbili; kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya; na kuongezeka kwa wataalam wa kada za afya.

Vilevile, utekelezaji wa programu na miradi hiyo kumewezesha kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi kufikia 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022 na kuvuka lengo la vifo 180 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa wastani wa idadi ya uzazi uliohudumiwa na mhudumu wa afya mwenye ujuzi kufikia asilimia 94.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na lengo la asilimia 85 kwa kila vizazi 1000 mwaka 2025/26. Aidha, wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya afya kufikia asilimia 86 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 80 mwaka 2020; Idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa kila vizazi hai 1000 kufikia asilimia 43 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 67 mwaka 2021; wastani wa umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 67.8 (2023) hadi makadirio ya miaka 68.0 (2024); na kuwezesha asilimia 80 ya wananchi kupata huduma za afya ndani ya kilomita 5.

Mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya kwa kiasi kikubwa yanachangiwa pia na uwepo wa uwekezaji wa sekta binafsi. Hadi 2024 sekta binafsi imewekeza kwenye sekta ya afya kwa kujenga na kuendesha vituo vya kutolea huduma za afya 2,297 ambapo kati ya hivyo zahanati ni 1,794 ikilinganishwa na 1,698 mwaka 2021, vituo vya afya ni 295 ikilinganishwa na 277 mwaka 2021 na hospitali ni 208 ikilinganishwa na hospitali 197 mwaka 2021. Ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ya afya kumechangia kupatikana kwa ajira moja kwa moja kwa wataalam walioajiriwa katika zahanati, vituo vya afya na hospitali. Jedwali 3.18 linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya afya kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano.

**Jedwali 3.18: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Afya**[6]

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya vifo vya watoto wachanga kwa kila vizazi hai 1000 | 26 (2010 TDHS) | 25 (2015-16 TDHS-MIS) | 24 (2015-16 TDHS-MIS) | 24 (2022 TDHS-MIS) | 24 (2022 TDHS-MIS) | 24 (2022 TDHS-MIS | 15 |
| 2. | Idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa kila vizazi hai 1000 | 81 (2010 TDHS) | 67 (2015-16 TDHS-MIS) | 43 (2022 TDHS-MIS) | 43 (2022 TDHS-MIS) | 43 (2022 TDHS-MIS) | 43 (2022 TDHS-MIS) | 40 |
| 3. | Uzazi uliohudumiwa na mfanyakazi wa afya mwenye ujuzi | 80 | 92.3 | 93.6 | 94.4 | 94.6 | 94.7 (2023–AHSP) | 85 |
| 4. | Wastani wa umri wa kuishi (miaka) | 66.1 | 66.7 | 65.4 | 67.6 | 67.8 (Sensa-2022) | 68 (Sensa-2022) | 68 |
| 5. | Kiwango cha maambukizi ya VVU kitaifa (%) | 4.7 | 4.9 | 4.9 | 4.9 | 4.4 | 4.4 (THIS 2022/ 2023) | 1,300 |
| 6. | Matumizi ya Serikali katika huduma za afya (%) | 10 | 10.6 | 10 | 9.0 | 9.1 | 10.3(2023-AHSP) | 12.2 |
| 7. | Idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi kwa kila vizazi hai 100,000 | 454 (2010 TDHS) | 530 (2015-16 TDHS-MIS) | 220 | 220 | 104 (2022 TDHS-MIS) | 104 (2022 TDHS-MIS) | 180 |
| 8. | Matumizi ya Serikali katika afya (% ya matumizi yote ya Serikali) | 10 | 10.6 | 10 | 9.0 | 9.1 | 10.3 (2023-AHSP) | 12.2 |

***Chanzo:*** *: Wizara ya Afya na Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

## 3.3.18 Sekta ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira

Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika maeneo mbalimbali nchini. Programu hiyo imewezesha utekelezaji wa jumla ya programu na miradi 482. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kuongeza usambazaji wa huduma ya maji safi na salama mijini na vijijini; utunzaji wa vyanzo vya maji; kuendeleza miundombinu ya usafi wa mazingira; na kuendelea kuratibu shughuli za sekta ya maji.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi ya majisafi na usafi wa mazingira ni pamoja na: kuongezeka kwa asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba kutoka 79.6 mwaka 2023/24 kufikia 83 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa uwiano wa kaya za vijijini zenye miundombinu iliyoboreshwa ya usafi wa mazingira kutoka asilimia 77.5 mwaka 2023/24 kufiki asilimia 78.5 mwaka 2024/25; kupungua kwa kiwango cha upotevu wa maji katika makao makuu ya mikoa kutoka asilimia 35.3 mwaka 2023/24 kufikia 33.4 mwaka

6 Taarifa ya TDHS-MIS hutolewa kila baada ya miaka mitano, hivyo takwimu zilizotumika kwenye ulinganishi ni za mwaka 2022

2024/25. Vilevile utekelezaji wa miradi na programu hizi umechangia kupungua kwa milipuko ya magonjwa; kuongezeka kwa muda wa uzalishaji hususan kwa wananchi wanaoishi vijijini; kuongezeka kwa uzalishaji viwandani hususan katika Jiji la Dar es Salaam; na kuongeza mapato yatokanayo na mauzo ya maji pamoja na hifadhi ya mazingira. Aidha mafanikio yaliyoainishwa pia yamechangiwa na sekta binafsi ambayo imeshiriki katika kutekeleza miradi ya maji kama vile makampuni ya kutengeneza na kuuza vifaa yakiwemo mabomba na viungio vyake pamoja na washauri elekezi na wakandarasi takriban 161 ambao wanashiriki katika utekelezaji wa miradi ya maji nchini. **Jedwali 3.19** linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya maji kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali Na.3.19: Viashiria na Shabaha vya Utekelezaji wa sekta ya Usambazaji wa Maji na Huduma za Usafi wa Mazingira**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba au maji yalivyolindwa kama chanzo kikuu | 70 | 72.3 | 74.5 | 77 | 79.6 | 83 | 85 |
| 2. | Uwiano wa kaya za vijijini zenye miundombinu iliyoboreshwa ya usafi wa mazingira | 36 | 47.3 | 60.4 | 73.5 | 77.5 | 78.5 | 60 |
| 3. | Asilimia ya watu katika makao makuu ya mikoa wanaopata maji ya bomba au maji yaliyolindwa | 84 | 85 | 86.5 | 88 | 90 | 91.6 | 95 |
| 4. | Asilimia ya kaya katika makao makuu ya mikoa zilizounganishwa kwenye mfumo rasmi wa majitaka | 13 | 11 | 13 | 13 | 14 | 13 | 30 |
| 5. | Asilimia ya upotevu wa maji (NRW) katika makao makuu ya mikoa | 30 | 36.8 | 35.7 | 35.3 | 35.3 | 33.4 | 20 |
| 6. | Asilimia ya watu katika makao makuu ya wilaya na miji midogo wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu | 70 | 67 | 72 | 73.4 | 74.5 | 74.5 | 85 |
| 7. | Asilimia ya watu katika jiji la Dar es Salaam wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji salama kama chanzo kikuu | 85 | 87 | 89 | 90 | 92.5 | 93 | 95 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 8. | Asilimia ya kaya katika jiji la Dar es Salaam waliounganishwa kwenye mfumo rasmi wa majitaka | 13 | 13 | 11 | 13 | 12.4 | 13 | 30 |
| 9. | Idadi ya maboresho ya sheria na kanuni za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | 35 | 38.3 | 39.2 | 41.5 | 39.5 | 43.2 | 20 |
| 10. | Idadi ya maboresho ya kufuta au kupunguza tozo, ada na ushuru katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | 18 | 18 | 34 | 34 | 59 | 68 | 80 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maji*

### 3.3.19 Sekta ya Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuendeleza upimaji wa maeneo ya makazi, biashara, uwekezaji na huduma za jamii. Hii ni kwa kutambua kuwa ardhi iliyopimwa na kupangwa ni kichocheo muhimu cha shughuli za kiuchumi na kijamii, maendeleo ya makazi na miji, uhifadhi wa mazingira na udhibiti wa mabadiliko ya tabianchi. Katika kufikia lengo hilo, yafuatayo yalitekelezwa: Upimaji, upangaji na umilikishaji wa ardhi; urasimishaji wa ardhi; uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji; uthamini wa mali; na ujenzi wa nyumba na makazi.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuongezeka kwa idadi ya mali zilizorasimishwa katika makazi yasiyo rasmi kutoka 2,602,711 mwaka 2023/24 kufikia 3,102,715 mwaka 2024/25; na kuongezeka kwa idadi ya mabaraza ya ardhi yanayofanya kazi kutoka 105 mwaka 2023/24 kufikia 112 mwaka 2024/25. Mafanikio mengine ni pamoja na kupungua kwa migogoro ya ardhi; kuongezeka kwa mikopo kutoka taasisi za kifedha inayotokana na dhamana ya ardhi iliyopimwa; kuongezeka kwa wawekezaji kutokana na uwepo wa ardhi iliyopimwa; kuongezeka kwa mchango wa sekta ya ardhi katika Pato la Taifa; na kuinua kiwango cha maisha ya wananchi kutokana na uwepo wa nyumba bora pamoja na kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na kodi ya ardhi.

Aidha, mchango wa sekta binafsi umeendelea kukua katika kushirikiana na Serikali kuendeleza mipango miji ambapo jumla ya viwanja 116,732 kati ya viwanja 129,702 vilipimwa na sekta binafsi. Vilevile sekta binafsi imeendelea kushirikiana na shirika la nyumba la Taifa (NHC) ambapo jumla ya miradi ya ubia 20 inaendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali

nchini. **Jedwali 3.20** linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya Mipango, Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali Na. 3.20: Viashiria na Shabaha vya utekelezaji wa sekta ya Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya mali zilizorasimishwa katika makazi yasiyo rasmi | 70 | 72.3 | 74.5 | 77 | 79.6 | 83 | 85 |
| 2. | Asilimia ya eneo la ardhi yenye makazi yasiyo rasmi | 36 | 47.3 | 60.4 | 73.5 | 77.5 | 78.5 | 60 |
| 3. | Eneo la ardhi lililotengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma (ekari) | 84 | 85 | 86.5 | 88 | 90 | 91.6 | 95 |
| 4. | Idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohuishwa | 13 | 11 | 13 | 13 | 14 | 13 | 30 |
| 5 | Idadi ya viwanja vilivyotengwa | 30 | 36.8 | 35.7 | 35.3 | 35.3 | 33.4 | 20 |
| 6 | Idadi ya mashamba yaliyotengwa | 70 | 67 | 72 | 73.4 | 74.5 | 74.5 | 85 |
| 7 | Idadi ya ramani za msingi zilizohuishwa kwa eneo | 85 | 87 | 89 | 90 | 92.5 | 93 | 95 |
| 8 | Uwiano wa vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi (%) | 19.3 | 19.3 | 20.9 | 23.2 | 33.5 | 34.5 | 52.7 |
| 9 | Idadi ya mabaraza ya ardhi yanayofanya kazi | 57 | 68 | 81 | 93 | 105 | 112 | 139 |
| 10 | Asilimia ya ardhi iliyopimwa | 25 | 25 | 25 | 25 | 26 | 26 | 37 |
| 11 | Idadi ya leseni za makazi zilizotolewa katika makazi yasiyo rasmi | 1,738 | 1,738 | 23,862 (2021/22) | 23,862 (2021/22) | 23,862 (2021/22) | 23,862 (2021/22) | 20,000 |
| 12 | Idadi ya ramani za msingi zilizohuishwa kwa eneo | 1 | 19 | 62 | 84 | 86 | 88 | 26 |
| 13 | Idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohuishwa | 24 | 25 | 27 | 28 | 28 | 28 | 54 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*

### 3.3.20 Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kutekeleza programu na miradi mbalimbali ya maendeleo yenye lengo la kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo. Kwa mwaka 2024/25 jumla ya miradi nane (8) ya maendeleo imeendelea kutekelezwa.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na maendeleo ya sekta ni pamoja na: kuongezeka kwa idadi ya vituo vya malezi ya watoto vilivyosajiliwa kutoka 4,068 mwaka 2023/24 kufikia 4,800 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya wazee wasiojiweza wanaopata huduma za bima ya afya bure kutoka 365,284 mwaka 2023/24 na kufikia wazee 432,642 mwaka 2024/25; na kutolewa kwa vitambulisho kwa ajili ya msamaha wa matibabu na Bima ya Afya kwa wazee wasiojiweza 2,199,588 kati ya wazee wasiojiweza 4,975,473 waliotambuliwa. Mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa muda kwa wanawake kujihusisha na shughuli za kiuchumi; kuwezeshwa kwa wananchi kiuchumi; kupungua kwa ukatili wa kijinsia; uhakika wa chakula na lishe bora; pamoja na kuimarika kwa uwajibikaji.

Vilevile, Mashirika yasiyo ya kiserikali yameendelea kuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa shughuli zinazolenga kuleta maendeleo ya jamiii, ambapo utekelezaji wa miradi ya afua za afya, nishati, mazingira, uwezeshaji jamii, ulinzi wa jamii, elimu, kilimo, utawala bora, maji, haki za binadamu na jinsia ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. **Jedwali 3.21** linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya ustawi na maendeleo ya jamii kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali Na. 3.21: Viashiria na Shabaha vya Utekelezaji wa Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | Shabaha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya vituo vya malezi ya watoto vilivyosajiliwa | 1,543 | 1,543 | 2,714 | 3,233 | 4,068 | 4,800 | 7,500 |
| 2. | Idadi ya wazee wasiojiweza wanaopata huduma za bima ya afya bure | 166,866 | 166,866 | 201,509 | 262,513 | 365,284 | 432,642 | 574,321 |
| 3. | Idadi ya watoto wanaolelewa baada ya mapatano | 12,068 | 12,068 | 26,903 | 32,905 | 46,473 | 48,051 | 50,000 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum*

Serikali iliendelea na mikakati ya kuboresha ustawi wa jamii na kupunguza umaskini uliokithiri kupitia programu mbalimbali ikiwemo Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini - TASAF. Utekelezaji wa Mpango huo, ulihusisha uhawilishaji wa fedha kwa kaya maskini; kutoa ajira za muda mfupi kwa kaya za walengwa; kutekeleza miradi katika sekta za afya, elimu, maji, mazingira na barabara; na kuhamasisha uundaji wa vikundi vya kuweka akiba, kukopeshana na kuwekeza kwenye miradi ya uzalishaji mali kupitia vikundi hivyo. Lengo likiwa ni kupunguza umaskini na kujenga rasilimali watu kwa kizazi kijacho.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua hizi ni pamoja na: kusogeza karibu huduma za kijamii (elimu, afya na maji) katika maeneo ya makazi. Hii imechangia kuongeza uandikishaji na ufaulu wa watoto katika elimu ya msingi na upatikanaji wa huduma ya afya msingi kwa mama wajawazito, watoto na jamii kwa ujumla na hivyo kupunguza ujinga na athari za magonjwa kwa jamii hasa kwa kaya maskini; kuongezeka kwa vipato kwa wanufaika kutokana na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji mali ambapo wananchi waliwezeshwa kuanzisha miradi midogo ya kujiongezea kipato kupitia ruzuku na mikopo iliyotolewa kwa walengwa. Aidha, Mpango umewezesha kuboresha maisha ya kaya 400,000 zenye wanakaya zaidi ya 1,800,000 kuwa na shughuli zenye vipato endelevu na kupunguza umaskini uliokithiri.

### 3.3.21 Kuendeleza Ujuzi

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuendeleza ujuzi. Afua zilizotekelezwa ni pamoja na: mafunzo ya kukuza ujuzi kwa njia ya uanagenzi; mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu; mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi; urasimishaji wa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo; na kukuza kazi za staha nchini.

Mafanikio ya utekelezaji wa afua hizi ni pamoja na: kuongezeka kwa upatikanaji wa ajira kupitia taasisi za umma na binafsi; utoaji wa ruzuku kwa vyama vya watu wenye ulemavu; mikopo kwa vikundi/makampuni ya vijana, pamoja na utoaji wa mafunzo ya uwezeshaji ujuzi na stadi za kazi; umewezesha uzalishaji wa nguvukazi yenye ujuzi. Mafanikio haya yanachangia kukuza uzalishaji viwandani, ujenzi wa uchumi shindani na jumuishi, na kuwa na ustawi wa rasilimali watu. Jedwali 3.22 linaonesha mwenendo wa viashiria vya afua za kuendeleza ujuzi kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Utekelezaji wa afua za kukuza ujuzi umewezeshwa na mchango wa sekta binafsi kwa kutumia tozo ya uendelezaji ujuzi (SDL) pamoja na kugharamia mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu. Aidha, miongozo ya usimamizi wa mafunzo ya uanagenzi na mafunzo ya uzoefu mahali pa kazi ilitolewa kupitia taasisi za sekta binafsi kutoka Umoja wa Waajiri Tanzania (ATE), Shirikisho la Vyama vya wafanyakazi (TUCTA) na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ambao walipewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa programu ya kukuza ujuzi.

**Jedwali 3.22: Viashiria na Shabaha vya Utekelezaji wa Afua za Kuendeleza Ujuzi[7]**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | | Shabaha |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1 | Idadi ya watu wenye mafunzo ya uanagenzi | 46,200 | 14,440 | 22,200 | 11,973 | 6,300 | 8,250 | 46,200 |
| 2 | Idadi ya watu wanaotumia teknolojia ya kisasa kwenye kilimo | 40,000 | 8,980 | 4,480 | - | - | - | 40,000 |
| 3 | Idadi ya watu walioshiriki mafunzo ya utarajali (Internship) | 30,000 | 4,118 | 2,490 | 1,888 | 3,085 | 1,861 | 30,000 |

***Chanzo:*** *Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu)*

### 3.3.22 Sekta ya Utawala Bora na Utawala wa Sheria

Sekta ya utawala bora na utawala wa sheria inahusisha utekelezaji wa programu na mikakati ifuatayo: Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma; Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji ambapo awamu ya tatu imekamilika na kuzinduliwa kwa awamu ya nne; Programu ya Maboresho ya Mahakama; usalama wa raia na mali zao; uendelezaji wa nyumba za viongozi; na uendelezaji wa mji wa Serikali Dodoma.

i. **Utumishi na Utawala Bora**

Serikali imeendelea kuimarisha utawala bora kwa kufanya maboresho katika utumishi wa umma kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa programu hii ni pamoja na; kuongezeka kwa uwajibikaji wa taasisi za umma; kuongezeka kwa ufanisi katika utoaji wa huduma; kutolewa kwa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa e-Watumishi; na kuongezeka kwa uwazi na haki katika mchakato wa ajira Serikalini. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza utumishi wa umma kwa kuwapokea watumishi katika taasisi zao.

Aidha, kupitia TAKUKURU Serikali iliendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa kupitia Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu na kuanza Awamu ya Nne. Shughuli zilizotekelezwa kupitia mkakati huo ni pamoja na: ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo; operesheni za uchunguzi; ufuatiliaji wa rasilimali; na uelimishaji wa umma kuhusu mapambano dhidi ya rushwa.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na kukabiliana na vitendo vya rushwa na ufisadi nchini ni kuongezeka kwa nidhamu, uwazi, uadilifu na uwajibikaji katika nyanja mbalimbali zikiwemo za utumishi wa umma, biashara, uwekezaji, ukusanyaji mapato, pamoja na matumizi ya madaraka na fedha za umma. Kuimarika kwa utawala bora, kuongezeka kwa ubora

7 Sehemu ya viashiria ambazo ziko wazi inatokana na takwimu hizo kutozalishwa kwa mwaka husika

wa utoaji wa huduma na kufikiwa kwa thamani ya fedha kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mafanikio haya yameijengea imani Serikali kwa wadau wa maendeleo na wananchi na kuipa uwezo imara wa kukuza uchumi na kuongeza kasi ya utoaji huduma bora kwa umma.

ii. **Utawala wa Sheria**

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kuboresha mifumo ya utoaji na upatikanaji wa haki ambao ni muhimu katika kuimarisha usawa na ustawi wa jamii. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kutoa huduma za msaada wa kisheria kupitia kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia; kuanzishwa kwa madawati ya msaada wa kisheria katika mamlaka zote za serikali za mitaa; kuboresha mifumo na miundombinu ya mahakama pamoja na majengo jumuishi ya utoaji haki; kuongeza matumizi ya TEHAMA katika mifumo ya utoaji haki; na kuimarisha usajili wa matukio muhimu ya binadamu pamoja na usajili na ufilisi katika mikoa yote ya Tanzania Bara na kuratibu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kusogeza huduma za kisheria kwa wananchi na kusaidia kuleta amani na utulivu; kupunguza gharama na umbali katika kutafuta msaada wa kisheria; kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wakati; kuimarisha upatikanaji wa haki za msingi zinazotokana na nyaraka za kisheria za usajili wa matukio muhimu ya binadamu; na kuvutia uwekezaji kutokana na uwepo wa mifumo ya utoaji haki. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imewezesha uboreshaji wa mifumo ya utoaji na upatikanaji wa haki kupitia uhamasishaji na utoaji wa elimu juu ya masuala ya kisheria. Sekta hizo ni pamoja na Taasisi za kibenki, Makampuni ya Simu na Mashirika ya watoa huduma za msaada wa kisheria. **Jedwali 3.23** linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta ya Mifumo ya Utoaji Haki kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali Na. 3.23: Viashiria na Shabaha vya Utekelezaji wa Sekta ya Mifumo ya Utoaji Haki**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | | Shabaha |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1 | Asilimia ya raia wanaoishi katika mikoa yenye Mahakama Kuu inayofanya kazi | 69 | 77 | 77 | 83 | 83 | 83 | 100 |
| 2 | Asilimia ya kesi zilizohudumiwa na watoa msaada wa huduma za kisheria | 0.13 | 8.2 | 11.4 | 13.97 | 13.97 | 15 | 20 |
| 3 | Idadi ya IJCs zilizojengwa na zinazofanya kazi katika maeneo yaliyo chaguliwa | 10 | 6 | 3 | 0 | 9 | 0 | 28 |

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | | Shabaha |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 4 | Idadi ya majengo ya mahakama ya wilaya yaliyojengwa | 64 | 18 | 12 | 7 | 6 | 7 | 139 |
| 5 | Idadi ya majengo ya mahakama ya mwanzo yaliyojengwa | 649 | 7 | 7 | 4 | 1 | 72 | 791 |
| 6 | Idadi ya ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilizojengwa mikoani | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 3 | 10 |
| 7 | Idadi ya ofisi za NPS zilizojengwa mikoani | 1 | 0 | 0 | 4 | 6 | 4 | 7 |
| 8 | Idadi ya ofisi za NPS zilizojengwa wilayani | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 11 |
| **Ufanisi wa Huduma ya Utoaji Haki** | | | | | | | | |
| 10 | Wastani wa idadi ya siku tangu kufunguliwa kwa kesi na kutolewa hukumu | 390 | 312 | 166 | 239 | 242 | 78 | 350 |
| 11 | Asilimia ya watu walioridhishwa na huduma za mahakama | 78 | 78 | 78 | 88 | 88 | 88 | 80 |
| 12 | Wastani wa idadi ya siku tangu kufunguliwa kwa kesi na kutolewa hukumu katika Mahakama ya Biashara | 480 | 390 | 365 | 324 | 231 | 231 | 350 |
| 13 | Asilimia ya mlundikano wa kesi, kwa jumla ya kesi zote zinazosubiri maamuzi | 5 | 13 | 9 | 3 | 5 | 4 | 2 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Katiba na Sheria*

### iii. Amani, Utulivu na Usalama

Katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali ilipanga kuimarisha usalama wa raia na mali zao nchini kwa kupunguza kiwango cha uhalifu nchini; kuongeza utambuzi na usajili wa raia kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA); na kupunguza kiwango cha ajali barabarani.

Ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli hizo, Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi 44 kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa vyombo vya usalama nchi na kudumisha amani, utulivu na usalama nchini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa programu na miradi hiyo ni pamoja na kuongezeka kwa kiwango cha kupungua kwa asilimia za kiwango cha ajali za barabarani kutoka asilimia 54 mwaka 2023/24 kufikia asilimia 58 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa kiwango cha ushiriki wa jamii katika shughuli za usalama kutoka asilimia 50 mwaka 2023/24 kufikia asilimia 55 mwaka 2024/25; na kuongezeka kwa idadi ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa na NIDA kutoka 27,286,749 mwaka 2023/24 kufikia 34,080,610 mwaka 2024/25.

Aidha, Serikali imeendelea kusimamia shughuli za kampuni binafsi za ulinzi kwa lengo la kuimarisha usalama wa raia na mali zao; na kuimarisha utekelezaji wa shughuli za uchumi na maendeleo nchini. **Jedwali 3.24** linaonesha mwenendo wa viashiria vya sekta amani, utulivu na usalama kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Jedwali Na. 3.24: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Amani, Utulivu na Usalama**

| Na. | Kiashiria | Mwenendo wa utekelezaji | | | | | | Shabaha |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Kiwango cha kupungua kwa uhalifu nchini (%) | 5.2 | - 7.5 | - 1.9 | 4.3 | 3.2 | 35 | 35 |
| 2. | Idadi ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa na NIDA | 22,194,288 | 23,185,729 | 23,965,371 | 24,897,459 | 27,286,749 | 34,080,610 | 34,100,000 |
| 3. | Idadi ya kampeni za amani zilizofanyika | 50 | 60 | 70 | 90 | 110 | 130 | 150 |
| 4. | Kiwango cha ushiriki wa jamii katika shughuli za usalama (%) | 30 | 35 | 40 | 45 | 50 | 55 | 60 |
| 5. | Idadi ya ajira zilizozalishwa katika miradi ya maendeleo | 23,000 | 25,000 | 27,000 | 28,000 | 30,000 | 31,000 | 33,000 |
| 6. | Mchango katika ajira (%) | 14.7 | 15.2 | 15.8 | 16.3 | 17.2 | 18.1 | 18.8 |
| 7. | Kiwango cha kupungua kwa ajali za barabarani (%) | 45 | 48 | 50 | 52 | 54 | 58 | 60 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mambo ya Ndani*

iv. **Nyumba za Viongozi**

Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa viongozi na watumishi katika muhimili wa Mahakama na Tawala za Mikoa, pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo ujenzi na ukarabati wa ofisi na makazi ya viongozi ikijumuisha nyumba za waheshimiwa majaji. Lengo likiwa ni kuimarisha miundombinu na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi. Hatua hizi zimeimarisha utendaji kazi wa watumishi wa umma na kuboresha mazingira ya kazi katika ngazi mbalimbali za uongozi pamoja na kuboresha huduma kwa wananchi.

v. **Uendelezaji wa Mji wa Serikali Dodoma**

Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ililenga kukamilisha ujenzi wa majengo ya mji wa Serikali – Mtumba, Dodoma. Katika kutekeleza lengo hilo, shughuli zifuatazo zimetekelezwa: ujenzi wa majengo 29 ya ofisi, wizara na taasisi; kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa (Ngome) katika eneo la Kikombo.

Kukamilika kwa majengo haya kutawezesha utoaji wa huduma za Serikali katika eneo moja, kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma, na kupunguza gharama kwa wananchi kupata huduma kwa Serikali.

vi. **Kukabiliana na Maafa**

Serikali imeendelea kuimarisha mfumo wa kukabiliana na maafa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maghala ya kuhifadhi vifaa vya misaada ya kibinadamu wakati wa maafa, na chumba cha kutolea taarifa na maonyo ya mapema kuhusu dharura ya maafa (Situation Room for Multi-Hazard Monitoring and Early Warning) katika Kituo cha Taifa cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura EOCC.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongeza uwezo wa nchi kutabiri taarifa za aina mbalimbali za maafa yakiwemo mafuriko na ukame. Hii imesaidia taifa kuweza kupanga mikakati na namna bora ya kuzuia, kukabiliana na kujidhatiti baada ya majanga. Aidha, utoaji wa taarifa kwa wadau mbalimbali umewezesha kurejesha maisha katika hali yake ya awali baada ya maafa.

Serikali imeendelea kushirikiana na sekta binafsi, mashirika yasiyo ya Serikali na wadau wa maendeleo kama ilivyobainishwa katika Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa mwaka 2022. Ushirikiano huu umesaidia upatikanaji wa rasilimali katika kujiandaa na kukabilina na maafa hivyo kupunguza upotevu wa maisha na uharibifu wa mali katika matukio makubwa ya maafa.




Air Tanzania Cargo













SURA YA NNE

# *Vipaumbele na Malengo Kwa Mwaka 2025/26*

## 4.1 Utangulizi

Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yanaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayolenga kuwezesha Tanzania kuwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya watu ifikapo mwaka 2025. Mpango huu ni wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unahitimisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Hivyo, Mpango umejielekeza katika kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo ya maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Vilevile, Mpango huu ni kiungo baina ya mipango inayokamilika na mipango mipya inayotarajiwa kutekelezwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Hivyo, Mpango huu utaainisha na kutekeleza programu na miradi muhimu ambayo haikukamilika ili kuandaa mazingira shirikishi na endelevu kwa mipango ijayo kwa kufanya uchambuzi wa kina wa wadau (Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi) watakaoshiriki katika kutekeleza mipango husika.

## 4.2 Vigezo vya Kuchagua Vipaumbele vya Mapendekezo ya Mpango

Nguzo muhimu ya maandalizi ya Mpango ni ukuaji wa uchumi pamoja na maeneo matano ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maandalizi ya vipaumbele vya Mpango yamezingatia vigezo vilivyoainishwa kwenye mapendekezo ya mpango ambavyo ni: ukuaji endelevu wa uchumi; kupunguza umaskini; kuzalisha ajira kwa wananchi; kuimarishwa kwa ushindani katika masoko ya kikanda na kimataifa; maendeleo endelevu; pamoja na utawala bora na utawala wa sheria. Vilevile, Mpango huu unalenga kutekeleza na kukamilisha programu na miradi ya maendeleo ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Vipaumbele vinavyopendekezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026 vimezingatia malengo tarajiwa na matokeo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Vipaumbele vya Mpango wa mwaka 2025/26 vitakavyotekelezwa ni kama ifuatavyo:

## 4.3 Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi

Uchumi shindani unahusisha kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kitaifa, kikanda na kimataifa; kuimarisha utulivu na uendelevu wa viashiria vya uchumi jumla; kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara; kuchochea uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia za ndani na za kimataifa; kuimarisha hakimilki za ubunifu na mali; na kuendeleza miundombinu na huduma za reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini, usafiri wa anga, TEHAMA, nishati, bandari na viwanja vya ndege. Aidha, matumizi ya TEHAMA katika nyanja zote za kijamii na kiuchumi yataimarishwa.

### 4.3.1 Sekta ya Ujenzi

Sekta ya ujenzi itaendelea kutekeleza miradi ya kipaumbele inayolenga kuboresha na kuimarisha miundombinu kwa kujenga barabara, madaraja na vivuko ili kuifungua nchi na kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa kwenda kwenye maeneo mbalimbali. Miundombinu imara ni kichocheo kikuu cha ukuaji wa uchumi, ufanyaji biashara na kuongeza ajira hasa

ikizingatiwa kuwa Tanzania ni lango kuu la biashara kwa nchi za Zambia, Malawi, DRC, Burundi, Rwanda na Uganda. Kwa mwaka 2025/26, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi 108 ya ujenzi ambayo ipo katika hatua mbalimbali, kipaumbele kikiwekwa katika miradi 70 ambayo imechaguliwa kutokana na vigezo vilivyoainishwa.

Aidha, sekta binafsi itaendelea kushirikishwa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara, madaraja na majengo inayotekelezwa ambayo itachochea maendeleo ya sekta nyingine kama viwanda, huduma na maendeleo ya miji. Aidha, kupitia uhamasishaji kwa sekta binafsi, Serikali itaendelea kuwawezesha na kuwatumia makandarasi wa ndani katika utekelezaji wa miradi mikubwa. Vilevile, sekta binafsi itaendelea kushirikishwa kwa utaratibu wa ubia (PPP) katika ujenzi wa miundombinu ambayo ni muhimu na kichocheo kwa ukuaji wa uchumi. Ushirikishwaji huu utaongeza ajira na mapato ya Serikali na hivyo kukuza uchumi. Kwa mwaka 2025/26 viashiria na shabaha za sekta ya ujenzi ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali 4.1.** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I.**

**Jedwali Na. 3.24: Viashiria na Shabaha ya Utekelezaji wa Sekta ya Amani, Utulivu na Usalama**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Miundombinu (Nafasi katika mpangilio, kati ya nchi 189 kimataifa) | 50 | 45 |
| 2. | Kiwango cha wastani wa ukuaji (%) | 9.9 | 9.9 |
| 3. | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 16.7 | 16.7 |
| 4. | Mchango wa kampuni za ndani katika soko la ujenzi (%) | 40 | 60 |
| 5. | Idadi ya ajira zilizozalishwa katika miradi ya maendeleo | 30,129 | 30,155 |
| 6. | Nafasi ya barabara katika mpangilio wa kimataifa | 27 | 26 |
| 7. | Kiwango cha kupungua kwa ajali za barabarani (%) | 58 | 60 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Ujenzi*

### 4.3.2 Sekta ya Uchukuzi

Katika mwaka 2025/26, sekta ya uchukuzi itaendelea na utekelezaji wa shughuli zinazochochea ukuaji wa uchumi kwa kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko, kupunguza gharama za kufanya biashara na kuongeza uzalishaji pamoja na ushindani nchini. Kipaumbele kitakuwa katika miradi ya ujenzi wa reli na ukarabati wa miundombinu ya reli, ujenzi na ukarabati wa meli, uboreshaji wa bandari zilizopo, uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya usafiri wa anga. Katika mwaka 2025/26, jumla ya programu

na miradi 22 itatekelezwa ambapo kipaumbele kitakuwa katika miradi 16 ambayo imechaguliwa kutokana na vigezo vilivyoainishwa. Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya uchukuzi kwa mwaka 2025/26 ni kama vilivyoainishwa katika **Jedwali 4.2** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I.**

**Jedwali 4.2: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Uchukuzi**

| Na. | Kiashiria | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Nafasi ya reli katika mpangilio wa kidunia | 58 | 70 |
| 2. | Urefu wa reli ya kati kwa kiwango cha Standard Gauge (SGR) kwa kilometa | 680.38 | 1,219 |
| 3. | Kiasi cha shehena kinachosafirishwa na reli (tani) | 4,788,764 | 5,162,258 |
| 4. | Idadi ya abiria wanaosafirishwa na reli | 1,931,045 | 2,272,682 |
| 5. | Muda wa meli kurejea kituoni kwake (siku) | Wastani 11.2 | 8 |
| 6. | Idadi ya meli zinazoingia bandarini kwa mwezi | 411 | 254 |
| 7. | Muda wa makasha kukaa bandarini (siku) | 7.5 | 5 |
| 8. | Muda wa meli kukaa bandarini (siku) | 3.7 | 2 |
| 9. | Idadi ya bandari kavu | 2 | 3 |
| 10. | Idadi ya meli zinazohudumiwa | 2,471 | 4,000 |
| 11. | Mizigo inayotoka nje kuelekea nchi za jirani (tani milioni) | 34.7 | 18.0 |
| 12. | Mizigo ya kwenda nje toka kwa nchi jirani (tani milioni) | 27.9 | 10.0 |
| 13. | Idadi ya ndege zilizonunuliwa | 16 | 19 |
| 14. | Idadi ya ndege za mizigo zilizonunuliwa | 1 | 1 |
| 15. | Idadi ya ndege za abiria za masafa marefu zilizonunuliwa | 3 | 3 |
| 16. | Idadi ya ndege za abiria za masafa ya kati (kanda) zilizonunuliwa | 6 | 8 |
| 17. | Idadi ya ndege za ATCL zinazofanya kazi | 15 | 19 |
| 18. | Idadi ya wanaanga waliofunzwa | 1,088 | 1,359 |
| 19. | Idadi ya viwanja vya ndege vyenye mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege (AMIS) | 10 | 14 |
| 20. | Idadi ya mitambo ya ulinzi kwenye viwanja vya ndege (X-ray machines) | 101 | 71 |
| 21. | Viwanja vya ndege vyenye uzio kuzunguka kiwanja | 18 | 27 |
| 22. | Idadi ya rada za hali ya hewa zilizonunuliwa | 7 | 7 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Uchukuzi*

### 4.3.3 Sekta ya Nishati

Sekta ya Nishati itaendelea na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo kwa lengo la kuwezesha ongezeko la uzalishaji viwandani, maendeleo ya biashara, upatikanaji wa huduma za kijamii pamoja na shughuli nyingine za kiuchumi. Miradi hiyo ni pamoja na uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme mijini na vijijini; utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati; kuongeza matumizi ya CNG katika vyombo vya moto ikiwemo magari pamoja na usambazaji wa gesi asilia.

Kwa mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kutekeleza miradi 27 ya kipaumbele ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. I.** Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya nishati kwa mwaka 2025/26 ni kama zilivyoainishwa katika **Jedwali 4.3.**

**Jedwali 4.3: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Nishati**

| Na. | Kiashiria | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Uzalishaji wa Umeme (MW) | 4031.71 | 4,915 |
| 2. | Idadi ya Mikoa Iliyounganishwa na Gridi | 24 | 26 |
| 3. | Urefu wa Gridi ya Taifa (km) | 8140.4 | 9,351 |
| 4. | Kupungua kwa Upotevu wa Umeme (%) | 12.3 | 7.9 |
| 5. | Asilimia ya Watu waliofikiwa na Umeme | 78.4 | 85 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Nishati*

### 4.3.4 Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itaendelea na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo zenye lengo la kurahisisha na kupunguza gharama za uendeshaji na ufanyaji biashara na kuwezesha utoaji wa huduma za kijamii. Katika mwaka 2025/26, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi saba (7) ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambayo ipo katika hatua mbalimbali ambapo kipaumbaele kitakuwa katika miradi sita (6).

Viashiria na shabaha za sekta ya mawasiliano kwa mwaka 2025/26 vimeainishwa katika **Jedwali Na. 4.4** na orodha ya miradi itakayo tekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na.I.**

**Jedwali Na. 4.4: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Uwiano wa watumiaji wa intaneti nchini (%) | 74 | 80 |
| 2. | Idadi ya Majengo yenye Anwani za Makazi | 18,186,0000 | 18,250,000 |
| 3. | Idadi ya watu wanaomiliki simu za mkononi (Milioni) | 45.2 | 28.6 |
| 4. | Idadi ya anwani zilizosajiliwa kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi | 13,200,000 | 15,231,392 |
| 5. | Idadi ya huduma zilizosajiliwa kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi | 1,000,000 | 1,100,000 |
| 6. | Idadi ya barua za utambulisho zilizotolewa kupitia Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi | 15,000 | 15,500 |
| 7. | Uwiano wa watu waliofikiwa na mitandao ya simu za mikononi (%) | 94 | 100 |
| 8. | Kaya zenye angalau mwanakaya mmoja anayemilik simu ya mkononi (%) | 87.6 (2023/24) | 87,8 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari*

## 4.4 Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma

### 4.4.1 Sekta ya Kilimo

Sekta ya kilimo itaendelea kutekeleza progamu na miradi ya kipaumbele inayolenga kuchangia kwenye Pato la Taifa, kuongeza ajira hususan kwa vijana na wanawake, kuongeza kipato kwa wakulima, kuongeza malighafi za uzalishaji viwandani na kuongeza mapato ya fedha za kigeni. Kwa kuzingatia umuhimu huo, vipaumbele katika sekta ya kilimo ni pamoja na: kuongeza tija na uzalishaji kwa kufanya utafiti wa mbegu bora; kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa; kutoa ruzuku ya mbolea na viuatilifu; kuimarisha usalama wa chakula na lishe; kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi; kuimarisha maendeleo ya ushirika; na kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika uendelezaji wa sekta ya kilimo. Kwa mwaka 2025/26, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi saba (7) ya kilimo ambayo ipo katika hatua mbalimbali huku kipaumbele kikiwekwa katika miradi sita (6) kama ilivyobainishwa katika **Kiambatisho Na. I. Jedwali Na. 4.5** linaonesha viashiria na shabaha vya sekta ya kilimo kwa mwaka 2025/26.

**Jedwali Na. 4.5: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Kilimo**

| Na. | Kiashiria | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Hekta za umwagiliwa | 727,280.6 | 1,200,000 |
| 2. | Mbegu zilizoidhinishwa na zilizozalishwa | 79,700,6 | 80,000 |
| 3. | Akiba ya taifa ya chakula (tani) | 662,151.271 | 1,140,000 |
| 4. | Kiasi cha mazao ya bustani yaliyozalishwa (tani) | 7,518,560.83 | 9,000,000 |
| 5. | Kiasi cha uzalishaji wa mazao ya biashara ya asili (traditional)(tani). | 1,451,694.11 | 1,583,200 |
| 6. | Idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika | 331 | 338 |
| 7. | Idadi ya vyama vya ushirika vinavotumia mfumo wa soko rasmi | 4,060 | 2,782 |
| 8. | Idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika (milioni) | 8.4 | 14.5 |
| | | | |

***Chanzo:*** *Wizara ya  Kilimo*

### 4.4.2 Sekta ya Mifugo

Mwaka 2025/26, Serikali itaendelea na utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika sekta ya mifugo kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Vipaumbele vitakavyotekelezwa katika sekta ya mifugo ni vile vilivyobainishwa katika Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili - ASDP II (Kiambatisho Na. I).  Katika mwaka 2025/26, sekta itatekeleza shughuli zifuatazo: kuongeza uzalishaji, masoko na thamani ya mazao ya mifugo; kuboresha afya ya mifugo; kuendeleza mazao na miundombinu ya mifugo; kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika sekta ya mifugo; kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya mifugo na kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo. **Jedwali Na. 4.6** linaonesha viashiria na shabaha za sekta ya mifugo kwa mwaka 2025/26.

**Jedwali 4.6: Shabaha na Viashiria  katika Sekta ya Mifugo**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Kiwango cha wastani wa ukuaji (%) | 5.5 | 6.5 |
| 2. | Mchango katika Pato la Taifa (bei za sasa) (%) | 6.2 | 7.0 |
| 3. | Kiwango cha vifo vya mifugo (%) | 16 | 12 |
| 4. | Kiwango cha magonjwa ya mifugo (%) | 2.5 | 3 |
| 5. | Kiwango cha uogeshaji mifugo katika josho (%) | 82 | 85 |
| 6. | Kiwango cha chanjo ya mifugo (%) | 42 | 50 |
| 7. | Wastani wa uzalishaji maziwa, ng'ombe wa asili (Lita) | 0.85 | 4 |
| 8. | Ngozi bora iliyochakatwa (%) | 40 | 50 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 9. | Uzalishaji wa nyama (Tani) | 1,124,449 | 951,700 |
| 10. | Uzalishaji wa maziwa (Lita bilioni) | 4.1 | 4.3 |
| 11. | Asilimia ya maziwa yaliyochakatwa | 2.2 | 14 |
| 12. | Ngozi zilizochakatwa (Tani) | 2,900 | 9,210.6 |
| 13. | Mauzo ya nyama nje ya nchi (Tani) | 14,900 | 7,200 |
| 14. | Usafirishaji wa ngozi (Tani) | 7,200 | 8,000 |
| | | | |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mifugo na Uvuvi*

### 4.4.3 Sekta ya Uvuvi

Katika mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: kusimamia na kuendeleza rasilimali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji; kuongeza uzalishaji, masoko na thamani ya mazao ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji; kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji; kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya uvuvi; na kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika sekta na uvuvi. Katika mwaka 2025/26, sekta ya uvuvi itatekeleza shughuli zifuatazo: kuongeza uzalishaji, masoko na thamani ya mazao ya uvuvi; ujenzi wa miundombinu muhimu ya uvuvi ya masoko ya samaki, mialo, vituo vya ukuzaji viumbe maji, mashamba darasa ya ukuzaji viumbe maji; vituo vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi; kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika sekta ya uvuvi; na kuendelea na ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa Masoko. Kwa mwaka 2025/26, Sekta ya uvuvi itatakeleza miradi minne (4) ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kipaumbele kitakuwa katika miradi mitatu (3) kulingana na vigezo vilivyoainishwa **(Kiambatisho Na. I)**. **Jedwali Na. 4.7** linaonesha shabaha na viashiria vya sekta ya mifugo kwa mwaka 2025/26.

**Jedwali 4.7: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Uvuvi**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Kiwango cha wastani wa ukuaji (%) | 4.5 | 8.4 |
| 2. | Asilimia katika Pato la Taifa (Bei za sasa) | 1.9 | 1.9 |
| 3. | Asilimia katika mapato yatokanayo na mauzo nje | 3 | 4.5 |
| 4. | Ulaji kwa kila mtu | 8.5 | 10.5 |
| 5. | Mchango katika ulaji wa protini ya wanyama kitaifa | 33 | 35 |
| 6. | Uzalishaji wa samaki (tani) | 575,000 | 600,000 |
| 7. | Idadi ya viwanda vya kusindika samaki | 21 | 17 |
| 8. | Idadi ya Vituo vya Ukuzaji Viumbe Maji (Aquaculture Development Centres - ADC) | 12 | 12 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 9. | Uzalishaji wa chakula cha samaki (tani) | 5,000 | 8,000 |
| 10. | Idadi ya Maafisa Ugani wa Uvuvi | 700 | 1,850 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mifugo na Uvuvi*

### 4.4.4 Sekta ya Uzalishaji Viwandani

Sekta ya uzalishaji viwandani ni sekta wezeshi katika kufikia malengo ya uchumi shindani wa viwanda kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Uwepo wa viwanda vikubwa na vya kimkakati vyenye kuzalisha bidhaa zinazohitajika kwenye soko la ndani na nje utasaidia kuongeza thamani kwa bidhaa, kuongeza mauzo nje, kuchochea shughuli za biashara na kuongeza upatikanaji wa ajira.

Kwa mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kutekeleza miradi 21 ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji (Kiambatisho Na. II) ambapo kipaumbele kitakuwa katika programu/miradi nane (8) kulingana na vigezo vilivyoainishwa **(Kiambatisho Na. I)**. Shabaha na viashiria vya sekta ya uzalishaji viwandani ni kama zilivyoainishwa katika **Jedwali 4.8.**

**Jedwali 4.8: Shabaha ya Viashiria katika Sekta ya Uzalishaji Viwandani**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 7.3 | 8.5 |
| 2. | Kiwango cha ukuaji halisi wa Pato la Taifa (%) | 4.8 | 6.8 |
| 3. | Mchango katika ajira zote (%) | 12.8 (2024) | 12.8 (2025) |
| 4. | Mchango katika mapato ya mauzo nje (%) | 19 | 19 |
| 5. | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya kati katika mauzo nje (%) | 36 | 39 |
| 6. | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya juu katika mauzo nje (%) | 42 | 10 |
| 7. | Mchango katika mauzo yote nje (%) | 39 | 24 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Viwanda na Biashara*

### 4.4.5 Sekta ya Madini

Sekta ya madini nchini ni muhimu katika kuongeza mchango kwenye Pato la Taifa, kutoa ajira, kuchochea uwekezaji, kukuza sekta nyingine ikiwemo viwanda na kusaidia maendeleo ya jamii. Katika mwaka 2025/26, Serikali itaendelea: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli; kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye ukuaji wa Pato la Taifa; kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati; kuhamasisha uwekezaji na uongezaji thamani madini; kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za madini za kina; pamoja na kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo wakiwemo vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Miradi miwili (2) ya kipaumbele itatekelezwa kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho I.** Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya uchukuzi ni kama zilivyoainishwa katika **Jedwali 4.9.**

**Jedwali 4.9: Shabaha ya Viashiria katika Sekta ya Madini**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Wastani wa ukuaji (%) | 8.6 (Robo ya Tatu, 2024) | 11.6 |
| 2. | Mchango kwenye Pato la Taifa (%) | 11.4 (Robo ya Tatu, 2024) | 11.2 |
| 3. | Jumla ya mapato ya fedha za nje (dola za Marekani milioni) | 3,551.4 | 3,760.4 |
| 4. | Mauzo ghafi nje (%) | 9 | 5 |
| 5. | Bidhaa zilizoongezwa thamani (%) | 93 | 95 |
| 6. | Mchango katika mapato yote ya fedha za nje yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje (%) | 56.2 | 51.7 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Madini*

### 4.4.6 Sekta ya Utalii

Katika mwaka 2025/26, Serikali itaendelea na utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali katika sekta ya maliasili na utalii kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maeneo ya vipaumbele katika sekta ni pamoja na: kutangaza utalii ndani na nje ya nchi; kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati; kuboresha miundombinu ya utalii na uhifadhi; kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika usimamizi wa uhifadhi; na kuimarisha usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato. Katika mwaka 2025/26, jumla ya miradi 16 ambayo ipo katika hatua mbalimbali itatekelezwa ambapo kipaumbele kitakuwa katika miradi 10. Miradi hii ya vipaumbele imechaguliwa kutokana na vigezo vilivyoainishwa. Orodha ya miradi inayoendelea kutekelezwa katika sekta hii imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I**. Aidha, viashiria na shabaha za sekta ya utalii kwa mwaka 2025/26 ni kama vilivyoainishwa katika **jedwali Na. 4.10.**

**Jedwali 4.10: Shabaha ya Viashiria katika Sekta ya Utalii**

| Na. | Kiashiria | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa (bei za sasa) (%) | 17.5 | 18.9 |
| 2. | Idadi ya watalii kutoka nje ya nchi | 2,141,895 | 5,000,000 |
| 3. | Idadi ya watalii ndani ya nchi | 2,102,371 | |
| 4. | Wastani wa idadi ya siku za kulala mtalii. | 10 | 14 |
| 5. | Wastani wa matumizi ya mtalii kwa siku (USD) | 260 | 276 |
| 6. | Mchango katika mapato ya fedha za kigeni (%) | 26 | 27 |
| 7. | Mapato yatokanayo na watalii (dola za Marekani bilioni) | 4.1 | 6.0 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maliasili na Utalii*

### 4.4.7 Sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo

Utamaduni, sanaa na michezo ni moja ya sekta ya huduma ambayo inakua kwa kasi nchini na inavutia nguvu kazi ya vijana. Hivyo, uimarishaji wa sekta hii ni muhimu kwa kuwa itasaidia kutoa fursa za ajira, kuvutia watalii na kuchangia katika Pato la Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu huo, katika mwaka 2025/26, vipaumbele vya sekta hii ni pamoja na: kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya msingi ya habari, michezo na kazi za sanaa na ubunifu; kuimarisha Bodi ya Ithibati ya Wanahabari; kutambua, kukusanya, kuendeleza, kulinda na kuhifadhi kumbukumbu na taarifa za urithi wa ukombozi wa bara la Afrika unaoshikika na usioshikika ndani na nje ya nchi; kuendelea na maandalizi ya mashindano ya AfCON; kuratibu utoaji wa mikopo na mafunzo kwa wadau wa sekta ya utamaduni na sanaa; na kuimarisha, kukuza na kubidhaisha Kiswahili kitaifa, kikanda na kimataifa.

Katika kuhakikisha kuwa vipaumbele vilivyoainishwa vinafikiwa kikamilifu, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine katika mwaka 2025/26 itaendelea na utekelezaji wa miradi 18 ambayo ipo katika hatua mbalimbali huku kipaumbele kitakuwa katika miradi 13 **(Kiambatisho Na. I)**. Miradi hii ya kipaumbele imechaguliwa kutokana na vigezo vilivyoainishwa. Kwa mwaka 2025/26 viashiria na shabaha za sekta ya sanaa, utamaduni na michezo ni kama zilivyoainishwa katika **Jedwali 4.11.**

**Jedwali Na. 4.11 Shabaha ya Viashiria katika Sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya miundombinu ya michezo na iliyoboreshwa nchini kote | 174 | 72 |
| 2. | Idadi ya miundombinu iliyojengwa/kukarabatiwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamaoyo (TaSUBa). | 58 | 40 |
| 3. | Idadi ya filamu na muziki zilizoidhinishwa, kusambazwa na kutumika | 4,342 | 25,735 |
| 4. | Idadi ya wasanii waliosajiliwa katika tasnia ya ubunifu | 7310 | 8,666 |
| 5. | Idadi ya wataalamu katika tasnia ya ubunifu waliopata mafunzo | 11,500 | 4,297 |
| 6. | Idadi ya michezo na mashindano ya kimataifa yaliyoandaliwa na Tanzania kushiriki | 110 | 350 |
| 7. | Idadi ya vibali vilivyotolewa kwa vyama vya michezo na wanamichezo binafsi | 110 | 400 |
| 8. | Idadi ya wanariadha wanaocheza nje ya nchi | 62 | 150 |
| 9. | Idadi ya wageni wanaoendesha shughuli za kuzalisha filamu nchini Tanzania. | 70 | 1,059 |
| 10. | Idadi ya wasanii/wataalamu katika tasnia ya ubunifu/ makundi yanayofanya maonesho yao nje ya nchi | 61 | 1,755 |
| 11. | Idadi ya wasanii wa nje/wataalamu katika tasnia ya ubunifu wanaofanya maonesho yao nchini Tanzania | 2 | 2,312 |
| 12. | Idadi ya wataalamu wa Kiswahili wanaofanya kazi nje ya Tanzania | 384 | 656 |
| 13. | Idadi ya machapisho ya Kiswahili yaliyouzwa nje ya nchi | 502 | 700 |
| 14. | Idadi ya tuzo za kimataifa zilizoandaliwa na kutolewa kwenye utamaduni, sanaa na tasnia ya ubunifu | 68 | 130 |
| 15. | Idadi ya vikundi vya utamaduni na sanaa kutoka nje ya nchi vilivyoshiriki katika matamasha ya kimataifa yanayoandaliwa kila mwaka na TaSUBa. | 11 | 20 |
| 16. | Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya | 503 | 1,300 |
| 17. | Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa TaSUBa | 947 | 1,200 |
| 18. | Idadi ya wilaya zinazofikiwa na matangazo ya TBC (TBCFM na TBCT aifa) | 138 | 161 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo*

## 4.5 Kukuza Uwekezaji na Biashara

### 4.5.1 Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Biashara

Katika kukuza uwekezaji na biashara, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kielelezo na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi. Kwa mwaka 2025/26, vipaumbele ni kuboresha vivutio vya uwekezaji na mazingira ya biashara, kujenga na kuimarisha mifumo ya usimamizi katika Taasisi na Mashirika ya Umma, na kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa, kufanya utafiti wa urahisi wa ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ili kuchochea ushindani zaidi katika biashara na uwekezaji.

Kutekelezwa kwa vipaumbele hivyo kutasaidia kuongeza mchango katika pato la taifa kwa kuvutia wawekezaji zaidi, kuongeza ajira zitokanazo na uwekezaji na biashara, kuchochea ubunifu na teknolojia, kuongeza fedha za kigeni na kuimarisha miundombinu katika sekta mbalimbali kama vile barabara, umeme, maji, na mawasiliano. Orodha ya miradi itakayotekelezwa kwa mwaka 2025/26 kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I.** Aidha, shabaha na viashiria vya kukuza uwekezaji na biashara ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali 4.12**

**Jedwali 4.12: Shabaha na Viashiria katika Kukuza Uwekezaji na Biashara**

| Na. | Kiashiria | Shabaha (Maoteo) | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na TIC na EPZA | 640 | 600 |
| 2. | Thamani ya miradi ya uwekezaji (dola za Marekani) | 8,813 | 8,500 |
| 3. | Idadi ya ajira kutokana na miradi ya uwekezaji | 280,000 | 250,000 |
| 4. | Idadi ya kongano za uwekezaji | 21 | 5 |
| 5. | Idadi ya miongozo ya uwekezaji ya mikoa | 26 | 26 |
| 6. | Idadi ya Ofisi za Utoaji Huduma Mahala Pamoja | 15 | 18 |
| 7. | Kiasi cha ardhi ya uwekezaji iliyotengwa (ekari) | 391,030.94 | 528,917 |
| 8. | Idadi ya Makongamano ya Uwekezaji Kimataifa | 180 | 150 |
| 9. | Idadi ya maboresho ya sheria na kanuni za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | 80 | 88 |
| 10. | Idadi ya maboresho ya kufuta au kupunguza tozo, ada na ushuru katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | 383 | 388 |

***Chanzo:*** *Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji*

### 4.5.2 Uwekezaji wa Sekta Binafsi

Katika mwaka wa fedha 2025/26 Serikali itaendelea kuhamasisha mamlaka za umma kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye viashiria vya biashara. Utekelezaji utahusisha mikakati mbalimbali ikiwemo:

i. Kuendelea na mapitio ya mipango ya maendeleo na bajeti ya Serikali ya kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2024/25 ili kubaini miradi ambayo inaweza kutekelezwa kwa ubia na sekta binafsi na kushauri ipasavyo utekelezaji wa sheria na kanuni za ubia;
ii. Kuendeleza mashirikiano na wadau wa maendeleo ili kujengea uwezo watumishi katika uibuaji, uandaaji na uthamini wa miradi ya ubia;
iii. Kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya PPP iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama vile miradi ya: usambazaji wa gesi asilia; mabasi yaendayo haraka (BRT); Barabara ya Kulipia (Morogoro – Dodoma); daraja la Kigamboni; barabara ya mzunguko wa ndani na nje katika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam; *Commuter Railways;* na miradi ya usambazaji wa umeme.

Aidha, Serikali itaendelea kufanya tathmini ya mchango wa Sekta binafsi katika kukuza uchumi; kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Sekta Binafsi pamoja na Mkakati wake wa utekelezaji, Sera ya Taifa ya Ushiriki wa Wazawa *(Local Content Policy)*; kuimarisha majadiliano na mashirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi kwa ngazi ya Taifa, Wizara, Mikoa na Wilaya; kuwajengea uwezo wajumbe wa mabaraza ya biashara katika ngazi za mikoa na wilaya pamoja na kuainisha vyama vya sekta binafsi vilivyopo nchini.

### 4.5.3 Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi

Katika mwaka 2025/26 Serikali itaendelea kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa diplomasia ya kisiasa na kiuchumi ambao unalenga; kujenga na kuboresha miundombinu ya ofisi za Tanzania nje ya nchi; na kupanua na kuimarisha ushirikiano na ushiriki wa Tanzania katika shughuli za kikanda na kimataifa. Serikali itaendelea kutekeleza miradi mitatu (3) huku kipaumbele kikiwa katika mradi wa ujenzi, ukarabati na ununuzi wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi balozini ili kuimarisha mahusiano na nchi za nje na kukuza mahusiano ya kimataifa na diplomasia ya uchumi. Kwa mwaka 2025/26 shabaha za sekta ya mahusiano ya kimataifa na diplomasia ya uchumi ni kama zilivyoainishwa katika **Jedwali 4.13** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I.**

**Jedwali Na. 4.13 Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya mikutano kati ya Tanzania na nchi moja moja, ya kikanda na kimataifa iliyoshiriki | 110 | 250 |
| 2. | Idadi ya Watanzania walioshiriki katika ulinzi wa amani nje ya nchi | 1500 | 3,500 |
| 3. | Idadi ya ofisi na nyumba za kuishi zilizokarabatiwa | 4 | 14 |
| 4. | Idadi ya Hati za Makubaliano ya Pamoja zilizosainiwa kati ya Tanzania na nchi nyingine | 84 | 80 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki*

## 4.6 Kuchochea Maendeleo ya Watu

Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi inayolenga kuboresha maisha ya watu ikiwemo: elimu na mafunzo; afya na ustawi wa kijamii; hifadhi ya jamii; huduma za maji na usafi wa mazingira; mipango miji; nyumba na maendeleo ya makazi; na athari dhidi ya tabianchi. Maendeleo ya watu ni azma kuu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26, katika kufanikisha hilo Mpango utaweka kipaumbele katika kuboresha huduma za afya, elimu na ujuzi, maji, lishe, makazi, mipango miji; hifadhi ya jamii pamoja na kuchochea ushiriki wa sekta binafsi katika kuimarisha ustawi wa jamii.

### 4.6.1 Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi

Serikali itaendelea kuhakikisha elimu na mafunzo nchini inatolewa kwa kuzingatia vipaumbele na mipango ili kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu. Ili kukuza viwango vya elimu na kuwezesha wahitimu kuwa na ujuzi unaotakiwa katika soko la ajira, Serikali itaendelea kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ikiwemo: Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la mwaka 2023 pamoja mitaala ambayo imeweka msisitizo wa kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali; kuwezesha ongezeko la fursa na kuimarisha ubora wa elimu kwa ngazi zote; kuwezesha upatikanaji wa vifaa na mitambo ya mafunzo; kujenga uwezo kwa walimu, wahadhiri na watumishi wa sekta ya elimu; kufungamanisha masomo ya ujuzi katika ngazi zote za elimu; kuwezesha mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa waajiriwa; kutoa mafunzo ya ujuzi kwa vijana/waliohitimu vyuo (mafunzo ya utarajali na uanagenzi); kutambua elimu na ujuzi ili kuchochea upatikanaji wa ajira; na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu.

Katika kuhakikisha ujuzi unaopatikana unaendana na wakati, Serikali itahamasisha matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za elimu. Vilevile, Serikali itaimarisha uwezo wa nchi katika tafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuwezesha nchi kuendana na maendeleo ya sayansi na

teknolojia ulimwenguni pamoja na kuchochea ubunifu katika utekelezaji wa afua na ajenda za kimkakati kwa maendeleo ya uchumi wa viwanda.Aidha,Serikali itahakikisha sekta binafsi zinaendelea kushirikishwa katika utekelezaji wa afua mbalimbali ikiwemo miradi ya uendelezaji wa elimu na mafunzo kama vile ujenzi na ukarabati wa shule pamoja na utoaji wa vifaa vya elimu ili kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo pamoja na kuimarisha ubora. Katika kuhakikisha hilo, Serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki kwa lengo la kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya elimu ambapo uwekezaji huo unatarajiwa kuchochea maendeleo ya watu na nchi kwa ujumla. Kwa mwaka 2025/26, shabaha zitakazotekelezwa na sekta ya elimu ni kama zilivyoainishwa katika **Jedwali 4.14** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I.**

**Jedwali 4.14: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | **Elimu** | | |
| **1.1** | **Elimu ya Awali** | | |
| 1.1.1 | Kiwango cha uandikishaji rika lengwa (% ya wanaostahili) | 89.5 | 100 |
| 1.1.2 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa | 1:151 | 80 |
| **1.2** | **Elimu ya Msingi** | | |
| 1.2.1 | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) | 84.2 | 100 |
| 1.2.2 | Kiwango cha uandikishaji wa rika lengwa | 79.6 | 100 |
| 1.2.3 | Asilimia ya kundirika la wanafunzi waliofaulu mtihani wa elimu ya msingi | NA | 100 |
| 1.2.4 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi wa elimu ya msingi kwa mwalimu | 1:56 | 1:50 |
| 1.2.5 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa kitabu | 1:2 | 1:1 |
| 1.2.6 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa | 1:63 | 1:60 |
| 1.2.8 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi wa kiume kwa tundu la choo | 1:43 | 1:25 |
| 1.2.7 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi wa kike kwa tundu la choo | 1:47 | 1:20 |
| 1.2.8 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa dawati | 1:4 | 1:2 |
| 1.2.9 | Asilimia ya shule za msingi zenye umeme | 68.0 | 60.0 |
| **1.3** | **Elimu ya Sekondari ya Chini (I-IV)** | | |
| 1.3.1 | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) | 51.7 | 48 |
| 1.3.2 | Uwiano wa uandikishaji wa watoto wenye umri wa rika lengwa Ikilinganishwa na idadi ya watoto wote wenye umri wa kwenda shule | 40.6 | 42 |
| 1.3.3 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi wa elimu ya sekondari kwa mwalimu | 1:26 | 1:20 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1.3.4 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi wa elimu ya sekondari kwa darasa | 1:34 | 1:40 |
| 1.3.5 | Uwiano wa idadi ya wanafunzi wa sekondari kwa tundu la choo | 1:28 | 1:20 |
| 1.3.6 | Asilimia ya shule za sekondari zenye umeme | 81.4 | 85 |
| 1.3.7 | Asilimia ya kundirika la wanafunzi waliofaulu mtihani wa elimu ya sekondari ya chini | NA | 90.0 |
| **1.4** | **Elimu ya Sekondari ya Juu (V – VI)** | | |
| 1.4.1 | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya Wanaostahili) | 9.1 | 10 |
| 1.4.2 | Kiwango cha uandikishaji rika lengwa (% ya wanaostahili) | 5.2 | 8 |
| 1.4.3 | Uandikishaji halisi wa wanafunzi wa kiume (%) | 5.0 | 4 |
| 1.4.4 | Uandikishaji halisi wa wanafunzi wa kike (%) | 5.4 | 4 |
| 1.4.5 | Asilimia ya wanafunzi wanaofaulu mtihani wa kidato cha VI | NA | 100 |
| **1.5** | **Elimu ya Juu** | | |
| 1.5.1 | Idadi ya wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu | 250,567 | 180,000 |
| 1.5.2 | Idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu | N/A | 70,081 |
| 1.5.3 | Idadi ya wahitimu kwa wanafunzi wa kiume | | 39,690 |
| 1.5.4 | Idadi ya wahitimu kwa wanafunzi wa kike | | 44,700 |
| **1.6** | **Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi** | | |
| 1.6.1 | Kiwango cha udahili jumla (%) | NA | 6.0 |
| 1.6.2 | Idadi ya wanafunzi wanaohitimu kwa mwaka | NA | 120,000 |
| 1.6.3 | Asilimia ya wanafunzi wanaohitimu masomo ya sayansi na uhandisi kwa mwaka | NA | 40 |
| 1.6.4 | Asilimia ya wanafunzi wa kike wanaohitimu kwa mwaka | | 43 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia*

### 4.6.2 Sekta ya Afya

Katika mwaka 2025/26, Serikali itaendelea na utekelezaji wa programu na miradi 14 ambapo miradi 11 ni ya kipaumbele. Mpango utajielekeza katika kuimarisha mifumo ya usimamizi, upatikanaji wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; kukamilisha miradi ya ujenzi ya miundombinu ya huduma za mama na mtoto, huduma za dharura pamoja na huduma za uangalizi; kuajiri na kuendeleza wataalam wa sekta ya afya katika ngazi mbalimbali za utoaji wa huduma za afya nchini.

Aidha, Sekta binafsi itaendelea kushiriki katika kutoa huduma za afya, kuzalisha wataalamu wa afya pamoja na kuzalisha bidhaa za afya. Ushiriki huo utachochea

ukuaji wa sekta ya afya, ajira, ustawi na maendeleo ya watu. Kwa mwaka 2025/26 shabaha za sekta ya afya ni kama zilivyoainishwa katika **Jedwali 4.15** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I.**

**Jedwali 4.15: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Afya**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya vifo vya watoto wachanga kwa kila vizazi hai 1000 | 24 (2022 TDHS-MIS | 15 |
| 2. | Idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa kila vizazi hai 1000 | 43 (2022 TDHS-MIS) | 40 |
| 3. | Uzazi uliohudumiwa na mfanyakazi wa afya mwenye ujuzi | 94.7 (2023–AHSP) | 85 |
| 4. | Wastani wa umri wa kuishi (miaka) | 68 (Sensa-2022) | 68 |
| 5. | Kiwango cha maambukizi ya VVU kitaifa (%) | 4.4(THIS 2022/2023) | 3.1 |
| 6. | Matumizi ya Serikali katika huduma za afya (%) | 10.3(2023-AHSP) | 12.2 |
| 7. | Idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi kwa kila vizazi hai 100,000 | 104 (2022 TDHS-MIS) | 180 |
| 8. | Matumizi ya Serikali katika afya (% ya matumizi yote ya Serikali) | 10.3 (2023-AHSP) | 12.2 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Afya*

### 4.6.3 Sekta ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira

Katika mwaka 2025/26, Serikali itahakikisha upatikanaji wa maji safi na salama na huduma za usafi wa mazingira ambapo kipaumbele kitakuwa katika kujenga na kuboresha miundombinu ya maji, kuongeza upatikanaji wa huduma za usafi wa mazingira na kuendesha kampeni za kuhamasisha matumizi bora ya maji na usafi. Hivyo, Serikali itaendelea na utekelezaji wa programu 13 yenye jumla ya miradi midogo 1,069 ambayo inaendelea na utekelezaji na ipo katika hatua mbalimbali. Kipaumbele kitawekwa kwenye miradi mitano (5).

Orodha ya miradi inayoendelea kutekelezwa katika sekta ya maji imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I.** Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kusimamia na kutekeleza ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira ikiwa ni hatua muhimu ya kuifanya sekta ya maji kujiendesha kibiashara. Kwa mwaka 2025/26 shabaha za sekta ya maji ni kama zilivyoainishwa katika **Jedwali 4.16.**

**Jedwali 4.16: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba au maji yalivyolindwa kama chanzo kikuu | 83 | 85 |
| 2. | Uwiano wa kaya za vijijini zenye miundombinu iliyoboreshwa ya usafi wa mazingira | 78.5 | 60 |
| 3. | Asilimia ya watu katika makao makuu ya mikoa wanaopata maji ya bomba au maji yaliyolindwa | 91.6 | 95 |
| 4. | Asilimia ya kaya katika makao makuu ya mikoa iliyounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka | 13 | 30 |
| 5. | Asilimia ya upotevu wa maji (NRW) katika makao makuu ya mikoa | 33.4 | 20 |
| 6. | Asilimia ya watu katika makao makuu ya wilaya na miji midogo wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu | 74.5 | 85 |
| 7. | Asilimia ya watu katika jiji la Dar es Salaam wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji salama kama chanzo chao kikuu | 93 | 95 |
| 8. | Asilimia ya kaya katika jiji la Dar es Salaam waliounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka | 13 | 30 |
| 9. | Kiwango cha upotevu wa maji (NRW) katika jiji la Dar es Salaam | 43.2 | 20 |
| 10. | Idadi ya vyanzo vya maji vilivyotengwa na kutangazwa kwa ajili ya ulinzi na uhifadhi | 68 | 80 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maji*

## 4.6.4 Sekta ya Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Serikali kupitia mpango wa mwaka 2025/26 itahakikisha uwepo wa nyumba na makazi bora, miundombinu wezeshi na upatikanaji wa huduma za jamii kulingana na mahitaji ya watu katika eneo husika. Maeneo ya kipaumbele ni pamoja na: kuimarisha mifumo ya uandaaji wa mipango kabambe ya matumizi ya ardhi; kuendeleza miji na maeneo tengefu; kuhamasisha uwekezaji katika ardhi na hatimiliki za ardhi; kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika upimaji na utunzaji wa taarifa za ardhi; na kuendeleza nyumba na makazi bora. Kwa mwaka 2025/26, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi mitano (5) ya mipango miji, nyumba, na maendeleo ya makazi ambapo kipaumbele kitakuwa katika miradi minne (4). Miradi hii ya kipaumbele imechaguliwa kutokana na vigezo vilivyoainishwa. Orodha ya miradi inayoendelea kutekelezwa katika eneo la mipango miji, nyumba, na maendeleo ya makazi imeainishwa katika **Kiambatisho I.**

Aidha, sekta binafsi itaendelea kushirikishwa katika utekelezaji wa miradi katika eneo la mipango miji, nyumba, na maendeleo ya makazi inayotekelezwa na Serikali kupitia uhamasishaji wa sekta binafsi kujihusisha na utekelezaji wa miradi binafsi katika eneo la mipango miji, nyumba, na maendeleo ya makazi. Ushirikishwaji huu utachochea uwekezaji katika ardhi na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Kwa mwaka 2025/26 shabaha za sekta ya mipango miji, nyumba, na maendeleo ya makazi ni kama zilivyoainishwa katika **Jedwali 4.17.**

**Jedwali 4.17: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya mali zilizorasimishwa katika makazi yasiyo rasmi | 3,102,715 | 3,402,715 |
| 2. | Asilimia ya eneo la ardhi yenye makazi yasiyo rasmi | 67.3 | 60 |
| 3. | Eneo la ardhi lilitengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma (ekari) | 874,937 | 1,452,415 |
| 4. | Idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohuishwa | 28 | 54 |
| 5. | Idadi ya viwanja vilivyotengwa | 3,097,455 | 4,051,716 |
| 6. | Idadi ya mashamba yaliyotengwa | | |
| 7. | Idadi ya ramani za msingi zilizohuishwa kwa eneo | 88 | 26 |
| 8. | Uwiano wa vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi (%) | 34.5 | 52.7 |
| 9. | Idadi ya mabaraza ya ardhi yanayofanya kazi | 115 | 139 |
| 10. | Asilimia ya ardhi iliyopimwa | 26 | 37 |
| 11. | Idadi ya leseni za makazi zilizotolewa katika makazi yasiyo rasmi | 23,862 | 20,000 |
| 12. | Idadi ya ramani za msingi zilizohuishwa kwa eneo | 88 | 26 |
| 13. | Idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohuishwa | 28 | 54 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*

### 4.6.5 Sekta ya Hifadhi ya Jamii

Katika mwaka 2025/26, Serikali kupitia mifuko ya hifadhi ya jamii itaendelea kutekeleza miradi 10 ikiwemo miradi 5 ya kipaumbele. Miradi hii ni pamoja na majengo ya vitega uchumi na viwanda vya uzalishaji mali.

Aidha, Serikali itaendelea kuwashirikisha sekta binafsi katika kuhamasisha uwekezaji katika utoaji wa huduma za hifadhi ya jamii; kuongeza wigo wa huduma za hifadhi ya jamii kwa sekta binafsi; na kuimarisha ushiriki wa jamii katika mipango ya hifadhi ya jamii  na maendeleo ya sekta binafsi. Ushiriki huu utaongeza ulinzi wa jamii dhidi ya umaskini na ajira zisizo na staha.

### 4.6.6 Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

Katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano, sekta ya ustawi na maendeleo ya jamii inajielekeza kuweka mikakati kuhusu maendeleo ya watu. Katika mwaka 2025/26 sekta ya maendeleo ya jamii inatarajia kutekeleza jumla ya miradi tisa (9) ukiwemo mradi wa TASAF ambapo kipaumbele kitakuwa katika miradi nane (8). Utekelezaji wa miradi hii unalenga: kupunguza uwepo wa mila na desturi kandamizi na zenye madhara; kuimarisha mazingira wezeshi ya uendeshaji wa Mashirikia Yasiyo ya Kiserikali nchini; kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia mikopo yenye riba nafuu na majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi; kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai katika kuimarisha huduma za haki jinai kwa watoto na kuendelea kuwajengea uwezo watoa huduma walio kwenye mfumo wa haki jinai;  kuimarisha matunzo, ulinzi na usalama wa mtoto; kupunguza matumizi yasiyo sahihi ya teknolojia ikiwemo mitandao yanayosababisha ongezeko la mmomonyoko wa maadili katika jamii. Kwa mwaka 2025/26 shabaha za sekta ya ustawi na maendeleo ya jamii ni kama zilivyoainishwa katika **Jedwali 4.18.**

**Jedwali 4.18: Shabaha na Viashiria katika sekta ya  Ustawi na Maendeleo ya Jamii**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya vituo vya malezi ya watoto vilivyosajiliwa | 4,800 | 7,500 |
| 2. | Idadi ya wazee wasiojiweza wanaopata huduma za bima ya afya bure | 432,642 | 574,321 |
| 3. | Idadi ya watoto wanaolelewa baada ya mapatano | 48,051 | 50,000 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum*

### 4.6.7 Sekta ya Utawala Bora na Utawala wa Sheria

Uongozi bora na utawala wa sheria ni msingi wa maendeleo na uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo katika kufanya maamuzi. Hivyo, Mpango huu utajielekeza katika kuimarisha misingi ya kidemokrasia; kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa; kuboresha mifumo ya utawala na uratibu wa shughuli za Serikali; kuimarisha motisha ya utendaji na uwajibikaji; na kuboresha michakato ya utoaji wa huduma kwa sekta ya umma na binafsi.

#### i. Utumishi na Utawala Bora

Kwa mwaka 2025/26 Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi 10 ya eneo la utawala bora ambayo ipo katika hatua mbalimbali ikijumuisha kuboresha miundombinu ya Bunge. Kipaumbele katika eneo hili itakuwa akatika miradi mitano (5) kama ilivyoainishwa katika Kiambatisho I. Kwa mwaka 2025/26 shabaha za eneo la uongozi bora na utawala wa sheria ni kama zilivyoainishwa katika **Jedwali 4.19.**

**Jedwali 4.19: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Utumishi na Utawala Bora**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya watumishi waliopatiwa mafunzo ya maadili ya utendaji katika utumishi wa umma | 6,000 | 15,000 |
| 2. | Kupungua kwa malalamiko yatokanayo na utawala bora na masuala ya utawala bora | 165 | 121 |
| 3. | Idadi ya taasisi zilizofundishwa matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho (ili kuongeza uwajibikaji na mapambano dhidi ya rushwa katika utumishi wa umma na nchi kwa ujumla) | 340 | 100 |

***Chanzo:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma*

#### ii. Utawala wa Sheria

Katika mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kuboresha mifumo ya utoaji na upatikanaji wa haki ambayo ni muhimu katika kuimarisha usawa na ustawi wa jamii. Vipaumbele vitakavyotekelezwa ni pamoja na: kuboresha mifumo na miundombinu ya mahakama pamoja na majengo jumuishi ya utoaji wa haki; kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji na upatikanaji wa haki; kuimarisha taratibu na miongozo ya utoaji wa msaada wa kisheria nchini ikiwemo kuimarisha madawati ya msaada wa kisheria yaliyoanzishwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuendeleza kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia; Kuimarisha mfumo wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu; na kuimarisha mifumo ya utunzaji wa taarifa na kumbukumbu za mahakama.

Katika kutekeleza vipaumbele hivyo, Serikali itatekeleza jumla ya miradi 15 ambapo kipaumbele kitakuwa katika miradi tisa (9) ambayo ipo katika hatua mbalimbali. Orodha ya miradi itakayotekelezwa imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I. Jedwali 4.20** linaonesha shabaha na viashiria katika mifumo ya utoaji haki kwa mwaka 2025/26.

**Jedwali 4.20: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Mifumo ya Utoaji Haki**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Asilimia ya raia wanaoishi katika mikoa yenye Mahakama Kuu inayofanya kazi | 83 | 100 |
| 2. | Asilimia ya kesi zilizohudumiwa na watoa msaada wa huduma za kisheria | 15 | 20 |
| 3. | Idadi ya IJCs zilizojengwa na zinazofanya kazi katika maeneo yaliyo chaguliwa | 0 | 28 |
| 4. | Idadi ya majengo ya mahakama ya wilaya yaliyojengwa | 7 | 139 |
| 5. | Idadi ya majengo ya mahakama ya mwanzo yaliyojengwa | 72 | 791 |
| 6. | Idadi ya ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilizojengwa mikoani | 3 | 10 |
| 7. | Idadi ya ofisi za NPS zilizojengwa mikoani | 4 | 7 |
| 8. | Idadi ya ofisi za NPS zilizojengwa wilayani | 3 | 11 |
| 9. | Idadi ya wilaya zenye watoa msaada wa huduma za kisheria waliosajiliwa | 116 | 138 |
| 10. | Wastani wa idadi ya siku tangu kufunguliwa kwa kesi na kutolewa hukumu | 78 | 350 |
| 11. | Asilimia ya watu walioridhishwa na huduma za mahakama | 88 | 80 |
| 12. | Wastani wa idadi ya siku tangu kufunguliwa kwa kesi na kutolewa hukumu katika Mahakama ya Biashara | 231 | 350 |
| 13. | Asilimia ya mlundikano wa kesi, kwa jumla ya kesi zote zinazosubiri maamuzi | 4 | 2 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Katiba na Sheria*

### iii. Amani, Utulivu na Usalama

Katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi 112 ya usalama ambapo kipaumbele kitakuwa katika miradi 76, kwa lengo la kuimarisha usalama wa raia na mali zao nchini; kuhamasisha amani na utulivu katika jamii; kuimarisha usimamizi wa taratibu za utambuzi na usajili wa raia; na kuboresha mifumo ya vyombo vya usalama.

Shabaha na Viashiria katika sekta ya usalama kwa mwaka 2025/26 vimeainishwa katika **Jedwali 3.21** na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I.**IV. Uendelezaji wa Mji wa Serikali

**Jedwali 4.21: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Usalama**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Kiwango cha kupungua kwa uhalifu nchini (%) | 35 | 35 |
| 2. | Idadi ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa na NIDA | 34,080,610 | 34,100,000 |
| 3. | Idadi ya kampeni za amani zilizofanyika | 130 | 150 |
| 4. | Kiwango cha ushiriki wa jamii katika shughuli za usalama (%) | 55 | 60 |
| 5. | Idadi ya ajira zilizozalishwa katika miradi ya maendeleo | 31,000 | 33,000 |
| 6. | Mchango katika ajira (%) | 18.1 | 18.8 |
| 7. | Kiwango cha kupungua kwa ajali za barabarani (%) | 58 | 60 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Mambo ya Ndani*

iv. **Uendelezaji wa Mji wa Serikali**

Serikali itaendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba kwa kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi; Jumla ya gharama zitakazotumika katika ujenzi wa majengo ya Serikali awamu ya pili ni shilingi 738,945,024,353.75. Hadi kufikia Desemba 30, 2024 jumla ya **shilingi 54,703,424,818.49** ni madai ya malipo ya wakandarasi na washauri waelekezi yaliyowasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Wizara na Taasisi. Aidha, ujenzi wa awamu ya pili wa Mji wa Serikali unahusisha ujenzi wa miundombinu mingine ya kudumu ikiwemo maji safi, maji taka, umeme, gesi, mawasiliano, tehama, usalama, zimamoto na uokoaji na upandaji miti. Gharama za ujenzi wa miundombinu hiyo ni Shilingi 253,253,602,170.78.

v. **Kukabiliana na Maafa**

Serikali itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa Kituo cha Usimamizi wa Maafa ambao unahusisha ujenzi wa jengo la utawala, jengo la operesheni na mawasiliano ya dharura, Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura (Emergency Operation and Communication Centre – EOCC), kituo cha matangazo kwa umma na uzio. Ujenzi umekamilika kwa asilimia 51 na jumla ya shilingi bilioni 9.3 fedha za ndani zimetengwa kukamilisha ujenzi kwa awamu hii.

### 4.6.8 Sekta ya Mazingira na Maliasili Asilia

Katika mwaka wa fedha 2025/26, sekta ya mazingira itaendelea na utekelezaji wa programu na miradi 21 yenye lengo la kuimarisha utunzaji wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali asilia.

Miradi hii inajumuisha usimamizi jumuishi wa mfumo ikolojia na urejeshwaji wa uoto asili na hifadhi ya bioanuai; Mpango Jumuishi wa Kuimarisha Jamii Pamoja na Mifumo Ikolojia Katika Kustahimili Mabadiliko ya Tabianchi Kwenye Ukanda wa Misitu ya Miombo (Tanzania Bara) pamoja na Maeneo kame Zanzibar; Kujenga ustahimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi mkoani Kigoma; Kujenga uwezo wa kitaifa wa kuandaa taarifa za utekelezaji wa makubaliano ya Paris (Tanzania's Climate Enhanced Transparency Framework – ETF); na kukijanisha Jiji la Dodoma. **Jedwali 4.22** linaonesha Shabaha na Viashiria vya sekta ya Mazingira na Maliasili Asilia kwa mwaka 2025/26 na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I.**

**Jedwali 4.22: Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Mazingira na Maliasili Asilia**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Wastani wa Ukuaji (%) | 6 | 7 |
| 2. | Mchango katika Pato la Taifa kutokana na matumizi endelevu ya misitu, maji na rasilimali za bahari | 6 | 7 |
| 3. | Kiwango cha kupungua kwa uharibifu wa misitu (Reduced Deforestation Rate) (Ha.) | 469,420 | 234,710 |
| 4. | Maeneo ya misitu ya kibishara (commercial forest Plantation) yaliyoanzishwa (Ha) | 550,000 | 550,000 |
| 5. | Asilimia ya miradi mikubwa inayokidhi uchambuzi wa athari kwa mazingira (EIA) na kanuni za ukaguzi | 93 | 65 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Makamu wa Raisi Mazingira*

## 4.7 Kuendeleza Ujuzi

Katika mwaka 2025/26 kipaumbele kitakuwa katika miradi minne (4) ambapo kati ya miradi hiyo miwili (2) ni miradi ya kipaumbele. Orodha ya miradi itakayotekelezwa katika kuendeleza ujuzi imeainishwa katika **Kiambatisho I.**

Ili kuhakikisha ujuzi unaozalishwa una tija katika shughuli za uzalishaji sekta binafsi itaendelea kuwa mdau muhimu katika kuendelea kutoa ujuzi na kuainisha mahitaji ya elimu za ujuzi kulingana na soko la ajira. Sekta binafsi itashiriki katika vikao vya utatu vitakavyoamua aina za ujuzi hitajika katika soko la ajira na maeneo yanayohitaji kufanyiwa mafunzo ya kuongeza ujuzi hususani eneo la ukuzaji ujuzi kwa njia ya mafunzo kazini.

Wakala binafsi wa huduma za ajira watapewa kipaumbele ili kuhakikisha watafuta kazi wengi wanaunganishwa na waajiri ndani na nje ya nchi. Aidha, TaESA itaratibu wakala binafsi wa ajira ili kuhakikisha wanafanya kazi kwa kuzingatia taratibu na sheria za kazi.

Vyuo vya ufundi stadi kutoka sekta binafsi vitashiriki katika kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana watakaohitaji kujifunza ujuzi kwa ajili ya kujiajiri au kuajiriwa na hatimaye kushindana katika soko la ajira.

Serikali itahakikisha vikao vya utatu (Serikali, wafanyakazi na waajiri) vinawezeshwa kukutana mara kwa mara kulingana na matakwa ya sheria ili kusimamia sheria za kazi na kuzingatia kazi za staha. **Jedwali 4.23** linaonesha shabaha na viashiria vya sekta ya kuendeleza ujuzi kwa mwaka 2025/26 na orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na vipaumbele imeainishwa katika **Kiambatisho Na. I.**

**Jedwali 4.23 Shabaha na Viashiria katika Sekta ya Kuendeleza Ujuzi**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya waliopata mafunzo ya Uanagenzi (Apprenticeship) | 8,250 | 46,200 |
| 2. | Idadi ya waliopata mafunzo ya Utarajali (Internship) | 1,861 | 30,000 |
| | | | |

***Chanzo:*** *Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu)*



**Mpango huu ni kiungo baina ya mipango inayokamilika na mipango mipya inayotarajiwa kutekelezwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.**

SURA YA TANO

# *Ufuatiliaji, Tathmini na Vihatarishi*





## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaainisha mfumo mpya wa kusimamia utekelezaji wa mpango wa maendeleo, nguzo za mfumo wa ufuatiliaji na tathmini, muundo, hatua za utekelezaji wa nguzo kuu za mfumo, msingi wa ufuatiliaji na tathmini, pamoja na vihatarishi na mikakati ya kukabiliana navyo katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26. Lengo ni kufikia azma ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Mfumo huu utakuwa suluhisho la changamoto ya utekelezaji na uwajibikaji hafifu lililodumu kwa miongo mingi kwa Taifa.

## 5.2 Msingi wa Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26, utazingatia waraka, sheria na miongozo ya bajeti, ufuatiliaji na tathmini ikiwemo Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma Toleo la Mwaka 2022 (PIM-OM), Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Miradi na Programu za Maendeleo wa Mwaka 2022 na Mwongozo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mwaka 2024. Vilevile, mikakati pamoja na tathmini mbalimbali zilizofanyika zitazingatiwa katika ufuatiliaji na tathmini ikiwemo tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Miongozo hiyo imeainisha maelekezo mahsusi katika ufuatiliaji na tathmini, nyenzo zinazohitajika kukamilisha kazi za ufuatiliaji na tathmini, maandalizi ya viashiria vya utendaji na upimaji wa mchango wa kila taasisi katika kufikia malengo. Aidha, Wizara, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka zote za Serikali za Mitaa zinapaswa kuzingatia miongozo iliyotolewa katika eneo husika.

## 5.3 Nguzo za Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo huu umejengwa na nguzo kuu tatu zinazolenga kuhakikisha kuwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2025/26 unatekelezwa kwa ufanisi na ili kufikia matokeo yanayotarajiwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Nguzo hizo ni:

### 5.3.1 Kuainisha Vipaumbele:

Kutokana na ufinyu wa rasilimali, ni muhimu kuelekeza nguvu kwenye maeneo yenye tija kubwa zaidi kwa maendeleo ya Taifa. Maamuzi ya vipaumbele yatafanyika kwa njia shirikishi na katika ngazi ya juu Serikalini ili kuimarisha uwajibikaji na uungwaji mkono katika utekelezaji. Mfumo huu unahuisha kauli ya Baba wa Taifa: *"Maendeleo ni kupanga na kupanga ni kuchagua."*

### 5.3.2 Nidhamu ya Utekelezaji:

Ili kuepuka tofauti za uwezo wa utekelezaji miongoni mwa watendaji, mfumo huu umeweka mbinu za ufuatiliaji na utatuzi wa changamoto mapema kabla hazijageuka kuwa vikwazo. Pia, unajenga mazingira ya mashauriano ya wadau mbalimbali ili kuhakikisha utekelezaji unafanyika kwa ufanisi na kwa wakati.

### 5.3.3 Uwajibikaji:

Uwajibikaji unajengwa katika uwazi na usimamizi madhubuti. Malengo na matokeo ya utekelezaji yatawekwa wazi kwa umma kila mwaka ili kuwezesha wananchi kudai maendeleo. Viongozi wa Serikali, hususan mawaziri wa maeneo ya vipaumbele,

wataingia mikataba ya uwajibikaji na Rais na kuhakikisha majukumu yanasambazwa kwa watendaji wa chini. Hii itatoa nafasi kwa umma kupima maendeleo na kuwezesha hatua stahiki kuchukuliwa kwa watekelezaji wasiofikia malengo.

Kupitia mfumo huu, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2025/26 utajengwa juu ya misingi imara ya utekelezaji bora, uwajibikaji wa hali ya juu, na usimamizi makini wa rasilimali za umma ili kufanikisha maendeleo endelevu na shirikishi kwa wananchi wote.

## 5.4 Njia za Utekelezaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo huu unatekelezwa kupitia hatua nane muhimu zinazolenga kuongeza ufanisi, uwazi, na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya kipaumbele.

### 5.4.1 Kuainisha Dira:

Serikali kupitia FYDP III imeweka wazi sekta za kipaumbele zitakazofuatiliwa kupitia mfumo huu ambapo Mhe. Rais na Baraza la Mawaziri waliridhia vipaumbele vya Taifa kama vilivyoainishwa katika Mpango wa 2025/26. Hivyo, watashiriki kikamilifu katika kutatua changamoto zitakazojitokeza wakati wa utekelezaji.

### 5.4.2 Maabara za Uchambuzi:

Wadau mbalimbali, wakiwemo wataalam, sekta binafsi, na taasisi za utafiti, watakutana na kuchambua changamoto na kutengeneza suluhisho madhubuti. Maabara hizi zitatengeneza mpango wa utekelezaji, vigezo vya kupima matokeo (KPIs), majukumu ya wadau, na makadirio ya gharama. Mapendekezo yao yatapitiwa na kuridhiwa na Serikali kabla ya utekelezaji.

### 5.4.3 Uhamasishaji wa Umma:

Katika kuongeza uwajibikaji na ushirikishaji wananchi, Serikali itawasilisha kwenye Mpang kipaumbele, changamoto zinazoshughulikiwa, matokeo tarajiwa, na gharama. Hii itaimarisha uwazi na kuweka msingi wa uwajibikaji kwa umma kudai matokeo yaliyoahidiwa.

### 5.4.4 Malengo ya Utekelezaji (KPIs):

Katika hatua hii, Serikali itaweka malengo mahsusi ya miradi, na Mawaziri wa sekta husika watasaini makubaliano na Mhe. Rais kuthibitisha dhamira ya kusimamia utekelezaji. Hatua hii inaweka uwajibikaji wa moja kwa moja kwa viongozi wa sekta husika.

### 5.4.5 Mpango wa Utekelezaji:

Mwongozo wa utekelezaji wa miradi ya kipaumbele utaandaliwa na kusambazwa kwa wadau. Huu utabainisha nini kitafanyika, lini, kwa gharama gani, nani atasimamia, na vigezo vya upimaji wa matokeo.

### 5.4.6 Utekelezaji:

Utekelezaji wa miradi utafanywa na Wizara husika kwa kushirikiana na taasisi zake, huku Tume ya Taifa ya Mipango (TTM) na vitengo vya M&E vikisimamia maendeleo ya utekelezaji. Kila Wizara itatakiwa kuandaa ripoti ya utekelezaji kila wiki kwa ajili ya Waziri husika na TTM, ikieleza hatua iliyofikiwa, changamoto, na mapendekezo ya utatuzi. Changamoto zinazohitaji maamuzi ya juu zitapelekwa kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu au Baraza la Mawaziri.

### 5.4.7 Uhakiki wa Matokeo:

Matokeo ya utekelezaji yatapitiwa na taasisi huru ili kuhakikisha uwazi na ukweli wa taarifa. Tathmini itafanywa na wataalam wa kimataifa wenye uzoefu wa kusimamia maendeleo.

### 5.4.8 Ripoti ya Utekelezaji kwa Wananchi:

Serikali itatoa ripoti ya kila mwaka kwa umma, ikilinganishwa na ahadi zilizotolewa. Hatua za haraka zitachukuliwa pale ambapo utekelezaji haujafikia malengo ili kuhakikisha uwajibikaji wenye matokeo chanya.

Mfumo huu unalenga kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali, na kujenga uwajibikaji wa kweli kwa viongozi na taasisi zinazotekeleza mpango huu.

## 5.5 Muundo wa Kitaasisi wa Ufuatiliaji na Tathmini

Ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa, Serikali iliridhia mfumo wa kitaasisi unaowezesha kuzingatia misingi mitatu iliyotajwa awali.

**Kielelezo 5.1: Muundo wa Kitaasisi wa Mfumo Mpya Kusimamia Utekelezaji wa Miradi**



Muundo huu umejengwa katika ngazi kuu tatu (3), kila moja ikiwa na jukumu maalum katika kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa ufanisi, uwazi, na uwajibikaji.

**Ngazi ya Kwanza:** Uongozi na Mwelekeo wa Kimkakati. Ngazi hii inahusika na utoaji wa mwelekeo wa programu na utekelezaji wake. Inajumuisha uainishaji wa vipaumbele vya Taifa, kutatua changamoto za kisera, na kusimamia uwajibikaji kwa ujumla. Ngazi hii inaongozwa na viongozi wa juu wa Serikali, wakiwemo Rais na Baraza la Mawaziri.

**Ngazi ya Pili:** Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utekelezaji. Hii ni ngazi ya tathmini, usimamizi wa utekelezaji, na utatuzi wa changamoto za kiutekelezaji. Inafanya kazi kama kiungo kati ya watekelezaji wa miradi na viongozi wa kisera. Katika ngazi hii, taasisi kama Tume ya Kitaifa ya Mipango (TTM), vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini (M&E Units), na kamati za uratibu hufuatilia maendeleo ya miradi, kuchambua changamoto zinazojitokeza, na kupendekeza suluhisho kwa wakati.

**Ngazi ya Tatu:** Utekelezaji wa Miradi. Hii ni ngazi ya utekelezaji halisi wa miradi ya kipaumbele. Wizara, taasisi, na mamlaka zinazohusika zinahakikisha kuwa miradi inatekelezwa kwa mujibu wa mipango, bajeti, na vigezo vya utendaji vilivyowekwa. Ripoti za maendeleo huwasilishwa mara kwa mara kwa ngazi ya pili ili kurahisisha ufuatiliaji na marekebisho ya utekelezaji pale inapobidi.

## 5.6 Vihatarishi vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa

Ili kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2025/26, Serikali itadhibiti vihatarishi kwa kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekta ya Umma (2023). Vihatarishi hivyo vimegawanyika katika makundi mawili: (i) vya ndani vinavyotokana na utendaji au mifumo ya Serikali, na (ii) vya nje ambavyo Serikali haina udhibiti wa moja kwa moja.

### 5.6.1 Vihatarishi vya Ndani na Nje

Vihatarishi vya Ndani: Serikali imeweka mikakati ya kudhibiti kutokea au kukabili athari za vihatarishi hivi. Uchambuzi wa vihatarishi vya ndani, ikiwemo ukosefu wa mipango madhubuti ya utekelezaji, kutokuwepo kwa KPIs sahihi, ukosefu wa mifumo ya uwajibikaji na ufuatiliaji, na vitendo vya rushwa, umeainishwa katika **Jedwali 5.1**.

**Jedwali Na.5.1: Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana Navyo**

| Na. | Nguzo | Vihatarishi | Athari | Njia za Kuzuia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **Kuainisha Vipaumbele** | Vipaumbele kutoandaliwa au kuandaliwa bila kufuata mipango ya kitaifa mfano mpango wa miaka 5 | Kutokuwepo kwa mwendelezo wa utekelezaji wa miradi na matumizi mabaya ya rasilimali | Kuhakikisha vipaumbele vinaandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP) |
| 2. | **Nidhamu ya utekelezaji** | Kukosekana kwa mpango wa kina wa utekelezaji | Utekelezaji wa miradi kuwa wa kusuasua au kutofikiwa kwa malengo | Kutayarisha mpango wa utekelezaji unaoeleza hatua, muda, na wajibu wa kila mshiriki |

| Na. | Nguzo | Vihatarishi | Athari | Njia za Kuzuia |
|---|---|---|---|---|
| 3. | | Kukosekana kwa KPIs katika utekelezaji wa mpango au KPIs zisizoendana na mpango elekezi wa muda mrefu. | Kutoweza kupima maendeleo na mafanikio ya utekelezaji wa miradi | Kuainisha KPIs mahsusi zinazohusiana moja kwa moja na mpango elekezi |
| 4. | | Kukosekana kwa taarifa za utekelezaji wa miradi za kila wiki, mwezi na robo mwaka au kutotumiwa ipasavyo | Utekelezaji wa miradi kuwa na changamoto zisizogundulika kwa wakati, na ucheleweshaji wa ufumbuzi wa changamoto | Kuweka mfumo wa kisheria wa utoaji wa taarifa za utekelezaji |
| 5. | **Uwajibikaji** | Kukosekana kwa uwajibikaji kupitia vikao vya kila wiki, mwezi, na robo mwaka | Kukosa mawasiliano mazuri, ucheleweshaji wa maamuzi, na kupungua kwa ufanisi wa utekelezaji wa miradi | Kuanzisha mfumo wa uwajibikaji wa kisheria na kitaasisi |
| 6. | | Taarifa za wiki, mwezi, robo, nusu na mwaka n.k zisizoainisha matatizo na hatua za utatuzi katika ngazi mbalimbali za ufanyaji maamuzi | Maamuzi yasiyo sahihi au yasiyo na msingi wa takwimu na ushahidi | Kuweka mfumo wa lazima wa kuonyesha matatizo na hatua za utatuzi katika taarifa zote<br>Kuhakikisha vikao vya tathmini vinajumuisha majadiliano juu ya changamoto na suluhisho |
| | | | | |

**Vihatarishi vya Nje:** Mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko; mitikisiko na mdororo wa kiuchumi duniani; kuongezeka kwa kiwango cha riba katika masoko ya kimataifa; migogoro na hali ya siasa inayojitokeza kwa nchi jirani, kikanda na kimataifa; kuongozeka kwa kasi ya mabadiliko ya teknolojia; na kupungua kwa mwenendo wa mikopo yenye masharti nafuu na misaada. Uchambuzi wa vihatarishi vya nje pamoja na mikakati ya kukabiliana navyo umeainishwa katika **Jedwali 5.2.**

**Jedwali Na.5.2: Vihatarishi vya Nje na Mikakati ya Kukabiliana Navyo**

| Na. | Kihatarishi | Athari | Mikakati |
|---|---|---|---|
| 1. | **Mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko** | i. Kupungua kwa uzalishaji; na<br>ii. Rasilimali fedha kuelekezwa katika kukabiliana na majanga badala ya kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo kama ilivyokusudiwa. | i. Kuboresha mifumo ya kuzuia na kukabiliana na majanga;<br>ii. Kuimarisha mifuko ya maafa;<br>iii.Kutekeleza na kuendelea kuridhia itifaki za kimataifa kuhusu utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi; na<br>iv. Kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya |

| Na. | Kihatarishi | Athari | Mikakati |
|---|---|---|---|
| 2. | **Mitikisiko na mdororo wa kiuchumi duniani unaoweza kusababisha kupungua kwa mwenendo wa mikopo yenye masharti nafuu na misaada; kuongezeka kwa kiwango cha riba katika masoko ya kimataifa; n.k.** | i. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi; na<br>ii. Kuathiri mapato ikiwemo mapato ya kodi yatokanayo na kipato.<br>iii.Miradi kutotekelezwa kama ilivyopangwa kutokana na ukosefu wa fedha za ugharamiaji | i. Kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia uwekezaji wa ndani na wa kigeni kupitia sera thabiti za uchumi na kodi.<br>ii. Kudhibiti Matumizi ya Serikali na Kuboresha Ufanisi wa Bajeti<br>iii.Kuunda sera za kiuchumi zinazoweza kujibadilisha kulingana na mabadiliko ya kimataifa, kama vile kuimarisha akiba ya fedha za kigeni.<br>iv. Serikali kuendelea na majadiliano na jumuiya za kimataifa ili kuweza kupata fursa za mikopo yenye masharti nafuu.<br>v. kuchukua mikopo ya muda mrefu yenye masharti nafuu ili kuepuka athari ya kupanda kwa viwango vya riba; na<br>vi. kuimarisha mikakati ya kisera ili kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi duniani ikijumiisha kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, kama zao la ngano |
| 3. | **Migogoro ya kisiasa na mahusiano ya kidiplomasia** | i. Kudhoofika kwa Biashara na Masoko ya kikanda na kimataifa<br>ii. Kupungua kwa Uwekezaji, na kuathiri utalii | i. Kuendelea kuimarisha ushirikiano na nchi jirani, kikanda na kimataifa ili kukuza masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa viwandani; na<br>ii. Kutafuta masoko mbadala kwa bidhaa za viwandani na za kilimo ili kupunguza utegemezi mkubwa kwa nchi zilizo katika migogoro.<br>iii.Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni<br>iv. Kukuza masoko ya mitaji ya ndani |
| 4. | **Kuongezeka kwa kasi ya mabadiliko ya teknolojia** | i. Mifumo ya kisheria, kisera, na kitaasisi iliyopo kutoendana na mabadiliko ya teknolojia hivyo kuongezeka kwa gharama za uwekezaji katika mifumo ya teknolojia mpya; na<br>ii. Kupungua kwa uwezo wa kiushindani katika soko la kikanda na kimataifa.<br>iii.Matumizi ya roboti na Akili Mnemba yanaweza kuathiri upatikanaji wa ajira na uwezo wa watu kufikiri | i. Kuendelea kuboresha mifumo ya kisheria, kisera na kitaasisi ili iendane na mabadiliko ya teknolojia duniani; na<br>ii. Kuendelea kuimarisha mikakati ya kuongeza ujuzi, uhawilishaji wa teknolojia na kuhamasisha ubunifu wa teknolojia kwa wataalam wa ndani.<br>iii.Kuboresha elimu na mafunzo ya ujuzi mpya, kuhimiza ubunifu na ujasiriamali na kuhakikisha kuna kuwa na sera madhubuti za ajira na teknolojia |

| Na. | Kihatarishi | Athari | Mikakati |
|---|---|---|---|
| 5. | **Mabadiliko ya sera za washirika wa maendeleo** | i. Kupungua kwa misaada ya fedha za kutekeleza programu na miradi ya maendeleo<br>ii. Mabadiliko katika Masharti ya Ufadhili<br>iii.Kubadilika kwa Vipaumbele vya Maendeleo | i. Kuendelea kuimarisha mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani;<br>ii. Kutumia vyanzo mbadala vya kugharamia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo;<br>iii.Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni; na<br>iv. Kufanya tathmini ya athari zinazoweza kujitokeza kufuatia kusitishwa kwa utoaji wa fedha za misaada kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo la Kimataifa (USAID). |
| | | | |

# Kiambatisho Na. I

**Orodha ya Miradi kwa Sekta Itakayotekelezwa kwa Mwaka 2025/26**

| Na. | Namba ya Mradi | Jina la Mradi | Gharama kwa 2025/26 |
|---|---|---|---|
| 1 | 4001 | Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe | 3,200,000,000 |
| 2. | 4002 | Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi | 56,301,340,000 |
| 3. | 4004 | Barabara ya Nachingwea – Liwale – (km 175) na Liwale - Kihangara (Design & Build) | 3,200,000,000 |
| 4. | 4031 | Upanuzi wa barabara zinazoingia na kutoka katika Jiji la Dodoma | 22,399,780,000 |
| 5. | 4032 | Barabara ya Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Jct | 5,500,000,000 |
| 6. | 4005 | Barabara ya Ubena – Zomozi – Ngerengere | 2,000,000,000 |
| 7. | 4011 | Barabara ya Iringa – Ruaha National Park | 49,900,290,000 |
| 8. | 4037 | Barabara ya Mafinga – Mgololo | 2,500,000,000 |
| 9. | 4101 | Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge | 50,499,495,996 |
| 10. | 4029 | Barabara ya Sengerema – Nyehunge – Kahunda | 2,500,000,000 |

| Na. | Namba ya Mradi | Jina la Mradi | Gharama kwa 2025/26 |
|---|---|---|---|
| 11. | | Mradi wa Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Mapato ya Ndani (IDRAS) | 127,935,339,520 |
| 12. | 4041 | Barabara ya Kitai – Lituhi including Mnywamaji Bridge (90 km) | 4,033,355,360 |
| 13. | 4017 | Daraja la Ugalla | 550,000,000 |
| 14. | 4112 | Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 165) | 34,121,600,000 |
| 15. | 4146 | Ujenzi wa Barabara za mzunguko katika Jiji la Dodoma (km 112.3) | 60,538,480,000 |
| 16. | 4129 | Ukarabati wa Barabara ya Isaka – Lusahunga yenye urefu wa km 392 | 2,107,219,000 |
| 17. | 4170 | Ukarabati na matengenezo ya barabara nchini | 688,756,470,000 |
| 18. | 4161 | Barabara katika jiji la Dar es Salaam, madaraja ya iuu na barabara unganishi | 510,000,000 |
| 19. | 4164 | Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi | 40,230,044,000 |
| 20. | 4165 | Mafia Airport Access Road (km 16) | 2,000,000,000 |
| 21. | 4018 | Daraja la Kitengule na Barabara unganishi | 2,010,000,000 |
| 22. | 4285 | Barabara za Mwendo Kasi (BRT) Jijini Dar es Salaam ((Phase IV): Alli Hassan Mwinyi - Morocco - Mwenge - Tegeta; Mwenge – Ubungo) | 135,714,564,883 |
| 23. | 4285 | Barabara za Mwendo Kasi (BRT) Jijini Dar es Salaam ((Phase IV): Alli Hassan Mwinyi - Morocco - Mwenge - Tegeta; Mwenge – Ubungo) | 107,121,580,000 |
| 24. | 4286 | Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato | 114,866,660,000 |
| 25. | 4022 | Barabara ya Njombe – Makete – Isyonje | 3,320,000,000 |
| 26. | 4199 | Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma na Mbeya Bypass | 5,300,000,000 |
| 27. | 4027 | Barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ndembo (km 90.1) | 3,200,000,000 |
| 28. | 4040 | Barabara ya Singida - Sepuka - Ndago – Kizaga | 3,500,000,000 |
| 29. | 4039 | Barabara ya Kongwa - Kibaya - Arusha (km 453.42); Arusha Mjini (T/Packers/Mbauda Jct) – Losinyai | 2,500,000,000 |
| 30. | 4042 | Access Roads to SGR Stations | 8,890,000,000 |
| 31. | 4103 | Barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 133.9) | 6,033,442,000 |
| 32. | 4133 | Upanuzi wa Barabara ya Mwanza - Usagara - JPM Bridge kuwa njia mbili (km 37) | 2,500,000,000 |
| 33. | 4113 | Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke – Kibena (Njombe) km 346.43 | 7,260,480,000 |
| 34. | 4195 | Barabara ya Dodoma – Iringa (km 267.1) | 4,810,000,000 |

| Na. | Namba ya Mradi | Jina la Mradi | Gharama kwa 2025/26 |
|---|---|---|---|
| 35. | 4193 | Handeni – Kibirashi –Kibaya – Njoro – Goima – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro - Singida Lot 1 & 2 | 6,500,000,000 |
| 36. | 4003 | Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.5) | 2,200,000,000 |
| 37. | 4006 | Barabara ya Tamco – Vikawe – Mapinga | 2,000,000,000 |
| 38. | 4007 | Barabara ya Makofia – Mlandizi | 660,000,000 |
| 39. | 4008 | Barabara ya Musoma – Makojo – Busokela Lot 1 | 1,510,000,000 |
| 40. | 4010 | Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba | 1,000,000,000 |
| 41. | 4012 | Barabara ya Muheza – Amani | 880,000,000 |
| 42. | 4013 | Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (Lot 1&2) | 7,109,977,000 |
| 43. | 4014 | Barabara ya Kibaoni – Majimoto – Muze – Kilyamatundu | 3,800,000,000 |
| 44. | 4016 | Daraja la Mzinga | 275,000,000 |
| 45. | 4019 | Barabara ya Morogoro – Dodoma na Daraja la Mkundi | 2,750,000,000 |
| 46. | 4023 | Barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105) | 2,999,002,900 |
| 47. | 4024 | Barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (108.9) | 6,250,000,000 |
| 48. | 4025 | Barabara ya Mpemba – Isongole | 2,659,000,000 |
| 49. | 4026 | Barabara ya Ruanda – Iyula – Nyimbili | 1,000,000,000 |
| 50. | 4028 | Barabara ya Uyogo – Nyamilagano – Nyandekwa – Kahama | 1,050,000,000 |
| 51. | 4030 | Barabara ya Omurushaka – Nkwenda – Mirongo (km 125) (Sehemuy a Kyerwa – Chonyonyo km 50) | 2,200,000,000 |
| 52. | 4033 | Barabara ya Mugumu – Tarime | 5,200,000,000 |
| 53. | 4034 | Barabara ya Shelui -Nzega | 1,550,000,000 |
| 54. | 4035 | Barabara ya Nzega – Kagongwa | 550,000,000 |
| 55. | 4036 | Barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu | 4,000,000,000 |
| 56. | 4038 | Nyololo – Mtwango (km 40.4) | 550,000,000 |
| 57. | 4102 | Barabara ya Kisarawe – Maneromango | 1,500,000,000 |
| 58. | 4104 | Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke | 2,400,000,000 |

| Na. | Namba ya Mradi | Jina la Mradi | Gharama kwa 2025/26 |
|---|---|---|---|
| 59. | 4105 | Barabara ya Geita – Nzera (Sungusila – Nzera) – Nkome section (km 54) | 1,800,000,000 |
| 60. | 4106 | Barabara ya Arusha – Moshi- Himo – Holili (km 199.51) | 17,809,860,000 |
| 61. | 4107 | Access Roads to Rufiji Hydropower project (km 760.9) | 4,800,000,000 |
| 62. | 4108 | Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro – Dodoma Expressway | 3,541,000,000 |
| 63. | 4109 | Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 118.1) | 1,000,000,000 |
| 64. | 4111 | Nyakahura–Kumubuga–Rulenge – Kabanga Nickel Road (FS & DD) (km 141.0) | 3,000,000,000 |
| 65. | 4114 | Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389) | 7,000,000,000 |
| 66. | 4115 | Marangu–Tarakea–Rongai–Kamwanga/ Bomang'ombe – Sanya Juu(km 105.16) | 5,830,000,000 |
| 67. | 4116 | Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 60.6). Lot 3 & 4 | 4,110,000,000 |
| 68. | 4118 | Barabara ya Dodoma- Manyoni | 7,799,970,000 |
| 69. | 4119 | Tabora – Mambali – Bukene – Itobo (km 114,5) | 500,000,000 |
| 70. | 4121 | Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8) | 1,000,000,000 |
| 71. | 4123 | Dumila – Kilosa – Mikumi (km 141) | 520,000,000 |
| 72. | 4124 | Sumbawanga – Matai – Kasanga Port Lot 1&2 (km 107) | 4,610,000,000 |
| 73. | 4126 | Ujenzi, ukarabati na usanifu wa madaraja yapatayo 38 | 19,330,000,000 |
| 74. | 4128 | Kyaka – Bugene – Kasulo (km 156.6) | 4,010,000,000 |
| 75. | 4130 | Ujenzi wa mizani katika barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 256.75) katika eneo la Kizengi | 12,129,880,000 |
| 76. | 4132 | Ukarabati na matengenezo ya barabara katika mikoa yote 26 | 61,585,000,000 |
| 77. | 4141 | Barabara ya Nyamuswa - Bunda - Kisorya | 520,000,000 |
| 78. | 4142 | Barabara ya Kolandoto – Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi sehemu za Kolandoto - Kishapu – Lalago (km 64) na Iguguno – Shamba – Nduguti – Mkalama km 89 | 2,004,000,000 |
| 79. | 4163 | Barabara ya IPole - Rungwa | 1,000,000,000 |
| 80. | 4143 | Ujenzi na ukarabati katika Barabara ya Ndundu - Somanga | 3,810,200,000 |
| 81. | 4145 | Barabara ya Kasulu – Manyovu (km 68) | 3,275,249,000 |

| Na. | Namba ya Mradi | Jina la Mradi | Gharama kwa 2025/26 |
|---|---|---|---|
| 82. | 4147 | Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499) | 5,000,000,000 |
| 83. | 4149 | Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu | 10,220,000,000 |
| 84. | 4150 | Barabara ya Ibanda – Itungi Port | 4,020,000,000 |
| 85. | 4152 | Barabara ya Nzega – Tabora | 1,220,000,000 |
| 86. | 4154 | Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi Road (km 803.6) | 40,590,050,000 |
| 87. | 4155 | Barabara ya Nyanguge - Musoma / Kisesa Bypass | 1,530,000,000 |
| 88. | 4160 | Magole – Mziha – Handeni (km152.8) | 1,010,000,000 |
| 89. | 4167 | Ujenzi wa Daraja jipya la Nyerere (Kigamboni) na barabara unganishi | 2,030,000,000 |
| 90. | 4184 | Barabara ya Ulemo - Kinampanda - Gumanga – Mkalama, Upanuzi wa Barabara katika mlima Sekenke na ujenzi wa Barabara ya Singida mjini - Ilongero - Haydom Road (93km) Sehemu ya Igauri – Ilongero | 3,900,000,000 |
| 91. | 4185 | Barabara ya Mbagala (Kilwa Road) kuanzia Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 10.8) | 8,010,000,000 |
| 92. | 4187 | Ukarabati wa Barabara ya Korogwe - Mkumbara – Same – km 239 (Lots 1&2) | 6,000,000,000 |
| 93. | 4188 | Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Manyoni Lots 7A, 7B, ikiwemo barabara ya Itigi mjini, Mbalizi – Makongolosi na sehemu ya barabara ya Makongolosi – Rungwa | 8,313,202,200 |
| 94. | 4190 | Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda sehemu ya Itoni – Lusitu, | 4,010,000,000 |
| | | Lot 3: Mawengi - Ludewa – Manda na Barabara ya Nkomang'ombe – Mchuchuma (7km) | |
| 95. | 4194 | Barabara ya Makambako – Songea, Makambako (Lwangu) – Songea; Lot 3: Lutukila – Songea (km 95.18), Makambako – Lutikila (km 184) na Sehemu ya Ramadhani – Itulike | 22,999,790,000 |
| 96. | 4196 | Barabara ya Dodoma – Babati | 1,930,000,000 |
| 97. | 4156 | Kiwanja cha Ndege cha Kigoma | 22,910,240,000 |
| 98. | 4159 | Kiwanja cha Ndege cha Tabora | 12,728,670,000 |
| 99. | 4206 | Kiwanja cha Ndege cha Songwe | 4,317,370,000 |
| 100. | 4209 | Kiwanja cha Ndege cha Mwanza | 4,380,570,000 |
| 101. | 4221 | Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga | 16,540,200,000 |
| 102. | 4222 | Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga | 12,763,270,000 |

| Na. | Namba ya Mradi | Jina la Mradi | Gharama kwa 2025/26 |
|---|---|---|---|
| 103. | 4226 | Ujenzi wa Viwanja vya Ndege Sita (6) vya Mikoa | 15,359,578,450 |
| 104. | 4125 | Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko | 2,929,075,400 |
| 105. | 4138 | Barabara za kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam | 9,781,490,000 |
| 106. | 4139 | Ununuzi wa Vivuko Vipya | 9,691,280,000 |
| 107. | 4144 | Ukarabati wa Vivuko | 11,587,630,000 |
| 108. | 6327 | Ujenzi wa Nyumba na Majengo ya Serikali | 28,897,228,600 |
| 109. | 4168 | Upembuzi na Usanifu wa kina (FS&DD) Barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma - km 215.8 | 3,300,000,000 |
| 110. | 4172 | Upanuzi wa barabara ya Kimara - Kibaha | 500,200,000 |
| 111. | 4175 | Uboreshaji wa barabara ya Kisarawe – Mlandizi | 800,000,000 |
| 112. | 4178 | Uboreshaji wa barabara ya Pugu - Bunju | 1,000,000,000 |
| 113. | 4197 | Barabara ya Masasi - Songea - Mbamba Bay | 690,000,000 |
| 114. | 4162 | Barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi | 30,000,000 |
| 115. | 4148 | Barabara ya Tabora -Ipole Koga – Mpanda | 17,036,130,000 |
| 116. | 4186 | Ukarabati wa barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni - Mafinga (TANZAM) | 2,510,000,000 |
| 117. | 4198 | Barabara inayoingia to Uongozi Institute | 220,000,000 |
| 118. | 6304 | Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya ICoT | 2,000,000,000 |
| 119. | 6383 | Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya TANROADS | 4,070,210,000 |
| 120. | 4009 | Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe | 3,500,000,000 |
| 121. | 4021 | Mradi wa Barabara zinazoelekea kwenye maeneo yenye shughuli za kiuchumi (Tanzania Roads to Inclusion and Socioeconomic Opportunities (RISE) Program) | 24,073,918,240 |
| 122. | 4170 | Mradi wa kusaidia ukarabati na matengenezo ya Barabara (Support-Road Maintanance and Rehabilitation) | 710,316,035,000 |
| 123. | 6370 | Mradi wa miundombinu ya kubadilisha Miji ya Tanzania kuwa shindani (Tz Cities Transorming Infrast. and Competitiveness) | 140,200,481,008 |
